Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Nne – Tarehe 18 Juni, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MAKAMU MWENYEKITI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 25

**Kugawanya kwa Mabaraza ya Halmashauri ya Msalala**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Wilaya ya Kahama ina Halmashauri moja ya Wilaya ambayo, ni kubwa yenye Kata 55 na Baraza lenye Madiwani 75. Tangu mwaka 2011 Serikali ilishatangaza kuanzisha Halmashauri zingine tatu za Msalala, Ushefu na Hlamsahauri ya Mji wa Kahama kwa kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama:-

(a) Je, Halmashauri ya Msalala itaanza rasmi lini?

(b) Je, Serikali inaweza kuruhusu Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Kahama, kujigawa katika Mabaraza madogo matatu ya Msalala, Ushefu na Halmashauri ya Mji wakati wa kujadili masuala ya maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kwell kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ni kubwa yenye Kata 55 na Baraza la Madiwani lenye Madiwani 74 na Wabunge 2, na sio Madiwani 75 kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Aidha, ni kweli kwamba, mwaka 2011 Serikali ilitangaza kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama katika Halmashauri nyingine 3 za Msalala, Ushefu na Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Spika, suala la kuanzisha Halmashauri ya Msalala, linafanywa kwa mujibu wa Sheria Namba 7 ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, Kifungu cha 7 (1-4) ambacho, kinaeleza Waziri mwenye dhamana atatangaza dhamira ya Serikali ya kusudio la kuanzisha Halmashauri katika Gazeti la Serikali na Magazeti ya kawaida. Pia atatoa siku 60 kwa wadau kuwasilisha kwa maandishi, maoni, ushauri na pingamizi, kuhusiana na uanzishwaji wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ni miongoni mwa Halmashauri Mpya ambazo zipo katika hatua ya maelezo ya Kijiografia *(Geographical Boundaries)* kwa maana ya mgawanyo wa Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji/Mitaa, ili kuweza kutangaza kusudio la kuanzisha katika Gazeti la Serikali na Magazeti ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Msalala, itaanza rasmi sambamba na Halmashauri nyingine mpya zinazotarajiwa kuanzishwa baada ya kutekekeleza taratibu kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, Kifungu 7 (1-4).

(b) Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri zinazotarajiwa kuanzishwa ya Msalala na Ushefu, yataanza kujadili na kutekeleza majukumu yake baada ya taratibu za kuanzishwa rasmi kukamilika, yaani zitakapokuwa na Mamlaka Kamili *(Corporate Body).* Kwa kuwa, mchakato wa kuanzisha Halmashauri ya Msalala na Ushetu haijakamilika ni dhahiri kwamba, Baraza la Madiwani la Wilaya litaendelea kutumika hilohilo ambalo lipo kwa sasa hivi, mpaka taratibu zitakapokamilika.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa na swali moja dogo la nyongeza kwamba, kwa kuwa, Baraza hili la Wilaya ya Kahama ni kubwa, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amekiri. Na ni kubwa katika kiwango ambacho si cha kawaida. Tumekuwa tukiomba ikiwezekana Madiwani hao wanaokaa muda mrefu, angalao siku 2 kwa Vikao vya kawaida ili kupata muda wa kujadili vizuri Bajeti zao.

Je, Serikali walao iko tayari kuruhusu suala hilo kufanyika ili, kuwapa Madiwani kujadili vizuri masuala ya Halmashauri yao kabla ya kugawanywa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nime-*quote* hizi Sheria nilizozieleza hapa, ninaelewa *concern* ya Mheshimiwa Ezekiel Maige na ninampongeza sana kwa namna anavyosukuma jambo hili, anajaribu sana kila wakati kuhakikisha tunakwenda kwa mwendo ule ambao wananchi wote wanataka tupate kasi. Lakini maamuzi yote yanayofanywa na Mabaraza haya, kama hayatazingatia hizi taratibu nilizozisema hapa, watafanya maamuzi pale, watakwenda kutoza kodi

pale, watapanua eneo pale, watafanya maamuzi yoyote watakayoyafanya pale, kwa sasa hivi ni lazima yabaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, kufanya mabadiliko yoyote pale itakuja hapa tayari utasikia maswali yanaanza kuulizwa hapa kwamba, ilikuwakuwaje wakafanya hivyo? Kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kwamba, sisi tunafanya kila linalowezekana sasa hivi kwa sababu, pale kuna Ushetu inaanzishwa pale na kuna Msalala inaanzishwa pale na kuna Mji wa Kahama ambao umeanzishwa pale, sasa taratibu zile za kujua *geographical boundaries* zake na mambo mengine yote haya, ndio tunayazingatia ili waweze kuanza. Lakini awe na amani kwamba, hili jambo linakwenda vizuri sana.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais, ametupatia Mkoa mpya na pia ameweka Wilaya mpya na hususan Itirima, ambako tuna Halmashauri mpya. Ni lini hizi Halmashauri zitaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cheyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hizi Wilaya anazozizungumzia, kuna makundi mawili hapa, kuna wale wa Kahama wa Masasi na wale wengine wale ambao wanaingia katika *Town Council.* Kundi analolizungumzia Mheshimiwa Cheyo, ni kundi la hizi Wilaya 19 ambazo zimeanzishwa *plus* hizo Halmashauri mbili za Ushetu pamoja na ile ya Msalala ambazo, zinakuwa 21.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Rais, amekwisha kuteua Wakuu wa Wilaya katika hizo Wilaya unazozungumza. Hii mimi nilitegemea kwamba, tutampongeza sana Mheshimiwa Rais kwamba, amekwenda *fast,* tayari ameshaweka watu pale ambao sasa ndio watakuwa wanasimamia utaratibu mzima wa kuhakikisha kwamba, sasa kunakuwa na Halmsahauri hizo zinazozungumzwa hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuanza kwa kweli kimsingi kumeshaanza. Sasa tunapokwenda kwenye hatua ya pili, tunazungumzia sasa Halmashauri, Halmashauri nayo ina Sheria yake, nimei-*quote* hapa; watakwenda kuangalia mipaka, watakwenda kuangalia wananchi wale wanatakiwa wakae wa-*discuss.*

Unakwenda kugawa nchi ya watu pale, lazima waseme sawa sawa, hizi Kata sawa sawa na hizi Tarafa sawa sawa na hivi Vijiji sawa sawa na hii Mitaa iliyoko humu sawa sawa. Huwezi tu ukagawa hivi hivi ukasema sisi tumegawa, aah, ndicho kinachoendelea na Mheshimiwa Cheyo, wala usiwe na wasi wasi, mambo yako safi. *(Makofi)*

Na. 26

**Walimu Kujiendeleza Kitaaluma**

**MHE. RACHEL M. ROBERT** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwasisitiza Walimu nchini wajiendeleze kitaaluma, ili pale anapogota mwisho wa ngazi za mshahara katika kiwango hicho cha elimu alichonacho. Kwa mfano Mwalimu wa Daraja III A anatakiwa kujiendeleza kufikia ngazi ya Stashahada au Shahada, ili atoke kwenye ngazi ya mshahara wa *TGTS E* kwenda *TGT S* na kuendelea.

Kwa hali hiyo, Walimu wengi wa Mkoa wa Shinyanga waliojiendeleza kitaaluma kufikia kustahili kupandishwa viwango vya mshahara wamejikuta wakirudishwa ngazi ya nyuma kwa mfano *TGTS E* kurudi *TGTS D*:-

Je, Serikali haioni kwamba, haiwatendei haki Walimu hao kwa kuwanyima stahili hiyo baada ya kujiendeleza kitaaluma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwabadilisha vyeo Walimu wanaojiendeleza kitaaluma, uliokuwa umeelekezwa katika Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Namba 11 wa mwaka 2002, kuhusu Muundo wa Utumishi wa Kada zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ulirekebishwa kwa Nyongeza Namba 1 ya Waraka huo uliotolewa kwa Waraka wa Serikali wenye Kumbukumbu Namba *AC.87/260/01/B/34* wa tarehe 1 Disemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mabadiliko haya ulifafanuliwa kupitia Waraka wa Utumishi Namba 1 wa mwaka 2011. Kulingana na Miongozo hii, Walimu waliojiendeleza kitaaluma wanapaswa kuingizwa katika vyeo vipya bila kushushwa ngazi ya mshahara. Kwa mfano, Mwalimu Daraja la I aliye katika ngazi ya mshahara wa *Tanzania Government Teachers Scale D (TGTS D),* akipata Shahada atabadilishwa cheo kuwa Afisa Elimu Msaidizi Daraja la II, katika ngazi ya Mshahara ya *TGTS D.*

Vivyo hivyo Afisa Elimu Msaidizi Daraja la I, aliye katika ngazi ya mshahara ya *TGTS E,* akijiendeleza na kupata Shahada ya kwanza, atabadilishwa cheo na kuwa Afisa Elimu Daraja la I, katika ngazi ya mshahara ya *TGTS E.*

Mheshimiwa Spika, kimsingi hakuna Mwalimu, kuanzia sasa, atakayejiendeleza akashushwa cheo au akashushwa ngazi ya mshahara. Utaratibu huu wa sasa unalenga kuongeza ari ya kazi na kutoa motisha kwa Walimu waliojiendeleza kielimu.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mimi sio Mwalimu, lakini hili swali na haya maelezo nilipewa na Walimu ambao sasa hivi wanachukua Stashahada ya I na II. Ni Walimu wengi sana ambao wanamaliza Stashada ya kwanza, hawapandishwi daraja wala ngazi za mshahara; nilikuwa nataka kusema, Serikali haioni kama haiwatendei haki Walimu hawa ambao bado wanaendelea kujiendeleza, lakini wanabaki palepale?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikushauri tu Mheshimiwa Mashishanga kwamba, ni vyema nikakupa nyaraka hizi mbili halafu ukawapelekea Walimu wanaohusika, ili yeyote ambaye atakuwa na malalamiko, aweze kupeleka kwa Mwajiri aweze kurekebishiwa Mshahara wake na cheo chake. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kulikuwa na Walimu ambao walimaliza na kustaafu, halafu walipata Mkataba wa miaka 2 na Ofisi ya Rais Idara ya Utumishi. Walimu hawa wamemaliza Mkataba huo, lakini wanadai malipo yao na *gratuite* zao. Sasa inapata mwaka mzima na wamekuwa wakilalamika.

Je, Serikali iko tayari sasa kuwaangalia Walimu hao wa Wilaya ya Namtumbo, ambao wako karibu 14 walipwe stahili zao na haki yao?

**SPIKA:** Haya, hiyo ni very *specific,* lakini atajibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Walimu wale ambao wamemaliza Mikataba yao, kwa mujibu wa Sheria, wanatakiwa kulipwa *gratuite.* Kama kuna *specific case* ambayo anayo Mheshimiwa Vita Kawawa, aniletee, tutawarekebishia bila matatizo yoyote.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Walimu wengi wameitikia sana wito wa kujiendeleza, jambo ambalo limeleta pia upungufu wa Walimu katika baadhi ya shule, hasa katika Jimbo la Ukonga, wakati nilipozitembelea.

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuweka utaratibu mzuri wa Walimu hawa kwenda kusoma bila kuathiri huduma ya elimu kwa wanafunzi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwaiposa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Walimu wanapoenda kusoma wanapitishiwa barua zao na Mwajiri wao. Kwa hiyo, ni wajibu wa Mwajiri kuhakikishia kwamba, Walimu wanaenda kusoma bila kuathiri mafunzo kwa wanafunzi. Kwa hiyo, ni suala la Halmashauri husika kutengeneza *training program* ambayo, itawawezesha Walimu wengine wanaenda shuleni kujiendeleza na Walimu wengine wanabaki, bila kuathiri masomo ya wanafunzi.

Na. 27

**Umeme Unaonunuliwa Kutoka Uganda**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Serikali inanunua umeme kwa gharama ndogo toka Uganda na inauza umeme huo kwa watumiaji kwa bei kubwa inayowaumiza watumiaji hasa wa Mkoa wa Kagera.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kupunguza gharama hizo, ili watumiaji waweze kumudu kununua umeme huo kwa matumizi yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheeshimiwa Spika, mwaka 1993, *TANESCO,* iliingia Mkataba wa kuuziana umeme na Bodi ya Umeme ya Uganda, kwa senti za Marekani 8 kwa *uniti 1.* Mwezi Agosti, 2004 hadi Machi, 2009 bei hiyo ilipungua hadi senti za Marekani 6.5.

Kuanzia mwezi Aprili, 2009 wastani wa bei ya kununua umeme imekuwa ikiongezeka kila robo mwaka; hii ilitokana na ukame wa muda mrefu uliosababisha Shirika la Umeme la Uganda kutumia mitambo ya Mafuta kufua umeme, hivyo kuongeza gharama za uzalishaji wa umeme. Mamlaka ya Udhibiti wa Umeme ya Uganda, ililiagiza Shirika la Umeme Uganda, kupandisha bei ya kuuza umeme kwa wateja wake ikiwemo *TANESCO,* kulingana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009, wastani wa bei ya kununua umeme kutoka Uganda, ilikuwa ni senti za Marekani 9.6 kwa *Unit* 1, ambazo zilikuwa ni sawa na shilingi za Tanzania 128, wakati *TANESCO* ilikuwa inauza umeme huo kwa wastani wa bei ya shilingi za Tanzania 112. Mwaka 2010 wastani wa bei ya kununua umeme kutoka Uganda, ilipanda hadi senti za Marekani 13.8 ambazo ni sawa na shilingi za Tanzania 200 kwa *Unit 1.* Wakati huo *TANESCO* waliuza umeme kwa wastani wa shilingi za Tanzania 112 kwa *Unit* 1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 wastani wa bei ya kununua umeme kutoka Uganda, ilikuwa senti za Marekani 15.9 ambazo ni sawa na shilingi za Tanzania 253 kwa uniti 1, wakati huo *TANESCO* ilikuwa ikiuza umeme huo kwa wastani wa shilingi za Tanzania 141 kwa uniti moja. Aidha, kwa

mwaka 2012 wastani wa bei ya kununua umeme kutoka Uganda ni senti za Marekani 12.3 ambazo ni sawa na shilingi za Tanzania 199 na wakati huo *TANESCO* imekuwa ikiuza umeme huo kwa wastani wa senti za Marekani 12.24 ambazo ni sawa na shilingi za Tanzania 198.

Mheshimiwa Spika, kwa mtiririko niliouonesha kwa miaka minne mfululizo, *TANESCO* imekuwa ikinunua umeme kutoka Uganda kwa bei kubwa kuliko bei inayowauzia wateja wake walioko Mkoani Kagera.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri napenda kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa mkoa wa Kagera wamekuwa wahanga na gharama za maisha kutokana na kununua bidhaa kwa bei kubwa sana kwa ajili ya maisha yao. Je, Serikali haioni sasa kuweka ruzuku katika eneo hili la umeme ili kuwapunguzia wananchi wa mkoa gharama za uendeshaji wa maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI – MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa swali linalohusu umeme kama je, linaweza Serikali ikaona haja ya kuweka ruzuku, napenda tu niseme kwamba hata ukijaribu kulinganisha kwa hali ya sasa ya wenzetu majirani zetu sisi umeme wetu wa Tanzania unazalishwa bei yake tunayouza ni ndogo kuliko bei ya majirani zetu. Kwa mfano sisi Tanzania wakati tunauza umeme watu kwa wastani wa shilingi 144 kwa *unit* wenzetu wa Kenya ni 152 na Uganda ni shilingi 240 ukilinganisha hapa na kwa sababu tupo kwenye ukanda mmoja na tuko kwenye jumuiya moja ya Afrika Masharika naamini kabisa utaona kwamba umeme unaouzwa kwa wananchi wa Tanzania kwa wastani wa pesa hiyo ni kidogo sana.

Kwa hiyo, kama ziko sehemu nyingine ambazo Serikali inaweza ikatoa ruzuku lakini kweli kweli kwenye suala la umeme jambo hili bado tunahitaji kufikiri upya na tuone kwa sababu namna mpya ya uendeshaji wa mashirika yetu ya Umma katika mpango mzima wa dunia wenzetu wanaendesha Mashirika ya Umma kwa njia ya kisasa ni lazima kuwepo ile *Cost Effective* na sisi hapa tunazalisha umeme bei kubwa lakini tunauza bei ndogo kwa ajili hiyo hiyo na kwa sababu hiyo niseme kwamba Serikali inajitahidi kutoa ruzuku kwa namna hiyo.

Na. 28

**Wahitimu wa Fani ya Ugani**

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

Mpango mzima wa kilimo kwanza unahitaji maafisa ugani ili kuleta ufanisi:-

(a) Je, kuna mpango gani wa kuwapatia ajira wahitimu waliofaulu katika vyuo mbalimbbali?

(b) Je, wahitimu wangapi wanatoka wilaya ya Lindi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfani Barwany, Mbunge wa Lindi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 Serikali ilianzisha mpango wa kuwapatia mafunzo ya kilimo vijana katika ngazi ya astashahada na stashahada kwa lengo la kuwaajiri baada ya kuhitimu masomo yao ili kuhakikisha kuwa kila kijiji na kila na kila Kata kinakuwa na Afisa Ugani kufikia mwaka 2013.

Kufikia 2012 jumla ya wagani 4595 walikwishaajiriwa kwa mujibu wa mpango huo. Lengo la Serikali ni kuwa na maafisa ugani 15,082 ifika mwaka 2013 hii ni kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika

mwaka 2007 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kuendeleza sekta ya kilimo *ASDP* ambapo kulikuwa na jumla ya vijiji 12,855 na Kata 2,227 nchi nzima.

Kufikia Juni, 2012 idadi ya maafisa ugani kwa nchi nzima ilifikia 7974 hawa wakiwa wamepata mafunzo yao kutoka katika vyuo vya kilimo Naliendele, Ilonga, Uyole, Maruku, Inyala, Igabiro, Ukiriguru, Mlingano, Tengeru, Kilombero, Igurusi na Ifakara, Kilacha na *KATC.* Aidha, kuhusus wahitimu wa miaka ya 2010 na 2011, baadhi yao walichelewa kuajiriwa kutokana na kibali cha ajira toka Idara Kuu ya Utumishi kuchelewa na hivyo kukwamisha utekelezaji wa Mpango wa ajira kwa wahitimu hao. Katika mwaka 2012/2013 matarajio ni kuajiri Wahitimu 2514.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2008/2009 wahitimu kutoka Mkoa wa Lindi ni 22 wakiwemo wanaume kumi na mbili na wanawake kumi. Idadi hii inategemea jumla ya wadahiliwa waliosajiliwa kutoka Mkoa wa Lindi kushiriki mafunzo na kuhitimu. Idadi hii ni ndogo ukilinganisha na ukubwa wa mkoa ambao una wilaya tano. Wizara yangu kwa kushirikiana na viongozi wa mikoa na Halmashauri zote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, inakusudia kuwa na mkakati wa makusudi wa kuhamasisha udahili wa wanafunzi wengi zaidi kwa kila mkoa katika vyuo vya kilimo ili kuboresha mgao huo kwa nia ya kurahisisha mawasiliano na mazingira ya utekelezaji wa majukumu ya maafisa ugani hao.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii maswali ya nyongeza, kwa kuwa uzoefu unaonyesha muda mrefu kwamba wataalamu wengi hawapo tayari kufanya kazi katika maeneo ya Mikoa ya Kusini na Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba wadahiliwa katika mwaka uliopita ni wachache kulinganisha na mahitaji ya mkoa wa Lindi.

Je, Serikali ina mpango gani ya kuhakikisha hilo eneo la wataalam hao kufidiwa. Serikali ina mkakati gani sasa wa kuwaleta wataalam kutoka katika maeneo mengine na kuhakikisha kwamba wanafanya kazi katika mikoa hiyo?

Kwa muda mrefu malengo ya kufikia ufanisi katika kilimo kwanza yamekwamisha katika mambo mengi kuwepo pamoja na kuwa na wataalam. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi sasa kuhakikisha kwamba wataalam wengi wanadahiliwa katika maeneo katika nchi yetu ili kuleta ufanisi katika programu nzima ya kilimo kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ni kweli kwamba wadahiliwa kutoka Lindi ni wachache, kwa sababu katika wadahiliwa hawa kama 4500, ni wadahiliwa 22 ndiyo wanaonekana wanatokea mkoa wa Lindi. Lakini pia katika kuwadahili hawa tulichofanya ni kupokea anwani zao tu kusema kweli kwenye maombi yao hayaonyeshi makabila yao au wanatoka wapi na kadhalika ni anwani zao tu zinaonyesha wanatoka Lindi kwa hiyo tumepata wadahiliwa 22.

Lakini katika hili ni kweli kwamba hata katika utendaji tumeona kwamba watu wengi tunawapeleka kwenye Halmashauri ambazo zinaonekana zina mazingira magumu, hawa wahitimu wanakwenda halafu wanaacha kazi wanarudi.

Kwa hiyo, kusema kweli *responsibility* majukumu ya Wizara ya Kilimo yanaishia pale kwenye kuwadahili, kuwapa mafunzo na kuwapeleka kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, msisitizo tunaoweka kwa pamoja na TAMISEMI na Halmashauri ni kwamba wawachukulie wagani kama wanavyowachukulia walimu na maafisa matabibu ili wakifika pale wawapatie mazingira mepesi zaidi ya kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwapatia nyumba na vitendea kazi na kadhalika na kuwapa motisha zaidi ili hawa wengine wapate kukaa kule. *(Makofi)*

Sasa hili la pili ni kweli kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya swali la msingi tunatengeneza mkakati maalum ili hawa wagani wapate kuhamishwa kutoka kule kule Halmashauri ili tukitokea kwenye Wizara ya Kilimo maombi yale tunajua kabisa kwamba Mkoa wa Lindi umeleta wadahiliwa 200 na kwa hivyo tunajua kwamba wakienda hawa wanaotoka mkoa wa Lindi wakirudi kule watakuwa siyo wageni wa mazingira magumu yaliyoko katika mikoa hiyo.

**MHE. SULEMAIN MASOUD NCHAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa Wilaya na Jimbo la Kishapu mara kadhaa katika miaka mingi linaongoza kwa ukame. Je, Waziri wa Kilimo haoni umuhimu wa kuiwekea mpango mkakati wa kilimo cha umwagiliaji kwani hatuna hata asilimia moja ya kilimo cha umwagiliaji ili kuoa fedha nyingi Serikali inazotoa wakati wa nja kwa kupeleka mahindi mengi sana.

**SPIKA:** Nchambi, huoni kwamba hilo swali la umwagiliaji wenzako walikuwa wanazungumzia ugani? Haya tunaendelea.

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuweza kujenga chuo cha kilimo katika mkoa wa Lindi kutokana na matatizo yaliyokuwepo? Na vilevile kwa kuzingatia kwamba mkoa wa Lindi kuna mabonde mengi takribani 16 ambayo tunaweza kufanyia shughuli za kilimo?

**SPIKA:** Chuo cha kufanya nini?

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Chuo cha kufundisha ugani.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 wakati mkakati huu unaanza, wanafunzi waliokuwa wanadahiliwa walikuwa 600 tu, sasa kwa sababu ya mahitaji ya kitaifa na nimesema tumepeleka tumefufua vyuo hivi sasa vimefikia 13 na wakati mmoja wanafunzi waliokuwepo ni 3000 tunatarajia kwamba katika miaka miwili mitatu tutafikia malengo ya kuwa mahitaji ya wagani wote.

Kwa hiyo naomba niseme tu kwamba kwa vyuo tulivyokuwa navyo 13 sasa hivi na tunachokimoja pale pale Naliendele Mkoa wa Mtwara nadhani vinakidhi kwa sasa hivi isipokuwa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tufanye mkakati wa makusudi ili tuweze kukabiliana na mahitaji ya wagani wote wa mkoa wa Lindi.

**SPIKA:** Ahsante sasa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa atauliza swali hilo.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali langu naomba (a) iwe kiko nyuma kimaslahi.

**SPIKA:** Hebu sogeza *microphone* kwako sisi hatukusikii vizuri.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Iwe kiko nyuma kimaslahi baada ya marekebisho hayo naomba swali langu namba 29 sasa lijibiwe.

Na. 29

**Maslahi Duni ya Jeshi la Polisi**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Jeshi la Polisi lina dhima kubwa sana katika kulinda usalama wa raia na kuhakikisha haki na sheria zinafuatwa kila siku:-

(a) Je, ni kwa chombo hiki kiko nyuma kimaslahi?

(b) Je, ni vigezo gani vinatumika kulinganisha maslahi ya chombo hiki na chombo kama Jeshi la Ulinzi?

(c) Kwa kuwa vyombo hivi ni baba mmoja lakini haviungani kimaslahi. Je, Serikali haioni hii ndio sababu ya kurudisha nyuma utekelezaji wa majukumu yake.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba maslahi ya Jeshi la Polisi yapo chini kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiongea mara kwa mara na kuomba Serikali iwaongezee askari wetu maslahi zaidi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha maslahi ya askari kadri hali ya uchumi na Bajeti inavyoruhusu.

(b)Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni vyombo viwili tofauti na viliundwa kwa sheria mbili tofauti. Hakuna vigezo vyovyote vinavyotumika kulinganisha maslahi ya vyombo hivi kwani maslahi ya kila chombo yameainishwa kwenye sheria na kanuni husika.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya Jeshi la Polisi hatua kwa hatua sambamba na kuboresha vitendea kazi ili kuliwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

**MHE. YAHAYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria hizi ziko toka wakati wa ukoloni na tuliondoa ukoloni kwa ajili ya kujitawala pamoja na kutunga sheria zenye maslahi ya nchi. Kwanini hadi kufikia sasa ni miaka 50 sheria hizi hazijabadilishwa na kutiliwa kwamba zinadumaza utendaji wa Jeshi la Polisi?

Kwa kuwa shughuli za polisi tunajua kwamba ni nyingi sana hata wakati wa mapambano wanashiriki kikamilifu kama vile jeshi. Na hivi sasa tunajua kwamba copro analingana na inspekta wa polisi katika sehemu za mapato. Je, Serikali haioni hapa inajenga tabaka au mfarakano au kujenga kiburi kutokana na kipato hiki kati ya vyombo hivi viwili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba sheria ya polisi inachimbuko la kikoloni na hata polisi *General Orders* pia lina chimbuko hilo hilo. Hata hivyo, sheria hizi siyo kwamba hazijarekebishwa katika miaka 50 iliyopita. Marekebisho kadhaa yamefanywa katika muda tofauti ili kukidhi mazingira yanayobadilika pamoja na kuwa nchi yetu imekuwa huru. Pili, ni kwamba kidogo natofautiana kwamba kwa sababu ya tofauti za mishahara kwamba tunajenga matabaka na uhasama miongoni mwa vyombo hivi. Naomba kumhakikishia mheshimiwa Kassim kwamba askari wa Jeshi na askari wa Polisi au vyombo hivi vina mashirikiano makubwa na hakuna matabaka wala kudharauliana ushahidi ni kwamba wanafanya kazi kwa pamoja hasa yakitokea majanga au katika operesheni tofauti hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante, sheria ya nchi yetu ni kwamba mishahara na maslahi ya wafanyakazi yapitie benki, hivi sasa polisi au askari wa Jeshi la Polisi wa mkoa wa Kusini Pemba wanalipwa mkononi.

Je, ni lini askari wetu wa mkoa Kusini Pemba watalipwa kupitia Benki ili na wao waweze kunufaika na mikopo ya kibenki?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru kwa kunipa taarifa hii lakini pili nathibitisha kwamba kama hilo lipo basi ni kosa na tutalirekebisha mara moja na watalipwa kupitia benki.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza awali yote ni-declare interest kwanza mke wangu mimi ni afisa wa polisi na nataka kuzungumza maslahi.

**SPIKA:** Wewe ulikuwa polisi.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Ndiyo na mimi nilikuwa polisi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majibu ya swali la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba vyombo hivi viwili vyote ni nyeti pamoja na kwamba vimeanzishwa kwa sheria tofauti. Lakini kwa kuwa pia amegusia suala la ukosefu wa fedha kusababisha kutoongeza maslahi ndani ya Jeshi la Polisi.

Je, ni kwanini mtazamo huo wa ukosefu wa fedha katika nchi hii, maslahi ya Jeshi la Wananchi yanakuwa juu wao Jeshi la Wananchi fedha zinatoka wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nilipojibu swali la msingi nilisema kwamba maslahi ya jumla ya Jeshi la Polisi yanaongezwa pamoja na ya jeshi hali inavyoruhusu. Lakini tofauti ya mshahara inatokana na *scheme of service* ambayo nayo huwa inarekebishwa kwa wakati ambapo inaonekana ni tatizo. Tutaendelea kuibadilisha mishahara ya polisi lakini kufuatana na mabadili ya *schemes of service* bila hivyo tunajitahidi kuingiza mambo mengine kama ya *incentive schemes* na huduma nyingine za ziada ili kuhakikisha kwamba askari wetu wanaishi katika maisha yanayostahiki.

Na. 30

**Uhamiaji Haramu – Rorya**

**MHE. LAMECK OKAMBO AIRO** aliuliza:-

Kumekuwa na uhamiaji haramu kutoka Kenya kwenye mahame ya Vijiji vya Ikoma na Nyabirongo Wilayani Tarime, wahamiaji hao wanaongea Kikurya na kuwa vigumu kuwatofautisha na Wakurya wa Tarime na wamesababisha uhalibifu mkubwa ambao umesababisha mtu mmoja kupoteza maisha.

(a)Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka za kudhibitisha uhalibifu unaofanywa na Wahamiaji haramu?

(b)Je, Srikali kupitia Kanda maalum ya Tarime – Rorya inakabilianaje na hilo la wahamiaji haramu kwa ujumla wake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Nyabirongo na Ikoma Wilayani Tarime, vipo mpakani mwa Tanzania na Kenya ambapo wakazi wake wanaongea lugha moja na wakazi wa vijiji vya upande wa Kenya na kufanya utambuzi wa nani ni Mtanzani au Mkenya kuwa vigumu. Pamoja na changamoto na ugumu uliopo, jitihada za kuwatambua raia wa Tanzania na wasio raia katika maeneo tajwa zinafanyika kwa kushirikiana na viongozi wa Kata na Vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, matukio ya uhalifu ambayo yamekuwa yakitokea katika maeneo haya huwa yanahusisha zaidi wizi wa mifugo ambapo wanaobainika kuhusika na matukio hayo wamekuwa wakichukuliwa hatua za sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na wahamiaji haramu, Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imekuwa ikishirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama katika kufanya doria na misako katika maeneo mbalimbali ambapo katika kipindi cha Januari hadi Aprili, 2012 jumla ya wahamiaji haramu 84 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Kati yao Waethiopia 39, Wakongo 4, Wakenya 36, Wadenmark 4 na Mburundi 1. Aidha, Idara ya Uhamiaji

inaendelea kuimarisha mpango wake wa uhamiaji Kata ambapo kila Kata itakuwa na Afisa Uhamiaji anayeshirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata kwa lengo la kuwa karibu na wananchi na kutoa elimu ya uraia na uhamiaji ili kuwatambua wahamiaji haramu.

**MHE. CHACHA N. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba kuna wahamiaji katika Wilaya ya Tarime na Rorya ambao wamesababisha kuvunjika kwa amani na wananchi wa Tarime na Rorya kuonekana kwamba ni wakorofi. Kwa kuwa, hakuna hatua zozote madhubuti ambazo zimechukuliwa. Je, Serikali inakiri kwamba itashirikiana na wananchi wa Tarime na Rorya kuondoa wahamiaji haramu kutoka Wilaya ya Tarime?

Pili, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kazi ya Kanda Maalum iliyopo Tarime na Rorya ambayo kila siku inahusika na kulinda amani lakini wakati huohuo amani inavurugika katika Wilaya ya Tarime na hasa katika mji mdogo wa Sirali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo;

Swali la kwanza kuhusu ushirikiano wa Wizara na Idara ya Uhamiaji iko tayari kutoa ushirikiano na wananchi wa Rorya ili kuhakikisha kwamba wahamiaji haramu wanatambuliwa na wanachukuliwa hatua za kisheria.

Kuhusu swali la pili, Wizara inachukua juhudi za makusudi na inaongeza jitihada za hasa elimu ili kuhakikisha kwamba wahamiaji haramu hawapati nafasi za kutuharibia usalama uliopo. *(Makofi)*

Pamoja na mbinu ambazo tunazichukua za kushusha madaraka zaidi vijijini, suala la elimu kwa wananchi ni jambo ambalo tunaliona ni muhimu kwa sababu wakati mwingine ni wananchi ambao wanawaficha wahamiaji haramu. Kwa hiyo, tunataka tuwape elimu ili tushirikiane zaidi ili watoe taarifa wapi wapo ili tuwafuate.

**SPIKA:** Kanda, anasema utaratibu wa Kanda ya Ulinzi kule inafanya kazi gani? Umesikia hiyo? Kanda Maalum Tarime inafanya kazi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, taratibu za kuanzisha kanda maalum zinatokea pale ambapo pana mahitaji maalum na kwa sababu kule kuna ongezeko la matukio ya uhalifu ndiyo maana tukahisi kwamba tuanzishe Kanda Maalum ili tuweke *concentration* ya kusimamia mambo yale. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba uongeze majibu ya nyongeza hapo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba niongeze kidogo katika suala la Kanda Maalum katika mkoa wa ......

**SPIKA:** Ni kwamba Mic haisikiki vizuri au? Ongeza sauti!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, .....

**SPIKA:** Naomba usogee mbele tu! Sogea mbele wewe ni Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI UTALII:** Mheshimiwa Spika, suala la Kanda Maalum kama alivyosema Mbunge, makusudi na madhumuni ni kwa sababu kumekuwa na matatizo ya gomvi za koo katika maeneo hayo. Lakini pia kumekuwa na suala la wizi wa mifugo ambalo limekuwa ni kubwa sana

kutoka nchi jirani na Kanda Maalum kwa kweli imekuwa inafanya kazi ambayo inastahiki na Wabunge wengi hapa hata Wabunge ambao wanatoka katika Mkoa wa Mara wamekuwa wakisifia kazi ambayo imekuwa inafanyika. *(Makofi)*

Lakini niseme tu kwamba Kanda Maalum inataka ushirikiano mkubwa kutoka kwa wenyeji kwa sababu watu ambao wanavuka kuja katika sehemu ya Tanzania kama alivyojibu Naibu Waziri ni walewale, kabila ni zilezile na lugha ni zilezile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunahitaji ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa wananchi ili kuhakikisha kwamba Askari ambao tumewaweka pale wanashirikiana na wananchi ili kuhakikisha kwamba amani inakuwepo na gomvi hizi ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu zinakomeshwa.

**SPIKA:** Ahsante sana, tumechukua muda mrefu kwa swali hili kwa hiyo tunaendelea na Wizara ya Fedha Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, swali linalofuata!

Na. 31

**Kuhamishia Fedha za Mkopo wa Mabilioni ya Kikwete Kwenye Benki ya Wanawake**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuhamishia fedha za mkopo wa mabilioni ya Kikwete na kutumika katika benki ya wanawake ili wananchi wakiwemo wazee, wanawake na vijana waweze kupata mikopo ya uhakika katika kuimarisha miradi yao mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake inaweza kushiriki katika mpango wa kukopesha na kusimamia fedha za mabilioni ya Mheshimiwa Rais endapo inahitaji kufanya hivyo sambamba na taasisi zingine za fedha ambazo zinafanya kazi hiyo.

Taasisi zenyewe ni kama *CRDB, NMB,* Benki ya Posta, Benki ya Biashara ya Azania, Benki ya Biashara ya Akiba, Benki ya Wananchi za Mwanga na Kilimanjaro, Benki ya Uchumi, Benki ya Wakulima ya Kagera, *Pride Tanzania, Presidential Trust Fund DUNDULIZA* na *SCCULT.*

Kwa hiyo, Benki ya Wanawake inaweza kufanya hivyo baada ya kufanyiwa tathmini na *BOT* ili kuweza kukidhi vigezo vilivyowekwa ikiwa ni pamojan a uwezo wa kuhudumia wananchi walio wengi vijijini na vilevile kuwa na mizania nzuri za hesabu pamoja na uzoefu katika kuhudumia wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa walengwa wa mfuko wa mabilioni ya Rais ni vijana, wazee wanawake wa vijijini na mijini na ambao wanafanya shughuli ndogo ndogo za kiuchumi.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, kwanza naomba kuipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) katika kutekeleza ilani yake vilivyo kwa kuwapatia mikopo wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alivyotoa mfuko huu wa mabilioni yake kuwakopesha wananchi wa Tanzania alikuwa na madhumuni ya

kuwasaidia wananchi wafanyabiashara ili kuwaendeleza vipato vyao. Lakini inaonekana mfuko huu katika maeneo mengi haukuwa umetekelezwa vizuri yaani haukusimamiwa vizuri.

Je, Serikali imefanya tathmini gani kutujulisha sisi Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba mfuko huu umetumika vizuri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kumjibu Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar Mbunge wa Viti Maalum, swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ni muda sasa toka mwaka 2006/2007 ambapo Serikali ilitenga jumla ya bilioni 21 kwa ajili ya kuwapa wananchi. Kwa hiyo, tathmini ni muhimu kwa sasa na tayari *data* zimeshaanza kukusanywa kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Kwa wananchi ama wajasiriamali wapatao 74,593 ambao wamepatiwa fedha hizi jumla ya shilingi bilioni 49.64. Ni wakati muafaka wa kufanya tathmini na *data* tayari tumeshaanza kukusanya na ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba matokeo ya tathmini hiyo yatabainisha mafanikio na changamoto ili mafanikio tuweze kuyapeleka katika sehemu nyingine na zile changamoto tuweze kuzi-*address* ili kuzipatia ufumbuzi.

Kwa sasa Benki ya Wanawake, swali lake la msingil lilikuwa ni Benki ya Wanawake, nasema ina tawi moja tu Jiji Dar es Salaam lakini vilevile inaanza mchakato wa kukamilisha kufungua tawi lake Zanzibar.

Kwa hiyo, kabla hatujaenda kuipa hii Benki ya Wanawake tunafanya hiyo tathmini na matokeo ya tadhmini yatatuambia changamoto na mafanikio wapi tuelekee na wapi twende na kuna *constrain* gani hasa kwa wananchi kwa ajili ya matumizi ya fedha hizi za mikopo. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour!

Na. 32

**Misamaha ya Kodi Nchini Imekuwa Kero**

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR** aliuliza:-

Misahama ya kodi nchini imekuwa kero kwa muda mrefu kwa Taifa kukosa fedha na mapato kwa ajil ya maendeleo.

Je, Serikali inasemaji juu ya kupunguzwa kwa misamaha hiyo hadi kufikia chini ya 1% ya pato la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kupitia baadhi ya Sheria za misamaha ya kodi ili kuangalia kama bado zina manufaa kwa Umma. Lengo la Serikali ni kupunguza misamaha ya kodi ili isizidi 1% ya pato la taifa. Ili kutimiza azma hii, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), kupitia mfuko wa dhamana ya ushauri wa sera na usimamizi wa kodi ulioanzishwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), inafanya uchambuzi wa kina wa kuangalia sheria na kanuni za misamaha ya kodi na kuleta mapendekezo ya kuiondoa misamaha ya kodi na kuleta mapendekezo ya kuiondoa misamaha yote isiyo na maslahi na tija kwa taifa pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 20125/2013 kama tulivyosikia, Serikali imechukua hatua za kurekebisha sheria mbalimbali za kodi kwa nia ya kupunguza misahama ya kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi. Hatua hizo zimejitokeza kwenye hotuba ya Bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha mapendekzo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2012/20123.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, Serikali ilianza kutangaza kwa muda mrefu hatua hizi kuzichukua.

Je, Serikali iko tayari kutuonyesha program iliyoanza utekelezaji wa hatua hizi za misamaha ya kodi?

Pili, kwa kuwa, Bajeti ya safari hii imepunguza 10% tu ya misahama ya kodi na sisi Bungeni tunalalamikia misahama yote ya kodi. Je, hiki si kiini macho?

**SPIKA:** Lingine si litajibiwa wakati wa mchango? Hebu jibu swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, maswali yake mawili kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyosikia kwenye mapendekezo ya Bajeti ya matumizi na mapato ya Serikali mwaka 2012, tumetangaza hatua za kuchukua kwa ajili ya kupunguza hiyo misahama ya kodi, ni kweli sasa ni 10% tu lakini tunataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kazi hiyo itafanyika na itafanyika kikweli na matokeo tutakuja kuyaonyesha hapa katika Bunge lako Tukufu. Tunaomba tu tupewe muda kwa sababu kama tumetangaza katika Bunge la mwaka jana, basi naomba tupewe muda kwa sababu hakuna kitu kinachofanywa mara moja lakini matokeo tutakuja kuyaonyesha hapa katika Bunge lako Tukufu. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari atauliza swali hilo.

Na. 33

**Agizo la Wapagazi (Porters) Kulipwa Dola 10 Kila Siku**

**MHE. JOSHUA SAMWEL NASSARI** aliuliza:-

Utekelezaji wa maagizo ya Serikali kupitia tangazao la Serikali Na. 228 la tarehe 29 Juni, 2009 Wapagazi (*Porters*) wa kubeba mizigo ya Watalii kulipwa mshahara wa dola 10 za kimarekani kwa siku kutoka sh. 6000/= bado unasuasua.

(a) Je, Serikali kupitia tangazo la Serikali imezichukulia hatua gani kampuni za utalii ambapo zinakiuka agizo la Serikali?

(b) Je, ni lini kampuni hizo ambazo hazikulipa mshahara stahiki zitalipa fidia ya mishahara hiyo ambayo haikulipwa tangu tarehe 1 Julai, 2010?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wabeba mizigo hao wanaopanda milima ni vijana wa eneo husika na siyo kuchukuliwa vijana wa sehemu nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasil na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangazo la Serikali namba 228 la mwaka 2009 lilitoa kiwango elekezi cha malipo kwa ajili ya wapagazi wanaofanya kazi ya kubeba mizigo ya wapanda mlima kuwa wasilipwe chini ya dola za Kimarekani 10 kwa siku. Aidha, katika tangazo hilo, ilisisitizwa kwamba, wapagazi watakaopewa ajira ni wale waliojisajili katika vyama vya wapagazi vilivyosajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kazi Namba 6 ya mwaka 2004, imeweka bayana aina mbalimbali za mikataba ya kazi ambapo ipo mikataba ya kazi ya muda maalum, mikataba ya kazi maalum na ya kazi zenye utaalamu. Kwa mantiki hiyo, kila mfanyakazi anapaswa mara anapoingia kazini ahakikishe kuwa anasaini mkataba kati yake na na mwajiri wake kwa kuzingatia mikataba tajwa. Kisheria, waajiri wote nchini wanao uhuru wa kijipangia viwango vya mishahara ili mradi visiwe chini ya kima cha chini kinachowekwa na Serikali kulingana na Sheria ya kazi pamoja na *Wage Order.* Hata hivyo, Serikali imeamua kuwa katika siku za usoni mishahara ya kundi hili itapangwa kwa utaratibu wa kisekta kama ilivyoainishwa katika sheria ya taasisi za kazi namba 7 ya mwaka 2004. Vilevile, Wizara kupitia *TANAPA* huwashauri Wapagazi kujiunga na vyama vilivyosajiliwa kama *Kilimanjaro Porters Association na Kilimanjaro Porters Society* au inajulikana kama *Tanzania Porters Assistant Project* na kupata vitambulisho. Kupitia vyama hivyo wapagazi hupata nguvu ya pamoja ya kudai maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, sheria na Katiba ya Nchi inamruhusu kila Mtanzania kuishi na kufanya kazi mahali popote ili mradi havunji sheria ya nchi. Hivyo, kinachofanyika hapa ni kuhakikisha kwamba wapagazi wanaobeba mizigo ya wapandaa milima wanajisajili na wanapata vitambulisho vinavyotolewa na vyama vinavyotambulika kisheria.

**MHE. JOSHUA SAMWEL NASSARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme nimesikitika kwa majibu yasiyoridhisha kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu majibu niliyopatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri siyo majibu ambayo ninayo mkononi. Kwa ruhusa yako labda nikuonyeshe tu kama utaniruhusu kwamba maijbu yaliyotolewa ni tofauti sana na majibu ambayo ninayo mkononi ambayo yametoka Wizarani.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako katika hilo.

**SPIKA:** Haya endelea, swali la pili?

**MHE. JOSHUA SAMWEL NASSARI:** Mheshimiwa Spika, siwezi kuuliza swali la pili la nyongeza wakati swali la msingi halijajibiwa na ni tofauti na nililopewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri mwenyewe una majibu mawili au vipi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba tu niliambie Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu wa kuandaa majibu ya Serikali, mchakato wa majibu unaendelea mpaka wakati ambapo Waziri anayehusika atayasoma hayo majibu hapa. Kwa hiyo, majibu niliyomsomea ayachukue kama majibu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ni sahihi kwamba hayo uliyopokea Wizarani, sijui kutoka wapi, mimi Spika nita-*verify* kwamba majibu niliyo nayo ndiyo ambayo anayo Waziri. Kwa hiyo, nitafanya hivyo. Tutakutolea maelezo kesho. (*Makofi*)

Tunaendelea na swali linalofuata. Nyie hamuwezi kuuliza swali la nyongeza, mwenyewe hajalikubali. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Na. 34

**Kudhibiti Ujenzi Holela**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Ujenzi holela katika maeneo ya wazi na yale yaliyotengwa kwa matumizi maalum kama vile michezo na kadhalika. Limekuwa tatizo sugu katika miji yetu na Maafisa Mipangomiji wanapaswa kusimamia kikamilifu uendelezaji wa Miji na kutoruhusu wananchi kujenga katika maeneo yaliyotengwa kwa kazi maalum:-

(a)Je, Serikali haioni kuwa kutowachukulia hatua Maafisa Mipangomiji wasiotekeleza wajibu wao ni kuendekeza watumishi wasio waadilifu?

(b)Je, Serikali haioni kwamba kuwavunjia nyumba wananchi waliojenga katika maeneo hayo bila kuwaadhibu Maafisa waliohusika ni kuwaonea wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utendaji kazi wa Watumishi wa Serikali husimamiwa na sera, sheria na kanuni za utumishi wa umma. Mtumishi yeyote anapobainika kuwa amekiuka maadili ya taaluma na kazi yake, huchukuliwa hatua za kinidhamu kulingana na uzito wa kosa alilotenda.

Hivyo, Maafisa Mipangomiji ambao ni sehemu ya watumishi wa Serikali wamekuwa wakichukuliwa hatua za kinidhamu inapothibitika kuwa wamekiuka maadili ya kazi na taaluma zao na hivyo kukiuka sera, sheria, kanuni na miongozo inayosimamia upangaji na uendelezaji wa miji.

Pamoja na maafisa Mipangomiji, vilevile Serikali imekuwa ikiwachukulia hatua viongozi na watendaji wa ngazi zote inapobainika kuwa wameshirikiana na Maafisa hao pamoja na wavamizi wa maeneo ya wazi na ardhi yoyote ambayo hawajapangiwa kwa mujibu wa sheria ikiwemo viwanja vya michezo. Katika kipindi cha mwaka 2009 – 2012 Wataalam wa Sekta ya ardhi wapatao saba (7) waliachishwa kazi na wanane (8) wanaendelea kuchunguzwa. Tuhuma dhidi yao zitakapothibitika watachukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria itakapobidi.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha usimamizi wa Maafisa Mipangomiji, Serikali litunga sheria ya kusimamia taaluma za Maafisa Mipangomiji (Sheria Na. 7) ya mwaka 2007 ambayo imeweka pamoja na mambo mengine, adhabu kwa kila atakayekiuka maadili ya kazi yake.

(b)Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 mtu yeyote anayetaka kujenga mjini ni lazima awe na hatimiliki na kibali cha ujenzi kilichotolewa na mamlaka ya mji unaohusika. Mtu anayejenga bila kuwa na nyaraka hizo au kutumia nyaraka bandia zilizotolewa na maafisa wasio waadilifu au nyaraka zilizotengenezwa mitaani atakuwa amekiuka sheria.

Zaidi ya hayo anayejenga kwenye eneo la wazi atakuwa amekiuka sera na sheria za ardhi na ya mipangomiji. Kumvunjia nyumba mtu aliyekiuka sera na sheria si uonevu bali ni utekelezaji wa maelekezo na sheria za nchi.

Kabla ya majengo yaliyojengwa kwenye maeneo ya wazi, maeneo ya barabara na maeneo hatarishi kinyume cha sheria kuvunjwa, wamiliki hupewa taarifa inayowataka kuvunja wao wenyewe. Kama wakishindwa au wakikaidi maagizo hayo, Serikali huchukua hatua za kuvunja na kuwadai gharama.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi kuwa waepuke kujichukulia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali na kujenga kinyume cha sheria. Hii itawaepusha na hasara inayowapata inapobainika kuwa wamejenga kinyume cha sheria.

Vilevile, wananchi wanahimizwa kutoa taarifa juu ya uvamizi wa maeneo ya wazi au wanapohisi kuwa ujenzi unaofanyika haujazingatia sheria. Wizara yangu imetoa namba za simu (*hotlines*) kwa ajili ya kutoa taarifa ambazo ni 0712 274959, 0756 261286 na 0689 665312.

Mheshimiwa Spika, ziko taarifa kuwa baadhi ya Wenyeviti wa Mitaa na Watendaji wamekuwa wakishiriki kuruhusu uvamizi wa ardhi kutokea katika maeneo yao. Kupitia Bunge lako Tukufu natoa wito kwa viongozi na watendaji wote wa mitaa kwamba wahakikishe kuwa kuanzia sasa hakuna ujenzi utakaofanyika katika maeneo yao bila uthibitisho kuwa ujenzi huo umeruhusiwa kwa kudai na kuthibitisha uhalali wa vibali vinavyotumika.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba Wananchi wanaovamia maeneo ya wazi hawavamii kwa kupenda bali ni kutokana na urasimu uliopo katika ugawaji wa viwanja?

(ii) Kwa kuwa wananchi wana ari kubwa ya kujenga kwenye viwanja katika maeneo ya mjini, tatizo ni ucheleweshaji wa ugawaji wa viwanja na wakati mwingine watumishi wanaohusika katika ugawaji wa viwanja huhodhi viwanja vingi kwa nia ya kuuza kwa bei ghali kwa mlango wa nyuma.

Je, Serikali inatoa tamko gani katika kuweka wazi suala la ugawaji wa viwanja katika maeneo ya mijini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba kuna upungufu wa viwanja mijini. Hii inatokana na ukweli kwamba Serikali haina uwezo wa kwanza kutwaa maeneo, kwa sababu unapotaka kutwaa eneo la mtu lazima ulipe fidia kwa mujibu wa sheria. Kutwaa maeneo na kisha kuyapima na kuwamilikisha watu. Kwa hivyo, kuna upungufu huo.

Lakini hiyo haisababishi kwamba uvamie maeneo kama wewe ni raia mwema. Raia mwema huheshimu sheria. Huwezi ukaenda na kuvamia kwa sababu eti unataka kujenga tu. Lakini tunakiri pia kwamba, uhaba wa viwanja mjini, yaani vile vilivyopimwa imekuwa sababu ya ujenzi holela. Ndiyo sababu Serikali ilianzisha mpango wa kurasimisha maeneo hayo yaliyojengwa kiholela ili kuwatambua wamiliki wale kuwa ni wamiliki halali na kuwapa Hati.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwamba kuna ucheleweshaji wa ugawaji wa viwanja na pia kuwa watumishi wa sekta ya ardhi wamekuwa wakihodhi viwanja ili baadae wauze kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, zipo taratibu mbili za kugawa viwanja; kuna kugawa kiutawala (*administrative allocation of land*) na kugawa kwa njia ya soko (*market allocation*). Tunapofanya ile *administrative allocation* uwezekano wa kujilimbikizia ardhi upo. Lakini tunapofanya *market allocation* haupo uwezekano mkubwa kwa sababu viwanja hivi tunatangaza na tunaalika wale wenye nia ya kuviendeleza waweze kuomba na kuuziwa viwanja hivyo. Huu ni utaratibu ambao umekuwa ukitumika.

Kwa mfano pale Gezaulole kuna viwanja ambavyo vimetangazwa na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na wananchi wanaohitaji wamejitokeza kuomba na watapatiwa viwanja hivyo kwa kuuziwa, yaani kurejesha gharama zote ambazo Halmashauri imezitumia katika kupata maeneo hayo.

Kwa kufanya hivyo, hiyo inapunguza huo mwanya wa watu kujilimbikizia ardhi. Lakini pia sheria imeweka ukomo kwamba, kama umechukua ardhi eneo hili huwezi ukalimbikiza zaidi ya miaka mitatu. Ukiishagaiwa ardhi, baada ya miezi thelathini na sita (36) lazima uwe umejenga, kama hujajenga Serikali inatwaa tena ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwa kuweka masharti haya imesaidia kupunguza uwezekano wa Watumishi kujilimbikizia ardhi. Lakini nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwamba, kama mna taarifa ya watumishi waliojilimbikizia ardhi naomba mtupatie ili tuweze kuchukua hatua dhihi yao ya kuwanyang'anya ardhi ile.

**SPIKA:** Maswali yamekwisha, lakini na muda wenyewe umeisha.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo!

**SPIKA:** Nimesimama hakuna cha Mwongozo. Mheshimiwa Nassari wakati anajibiwa swali lake Na. 32 alieleza kwamba majibu aliyonayo ni tofauti na yale aliyokuwa anasoma Naibu Waziri.

Katika kufanya utafiti wetu tumekuta majibu anayosema Mheshimiwa Nassari, ni kweli yalitolewa kwanza lakini yakawa *withdrawn*. Ndiyo maana majibu niliyo nayo hapa yanafanana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini Mheshimiwa Nassari alipopewa nakala ya pili hakutaka kuipokea.

Sasa Waheshimiwa Wabunge ninachoomba, Serikali kama inaamua kubadilisha majibu yake huko tunakubali kwa sababu ni majibu yake. Kwa hiyo, ndivyo ilivyotokea.

Sasa nilikuwa nadhani kama mimi ningekuwa na majibu tofauti na yale aliyokuwa anasoma Mheshimiwa Waziri, hapo ningeuliza kwa sababu tunaogawa majibu ni sisi. Ofisi ya Bunge inagawa. Wali-*withdraw* majibu ya swali lile analosema yeye, wakaleta majibu mengine ambayo na mimi ninayo. Kwa hivyo, ndivyo ilivyokuwa.

**SPIKA:** Kuhusu mwongozo, Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kuomba Mwongozo kuhusiana na hili swali la Mheshimiwa Nassari.

Mheshimiwa Spika, majibu ya maswali yetu ambayo Wabunge huwa tunapewa, tunapewa siku nyingi, *at least* siku moja kabla swali halijajibiwa. Swali la Mheshimiwa Nassari, jibu lake alilipewa siku ya Ijumaa kwa mujibu wa taarifa yake. Sasa kama lilikuwa *withdrawn* ilitakiwa kuwe na *notification*.

Mheshimiwa Spika, suala alilosema Mheshimiwa Waziri kwamba kujibu swali ni mpaka dakika ya mwisho anaposimama kwenye *podium* kujibu inaenda kinyume kabisa na Kanuni ya 46 (1) ya Kanuni za Bunge inayotaka Mbunge apewe nakala ya jibu litakalosomwa Bungeni. Haijafanyika hiyo na hii siyo sawasawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, kama ungefuatilia maelezo yangu yale wala usingeuliza swali hilo. Ni kwamba, majibu yale ya Mheshimiwa Nassari yalikuwa *withdrawn.* Hilo analosema kwamba, ikaletwa nakala mpya ambayo hata mimi ninayo na alipewa Mheshimiwa Nassari akakataa lile jibu. Sasa si imekwisha?

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, tangazo kuhusu wageni wetu. Wageni tulionao hapa Bungeni ni Wageni kutoka *Bongo Star Search* (BSS) ambacho ni kikundi kinachokuza vipaji vya Wasanii hapa nchini ambao ni majaji watatu; Madame Ritha Pausen, yuko wapi.

Okay! Yuko mwingine Salama Jabiri (Salama J.) na yuko mwingine anaitwa Joachim Kimaro (Master J.). Wako hapa na ninadhani wengi wanaofuatilia mambo hayo wanawafahamu sana. Wako pamoja na timu ya wapiga picha za video ambao wako wanne. Wako wapi hao wapiga picha za video? Okay karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu kutoka *Lindi Community Development Foundation* wakiongozwa na Mwenyekiti wao Bi. Asha Muhidin. Bi. Asha na kikundi chake ahsante sana, tunashukuru sana.

Pia tuna Wanafunzi 41 kutoka Chuo cha Ufundi cha Usula, Singida Mashariki. Naomba walipo wasimame na Walimu wao. Ahsante sana. Tunawatakia masomo mema na mkiwa hapa mtajifunza yale mtakayokuwa mnaelekezwa na watu wetu hapa. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge tuna matangazo pia ya kazi. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa John Paul Lwanji, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 18 Juni, 2012 Saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 227 ghorofa ya pili.

Tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kuwa leo Saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge kutakuwa na kikao kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Kepteni na Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Amos Makalla anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge hasa wana michezo kuwa wanaombwa kuhudhuria mazoezi katika Uwanja wa *Jamhuri Stadium,* Dodoma kuanzia Saa 12. 00 asubuhi.

**UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA BUNGE**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Uongozi ilikutana siku ya Alhamisi, tarehe 14 Juni, 2012 na kufanya uteuzi wa jina la atakayejaza nafasi hiyo. Kikao hicho kilimteua Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala, Dar es Salaam, kuwa awe ndiye mgombea pekee katika nafasi hiyo. (*Makofi*)

Hivyo naleta jina lake kwenu ili mumthibitishe kuwa Mwenyekiti wa Bunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 11 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007.

**MBUNGE FULANI:** Kapita huyooooo.

**SPIKA:** Kwa hiyo, naleta jina lake. Kwa sababu yuko peke nitawahoji. Wanaoafiki na wasioafiki kwamba Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan awe Mwenyekiti wa Bunge.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MJUMBE FULANI:** Mgombea yuko wapi?

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala, Dar es Salaam, atakuwa ndiye Mwenyekiti wa tatu katika Wenyeviti wanaomsaidia Spika. Tunakupa dakika moja uje uzungumze hapa mbele. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii, kwanza, kuishukuru Kamati ya Uongozi, iliyoongozwa na Mheshimiwa Spika, kwa kuniteua mimi kuja hapa kuomba ridhaa ya Bunge hili kuwa Mwenyekiti wa Bunge kwa kipindi kilichobakia. Nafasi hii niliyopewa ni ya heshima kubwa sana, si kama hakuna watu wengine ambao wana uwezo, wote humu ndani tuna uwezo sawa sawa wa kufanya kazi hiyo, lakini mliamua mimi ndiyo niwe mtumishi wenu ndani ya Bunge

hili. Nashukuru sana kwa heshima hiyo. Naahidi kufanya kazi zangu kwa uadilifu na kwa Kanuni zote zilizoainishwa kwenye Bunge letu hasa nikizingatia Kanuni ya 8(1) na (2), iliyopo ukurasa wa sita. Nawashukuru sana ahsanteni sana. (*Makofi)*

**MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2012
*(The Finance Bill, 2012).*

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa maana hiyo, tukishamwita Waziri wa Nchi, kutoa hoja ya kufanya mabadiliko katika utaratibu wetu wa kujadili Bungeni, nitaomba Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu ukiacha wale watakaotakiwa kusoma hapa, tukutane *Speaker's Lounge* tushauriane jambo dogo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya kifungu cha 150(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

**KWA KUWA** Mkutano wa Nane wa Bunge unaoendelea pamoja na shughuli zingine zilizopangwa, kutakuwa na shughuli za kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 57 pamoja na kujadili na kupitisha Makadirio ya Wizara mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 99;

**NA KWA KUWA** idadi ya Waheshimiwa Wabunge wanaoweza kuchangia na kujadili Bajeti ya Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Wizara mbalimbali ni 298;

**NA KWA KUWA** kwa mujibu wa Kanuni ya 57(1) na 98 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, muda wa kujadili Bajeti ya Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Wizara mbalimbali ni dakika zisizozidi 15;

**NA KWA KUWA** kwa kutenga dakika 15 za kuchangia kutatoa nafasi kwa Wabunge 140 tu kuchangia katika Bajeti ya Serikali na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo ni sawa na asilimia 47 ya Wabunge wote; lakini kwa kutenga dakika kumi za kuchangia kutatoa nafasi kwa Wabunge 210 kuchangia Bajeti hizi ambapo ni sawa na asilimia 70 ya Wabunge wote;

**NA KWA KUWA** kwa kutumia dakika kumi za kuchangia kutatoa fursa ya wastani wa kila Mbunge kuchangia mara tatu katika Mkutano mzima;

**NA KWA KUWA** ili kuwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake kikamilifu na kwa wakati huo huo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge wengi kupata fursa ya kujadili Bajeti ya Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Wizara mbalimbali, inabidi kutengua Kanuni ya 57(1) na 99(8) zinazotoa maelekezo ya muda usiozidi dakika 15 kwa mchangiaji;

**HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Nane, Kanuni ya 97(1), 99(8) na 104 (4) na (5) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

(i) Kanuni ya 97(1) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Mbunge anayetaka kujadili Hotuba ya Bajeti ya Serikali ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 15 itenguliwe na badala yake itumike muda usiozidi dakika kumi;

(ii) Kanuni ya 99(8) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Mbunge anayejadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara mbalimbali ataruhusiwa kusema kwa

muda usiozidi dakika 15 itenguliwe na badala yake itumike muda usiozidi dakika kumi;

(iii) Kanuni ya 101(4) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Mbunge anayetaka ufafanuzi anaweza kuzungumza si zaidi ya mara mbili juu ya suala hilo itenguliwe na badala yake azungumze si zaidi ya mara moja; na

(iv) Kanuni ya 101(5) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba muda wa kusema katika Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kutoa ufafanuzi hautazidi dakika tano itenguliwe na badala yake muda usiozidi dakika tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima na kwa niaba yako, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, sababu kubwa ni kama alivyosema, tukisema tufuate Kanuni katika majadiliano haya asilimia 47 tu ya Wabunge watapata muda wa kuzungumza.

Tumefanya hesabu zetu, muda tunaofanya kazi kama Wabunge katika Bunge hili, Vikao vya Kamati na kadhalika ni siku 341. Kwa hiyo, imekuwa vigumu sana ukisema utaongeza isipokuwa ukipanga vizuri mambo yako dakika kumi ni nyingi sana.

Naomba sasa tukubaliane ili tutoe nafasi nzuri kwa kila Mbunge aliyechaguliwa kwa namna yoyote ile aweze kusikika. Kwa hiyo, naomba tupunguze kutoka dakika 15 ziwe 10 tuweze kufanya kazi vizuri zaidi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kupunguza muda wa kuchangia Bungeni iliafikiwa na Bunge)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, naomba Wenyeviti tushauriane jambo dogo hapo na wakati huo nitamwomba Mwenyekiti Jenista Mhagama aje anisaidie kushika Kiti hiki.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja inayofuata kama ilivyoelekezwa na Katibu wa Bunge. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya Mwenyekiti mwenzangu, Mheshimiwa Stephen Massele Mabumba, tunaomba tumpongeze sana Mheshimiwa Zungu, kwa kupitishwa na Bunge hili leo kuwa Mwenyekiti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi kama Wenyeviti wenzake, tutampa ushirikiano wa kutosha na tutafanya nae kazi bega kwa bega. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea, nimwite Mwenyekiti aliyechambua Sekta hiyo aweze kutupa maoni ya Kamati na wakati huo huo Msemaji wa Kambi ya Upinzani akiwa anajiandaa. Namwona Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Andrew Chenge, anakuja kusoma Taarifa ya Kamati kwa niaba ya Kamati yake.

**MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako asubuhi hii. Pili, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kunipatia heshima ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Nitumie nafasi hii pia kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuwapongeza baadhi ya Wajumbe waliokuwa Kamati hiyo ambao wamepata nyadhifa mbalimbali nikianza na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ameenda kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, ambaye sasa ni Waziri wa Fedha na Dkt. Binilith Saatano Mahenge, ambaye amekuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Maji.

Pia kuna Wajumbe ambao wanaendelea kubaki kwenye Kamati ambao wamepewa nyadhifa zingine, Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Rosemary Kirigini kuwa Wakuu wa Wilaya. Tunawatakia kila lililo jema katika nyadhifa zao mpya. *(Makofi)*

Ninampongeza pia Mwenyekiti wetu mpya, Mheshimiwa Zungu, Mbunge wa Ilala, naahidi ushirikiano wa karibu kwake kama ilivyo kwako Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, niseme naomba niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa, Mb, Naibu Mawaziri wa Fedha Mheshimiwa Janet Z. Mbene, Mb na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mb, kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais, kuiongoza Wizara hii muhimu.

Kamati vilevile inaipongeza Wizara kwa kuwa sikivu na kukubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati katika kuboresha Bajeti hii. Taarifa hii ni mwendelezo wa maoni na ushauri wa ziada katika maeneo kadhaa ambayo Kamati inaamini kuwa Serikali itayazingatia ili kuibua maeneo mengine ya kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi na kutekeleza vipaumbele tulivyojiwekea kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kwamba, uchumi imara wa nchi unahitaji nidhamu ya juu katika matumizi ya Serikali, ongezeko la mapato ya ndani, utumiaji bora wa rasilimali zilizopo na uendelezaji rasilimali watu kwa maendeleo endelevu. Hivyo ni muhimu Bajeti ya Serikali ikajielekeza katika kupima mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti iliyopita ambayo kimsingi ndiyo yanayopaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutafakari Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imezipokea vyema Taarifa zote za Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali, zilizotolewa na Serikali. Taarifa hizi kwa ujumla wake zimebainisha mfumo wa uchumi jumla na jinsi gani vipaumbele na mikakati vinatafsiriwa kupitia utengaji wa rasilimali baina ya sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishatoa maelezo ya ujumla kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2012/13 na Bajeti ya Fedha kwa Mwaka 2012/13. Aidha, Sera ya Mapato na Matumizi na Mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 nao umeelezwa katika Hotuba ya Waziri wa Fedha. Mwenendo wa Hali ya Uchumi unaonesha kuwa katika mwaka 2011, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 6.4 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010 ikiwa ni pungufu ya asilimia 0.6 ya Pato la Taifa. Kiwango cha juu cha ukuaji kilikuwa katika shughuli za Sekta ya Mawasiliano asilimia 19; huduma za fedha asilimia 10.7; ujenzi asilimia 9.0; uzalishaji viwandani asilimia 7.8 na elimu asilimia 7.4. Kwa upande wa Sekta ya Kilimo, kasi ya ukuaji imepungua hadi asilimia 3.6 kutoka asilimia 4.2 kwa mwaka 2010. Aidha, Sekta ya Mifugo ilikua kwa asilimia 3.9 kutoka asilimia 3.4 mwaka 2010.

Ukuaji wa wastani wa kipato kwa wananchi umeongezeka. Takwimu zinaonesha kuwa ukuaji huo ni sawa na Sh.869,436.3 (USD 550.45) mwaka 2011 ikilinganishwa na Sh. 770,464.3 (USD 537.94) kwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mfumko wa bei umeendelea kuwa changamoto kubwa. Takwimu zinaonesha kuwa mfumko wa bei uliongezeka kutoka kiwango cha asilimia 5.6 mwezi Desemba 2010 hadi kufikia asilimia 19.8 mwezi Desemba 2011. Aidha, hadi Aprili 2012, mfumko wa bei ulikuwa asilimia 18.7. Mfumko huu umesababishwa na kupanda kwa bei ya chakula hasa kwa upande wa bidhaa za mchele, unga wa sembe, mafuta ya kula na sukari; kupanda kwa gharama ya bei ya mafuta kwenye soko la dunia; kupanda kwa gharama ya nishati ya umeme na kuongezeka kwa gharama ya uzalishaji wa bidhaa muhimu za viwandani na usafirishaji.

Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Serikali kuhakikisha kuwa inadhibiti kasi ya kupanda kwa bei za bidhaa na huduma, taswira hii inaonesha kuwa bado tuna changamoto kubwa katika kuhakikisha kuwa makali ya maisha ya mwananchi wa kawaida yanapungua ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya shilingi ilishuka kwa asilimia 10.4 kutoka shilingi 1449.5 kwa Dola mwaka 2010 hadi shilingi 1599.98 mwaka 2011. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani kumesababishwa na ongezeko la uagizaji wa bidhaa na huduma nje ikilinganishwa na mauzo yetu ya nje, mahitaji makubwa ya Dola kwa ajili ya manunuzi ya mafuta kugharamia mpango wa dharura wa uzalishaji wa umeme na malighafi viwandani na anguko la uchumi kwa Nchi za Ulaya, hivyo kuifanya Dunia iwe na mahitaji makubwa ya Dola kuliko ya Sarafu ya *EURO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 5,180.6 na matumizi halisi yalikuwa bilioni 8,676.8; Deni la Taifa limeendelea kukua kwa asilimia 15.4 kutoka shilingi 17,578.9 mwaka 2011 hadi shilingi bilioni 20,276.6; akiba ya fedha za kigeni imepungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 3,948.0 mwaka 2010 hadi Dola za Kimarekani milioni 3,761.2 mwaka 2011 na hivyo kuwa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma toka nje kwa muda wa miezi 3.8. Kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 27 ikilinganishwa na asilimia 20.0 mwaka 2010; wastani wa viwango vya riba kwa amana za akiba za muda mafupi ziliongezeka kuwa asilimia 9.14 mwaka 2011 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2010. Aidha, viwango vya riba vilivyotozwa na Benki ya Biashara kwa mikopo ya mwaka mmoja ilipungua hadi asilimia 13.73 kutoka asilimia 14.14 mwaka 2010. Hata hivyo, viwango hivi bado vipo juu licha ya kuongezeka kwa ushindani katika Sekta ya Kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali ihakikishe inaweka usimamizi thabiti utakaowezesha maoteo ya ukuaji wa uchumi kukabiliana na mfumko wa bei na kushuka kwa thamani ya shilingi kwa viwango vilivyoainishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2011/12 hadi 2015/16 vinafikiwa; kwani mfumko wa bei na kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania kunaaathiri sana ukuaji wa uchumi na kuongeza gharama za uzalishaji na uendeshaji na hivyo kupunguza ushindani wa bidhaa za nchi yetu katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na misingi na shabaha ya Serikali katika utekelezaji wa bajeti hii ambazo kimsingi zinalenga kutatua changamoto zinazopaswa kuangaliwa na Serikali ili kuwa na uchumi tulivu *(Stable Economy*). Katika mwaka huu wa fedha, Serikali imejipangia kutekeleza sera za matumizi ya maendeleo kwa kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12 - 2015/16, yaani eneo la miundombinu; kilimo, mifugo na uvuvi; maendeleo ya viwanda; maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii; huduma za fedha; utalii na biashara za ndani na nje ya nchi. Usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa vipaumbele hivi na nidhamu ya matumizi ya fedha zilizoelekezwa kwenye vipaumbele hivi vilivyowekwa, itakuwa ndiyo nguzo kuu ya mafanikio ya ukuaji wa uchumi wetu ikiwa pamoja na kushirikisha sekta binafsi na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati inakubaliana na Serikali juu ya dhana nzima ya umuhimu wa kudhibiti na kusimamia matumizi makubwa ya Serikali ikiwemo kuendelea kuimarisha sera za mapato na matumizi na maboresho mbalimbali katika Sekta ya Umma ili kuimarisha ufanisi na tija

na kuhakikisha kuwa Bajeti inatekelezwa kama ilivyopangwa hasa katika miradi ya maendeleo na hivyo kuongeza juhudi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013. Kupanda kwa gharama za maisha:-

Tatizo kubwa linalojitokeza ni dhana ya uchumi kukua kwa asilimia 6.4, wakati wananchi wengi wanalalamika kuwa maisha ni magumu, hususan kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, kunakogusa maeneo yote muhimu. Kamati inaishauri Serikali juu ya umuhimu wa kuongeza uratibu katika vyombo vyake vya utendaji ili kuboresha eneo la kuendesha uchumi (*economic management*) badala ya kuelekeza nguvu zote kwenye kuendesha au kulinda utulivu wa bei (*price stability management*) unaoathiriwa na mfumko mkubwa wa bei. Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia Aprili 2012 mfumko wa bei ulikuwa asilimia 18.7 (asilimia 24.7 Aprili 2012 kutoka asilimia 9.2 Aprili 2011), ambao unachangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumko wa bei za vyakula muhimu kama mchele, unga wa sembe, mafuta ya kula na sukari. Bidhaa hizi ni muhimu na hutumiwa na watu wengi ambao kimsingi kipato chao hakiwezi kumudu bei hii kubwa ya vyakula. Kamati bado inaona kuwa jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha inakabiliana na kasi ya kupanda kwa bei za bidhaa na huduma ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumko wa bei umedumu kwa muda mrefu sasa *(Persistent Inflation)*, hivyo kuleta hisia kuwa Sera za Kifedha *(Monetary Policies)* na zile za Kodi *(Fiscal Policies)* zimeshindwa kutatua tatizo hili na kuufanya mfumko huu uwe sugu. Kamati inashauri Serikali ichukue changamoto hii kwa kuifanyia kazi ipasavyo ikiwemo pia kusimamia ipasavyo ugavi mzuri wa chakula kutoka kwenye maeneo ya ziada, kuimarisha mipango yake ya Hifadhi ya Chakula, kupatikana kwa nishati ya umeme wa uhakika. Aidha, Kodi za *VAT* kwenye vyakula muhimu kama vile mchele, unga wa sembe, sukari zifutwe au kurekebishwa, kupunguza ughali wa bidhaa hizi muhimu. Kwa mfano, sukari kutoka Kiwanda cha Kilombero huuzwa Sh.1,300/= ambapo pamoja na *VAT* bei ya sukari inakuwa Sh. 1,534/= na hadi ifike kwa mlaji inauzwa kwa Shilingi 2,200/= hadi 2,500/= kwa kilo.

Gharama hizi hazihimiliki kwa watu wenye kipato cha chini. Kamati inatambua nia njema ya Serikali ya kutoa vibali vya kununua sukari. Hata hivyo, utoaji wa vibali hivi kwa tani 500 tu kwa kila kibali umetukosesha fursa ya kuingiza tani nyingi kwa mara moja na hivyo kukosesha nafuu ya kushuka kwa bei. Serikali itumie vyombo vyake kubaini wafanyabiashara walioingiza sukari nchini na kuhodhi kwenye maghala yao wachukuliwe hatua zinazofaa. Aidha, ni muhimu Serikali ifikirie uamuzi wa uagizaji wa sukari katika mfumo wa Bulk Procument. Pia Serikali iongeze kasi ya kuboresha mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Kilimo cha miwa ili tuweze kujitoshereza katika mahitaji ya sukari kwa kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za mwaka 2011 zinaonesha kuwa Sekta ya Kilimo ambayo inahusisha idadi kubwa ya watu hasa wale wa vijijini, imechangia asilimia 6.4 ya Pato la Taifa. Hii ni pungufu ya asilimia 0.6 ikilinganishwa na mwaka 2010. Hali inaonesha ukuaji wa uchumi bado haujaweza kutegua kitendawili cha kupunguza gharama ya maisha kwa Watanzania. Kamati ina maoni kuwa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuendeleza Sekta ya Kilimo, bado hatua zilizochukuliwa hazijakuwa za kina za kuweza kusaidia wakulima wadogowadogo vijijini. Sekta ya Kilimo inaajiri takriban asilimia 75 ya Watanzania wote; hivyo, kuimarika kwa Sekta hii kutasaidia kuleta uwiano kati ya uchumi unaokua na kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Serikali imechukua uamuzi wa kuwekeza katika kilimo cha mpunga na miwa katika Mabonde Makuu ya Wami, Ruvu, Kilombero na Malagarasi na kukuza kilimo cha misitu, Kamati inaitaka Serikali ichukue uamuzi wa makusudi wa kuweka vivutio katika kilimo vitakavyogusa wakulima wote nchini, kwa maana ya wakulima wadogo vijijini, wa kati na wakubwa ili wazalishe zaidi na kuwekeza katika mabonde mengine kama vile mabonde yaliyopo katika Ukanda wa Ziwa na maeneo mengine nchini. Hatua zilizochukuliwa katika bajeti hii zinaonekana kuwagusa zaidi wakulima wa kati na wale wakubwa tu. Katika eneo hili, Kamati inasisitiza Serikali ichukue hatua zifuatazo:-

Kwanza, Serikali ihakikishe kuwa Bajeti ya Kilimo kupitia Programu zote za *ASDP, DADP,* fedha za umwagiliaji zinazoelekezwa kwenye Halmashauri za Wilaya zisimamiwe kikamilifu ili matumizi yake yalingane na thamani halisi ya fedha zilizotumika *(Value for Money).* Hivi sasa fedha nyingi zinaelekezwa kwenye kilimo, lakini uchangiaji wake katika Pato la Taifa unaendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Hoja hapa si kuongeza bajeti ya kilimo pekee, bali ni kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha zinazotengwa yatakayoleta tija na ufanisi katika sekta hii.

Pili, Serikali bila kusita ipunguze au kufuta kabisa kodi na ushuru wanaolipa wakulima kwenye Serikali za Mitaa. Nyingi ya kodi au tozo hizi mara nyingine huwa ni kero kwa wakulima wadogo. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kuongeza mapato kwenye Halmashauri, Kamati inashauri kuwa kodi ya ushuru wa mazao *(crop cess)* iwe asilimia tatu tu, kuliko ilivyo sasa ambapo Halmashauri zote zinachaji kiwango cha juu cha asilimia tano. Huu ni mzigo kwa wakulima ukilinganisha na tozo ya huduma *(service charge)* ya asilimia 0.3 anayolipa mwenye kiwanda. Takwimu hizi zinaonesha kuwa mkulima anatakiwa kulipia mara 17 ya kodi anayolipa mwenye kiwanda.

Tatu, kutekeleza mkakati wa KILIMO KWANZA ndiyo msingi wa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na kupunguza umaskini wa Watanzania walio wengi hasa wa vijijini. Hivyo, upungufu uliojitokeza katika eneo hili urekebishwe kwa ajili ya kukiwezesha kilimo kiwe cha kisayansi. Serikali iendelee kuongeza bajeti ya kilimo kila mwaka mpaka kufikia kiwango kilichowekwa katika Azimio la Maputo la asilimia kumi ya bajeti yote; kilimo cha mkataba *(Contract Farming System - CFS)* kihalalishwe kisheria kwa kutungiwa sheria mahususi; Serikali iweke vivutio sahihi vya sera na sheria kuwezesha uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo; Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo zoezi la kuainisha maeneo kwa ajili ya kilimo kwa kila wilaya; kuboresha miundombinu ya barabara vijijini, umeme, maji na huduma za kifedha na mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo; na aidha, taarifa za masoko hayo ziwafikie wakulima wenyewe.

Nne, Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(Tanzania Agriculture Development Bank)* ianzishwe katika mwaka huu wa fedha kwani imekuwa wimbo wa muda mrefu. Serikali itoe ufafanuzi kuhusu fedha zilizotengwa kwa Benki ya Rasilimali na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa mwaka huu wa fedha kama inavyooneshwa kwenye Ibara ya 77 ya Hotuba ya Waziri wa Fedha.

Tano, Serikali iweke msisitizo wa uanzishaji wa viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo *(Agro-based Processing Industries).* Pia, ihamasishe uwekezaji katika viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani ya bei ya mazao na kuongeza ajira.

Sita, kuwa na Sera thabiti na ya uwazi kuhusu uuzaji wa chakula nje ya nchi. Kutokana na mkanganyiko unajitokeza mara kwa mara katika msimu wa mavuno, Serikali iweke sera ya wazi inayoruhusu wakulima kuuza mazao nje ya nchi.

Kamati inashauri Serikali ijiandae mapema kununua mazao ya wakulima kwa bei ya soko na kuhifadhi kwenye Maghala ya Taifa ili kuhakikisha usalama wa chakula kwa Taifa na sehemu inayobaki wananchi waruhusiwe kuuza nje ya nchi. Sambamba na hili, mfumo wa kuanzisha masoko ya bidhaa za kilimo uandaliwe.

Saba, kuendelea kujenga uwezo wa sekta binafsi hasa wawekezaji wadogo na wafanyabiashara wadogo kitaaluma, kimuundo na kuwapatia fedha za kuendeshea miradi kupitia Mifuko mbalimbali ukiwemo wa *Financial Sector Deepening Trust*. Kamati bado inapendekeza Serikali isaidie kuboresha kupitia Vyama vya Ushirika, *SACCOS, VICOBA* na vikundi vingine vya uzalishaji.

Nane, Serikali iandae mkakati maalumu wa kuwawezesha vijana kujiajiri katika Sekta ya Kilimo kwa kuwatengea maeneo ya kilimo, kuwapatia vifaa vya kilimo, pembejeo na mikopo yenye masharti nafuu. Msisitizo uwekwe kwenye mazao ya kilimo cha mbogamboga, maua, matunda na kadhalika, ambacho kitawasaidia kuwapatia vipato kwa haraka. Aidha, wapatiwe mafunzo ya kilimo bora ili shughuli zao ziwe na tija.

Tisa, Serikali lazima isimamie kwa ufanisi eneo la ruzuku ya pembejeo kwa wakulima. Umakini mkubwa unahitajika ili pembejeo hizi ziwe na ubora unaotakiwa, ziwafikie wakulima kwa wakati na kwa bei wanazozimudu, la sivyo, pembejeo hizi zinaweza zisilete mafanikio yaliyotegemewa. Uwakala wa pembejeo zote ufanyiwe tathmini na ufuatiliaji wa mara kwa mara ili ulete tija na ufanisi katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali ichukue maamuzi ya makusudi juu ya hatua zilizoainishwa hapo juu ili kuwapunguzia mzigo wakulima wadogo, wa kati na wakubwa. Sekta ya Kilimo ndiyo yenye uwezo mkubwa wa kukuza uchumi wetu kwa haraka hasa kama Serikali itatoa kipaumbele na kuweka vivutio sahihi vitakavyoweza kuimarisha na kukuza uzalishaji na ajira katika sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hali ya chakula iliendelea kuwa nzuri katika maeneo mengi nchini kwa kipindi chote cha mwaka. Hata hivyo, mazao ya chakula yalipanda bei na kusababisha mfumko wa bei ya chakula.

Mikoa ya Kusini iliendelea kuwa na ziada kubwa ya chakula na kuna baadhi ya maeneo tete yalikumbwa na upungufu mkubwa wa chakula na jitihada za Serikali kuinusuru hali hii zilionekana. Kwa kuwa Mkoa wa Morogoro unatekeleza Mpango wa FANYA MOROGORO KUWA GHALA LA TAIFA (FAMOGATA) ndani ya KILIMO KWANZA na uliandaa mkakati mahususi mwaka 2009 kama njia mojawapo ya kuanza utekelezaji wa mpango huo; Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa Mkoa wa Morogoro ili mkakati huu ufanikiwe kutekelezwa ili tuweze kujitosheleza na kuwa na usalama wa upatikanaji wa chakula. Aidha Programu Kabambe ya Kuendeleza Shughuli za Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT)* kupitia ubia wa Sekta ya Umma na Binafsi, utekelezaji wake uharakishwe mapema ili kutekeleza azma ya KILIMO KWANZA. Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi changamoto zote zilizopo kwenye Sekta ya Kilimo ili kuwezesha utaratibu wa uwekezaji wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kukuza Sekta ya Kilimo kupitia *SAGCOT*. Utekelezaji wa Mpango ya *SAGCOT* na mipango ya uzalishaji wa chakula, uende sambamba na ujenzi wa maghala katika maeneo yenye ziada ya uzalishaji wa chakula ndani ya Ukanda huo. Pia, Serikali iendelee kuongeza akiba ya chakula kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi kuwa na fursa kubwa na kuwa chanzo muhimu katika kuchangia katika Pato la Taifa, bado Sekta hizi hazijatumika ipasavyo na wala hazijafanyika jitihada za kutosha kuzikuza na kuvutia uwekezaji. Bajeti ya mwaka huu haitengi fedha za kutosha kwenye Sekta ya Ufugaji na Uvuvi. Sehemu kubwa ya fedha zilizotengwa ya shilingi bilioni 262 zinaelekezwa kwenye shughuli ya kilimo; hivyo, kuendelea kudumaza Sekta hizi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya mifugo bado inakumbwa na changamoto za kukosekana kwa miundombinu ya mabwawa na malambo ya kunyweshea mifugo, huduma za ugani, madawa, maeneo yaliyotengwa mahususi kwa ajili ya malisho na kukosekana elimu ya ufugaji bora, ukosefu wa mitamba na madume bora ya borani ili iwe bora hasa katika kutoa nyama yenye ubora wa hali ya juu na mazao ya mifugo. Kamati inashauri katika mwaka ujao wa fedha, zitengwe fedha za kutosha kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Sekta hii. Aidha, Serikali iweke mikakati ya muda mfupi, kati na mrefu. Kwa kipindi cha mkakati wa muda mfupi, Serikali ijikite katika kujenga malambo, mabwawa na majosho kwenye maeneo ya wafugaji yakiwemo ya Manyara, Dodoma, Arusha, Singida, Shinyanga, Simiyu, Katavi, Mara, Tabora, Mwanza na Geita. Aidha, Serikali itumie mfumo wa utawala katika Serikali za Mitaa, kuwaelimisha wafugaji kutumia mifugo yao kuwaletea mabadiliko ya maisha.

Kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu, Serikali ihamasishe uanzishwaji wa viwanda vya usindikaji wa nyama na mazao ya mifugo katika maeneo ya wafugaji. Pia ibuni Programu Maalumu ya Mifugo inayofanana na *SAGCOT* kwa maeneo hayo tuliyoyataja ili kuboresha mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Mifugo na kichangie ukuaji wa uchumi na kunufaisha wafugaji katika kupambana na umaskini. Aidha, Serikali iendelee na mkakati wa kusomesha maafisa ugani na mifugo ili waweze kupelekwa maeneo ya vijijini na wawezeshwe kuwa na mashamba darasa ya mifugo ili waelimishe wafugaji ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zana duni za uvuvi, elimu bora ya ufugaji wa samaki, kutokuwepo na vivutio sahihi vya uwekezaji, kutokuwepo kwa viwanda vya kutosha vya kusindika samaki na mfumo kandamizi wa masoko ya nje ya samaki na kadhalika. Kutokana na changamoto zilizopo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

Moja, Serikali ifanye mapitio ya vivutio vilivyopo ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Msisitizo uwekwe katika uanzishaji wa viwanda vya usindikaji wa samaki na miundombinu ya kuhifadhi na kusafirishia samaki.

Pili, kwa uwekezaji wa ndani, Serikali ihakikishe inawawezesha wananchi kupata mitaji itakayowawezesha kupata zana za kisasa za uvuvi.

Tatu, Programu za Uwezeshaji Wananchi kama *Small Entrepreneurs Loan Facility (SELF),* zitumike kuwezesha wananchi hususan vijana na wahitimu wa vyuo vya uvuvi kuingia katika Sekta ya Uvuvi. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa taaluma ya mafunzo stahiki ya uvuvi inaimarishwa na kutolewa kwa wananchi ili waweze kutumia teknolojia ya kisasa kuendesha biashara hii kwa ufanisi.

Nne, Serikali iwekeze katika ufugaji wa samaki kwenye mabwawa, mito na bahari. Aidha, Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itumike katika kufanikisha suala hili. Pia ibuni Programu Maalumu ya Uvuvi inayofanana na *SAGCOT* kwa maeneo ya mito, ziwa na bahari kuu ili kuboresha mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi. Mfano mzuri wa kuigwa ni ule wa nchi ya Kenya ambayo kwa mwaka wa fedha 2009/10 na 2010/11; Serikali ya Kenya ilitoa Shilingi za Kenya bilioni 3.986 kwa ajili ya Mradi wa Uchimbaji wa Mabwawa ya Samaki katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha fedha kilichopita, Sekta ya Utalii iliingizia Taifa kiasi cha fedha za kigeni Dola za Kimarekani bilioni 1.35 na inaajiri asilimia 6.7 ya ajira zote na imeendelea kukua mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, kitakwimu pamoja na kuwa ya pili duniani katika kuwa na vivutio vya utalii, Tanzania ni ya 110 katika ushindani wa kitalii. Pamoja na vivutio hivi, bado nchi haijanufaika kiuchumi ukilinganisha na rasilimali za utalii zilizopo. Suala la kujiuliza hapa ni kwa nini hali hii ipo hivi? Suala hili ni changamoto kubwa kwa Serikali, Kamati inashauri kupitia upya Sera, Sheria na Kanuni za Utalii ili kuweka mazingira bora ya kuendeleza utalii wenye lengo la kukuza uchumi na kuongeza kipato kwa Watanzania. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili kutangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu duniani kote na kufanya utafiti wa mapato yatokanayo na utaratibu wa *package tours.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi duniani inayoweza kuendelea bila ya msukumo mkubwa katika uwekezaji na ushiriki wa sekta binafsi. Hata hivyo, ili uwekezaji ushamiri unahitaji kujengewa mazingira mazuri ikiwa pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji na uendeshaji wa biashara *(reducing cost of doing busness*). Urasimu, ucheleweshaji wa kutoa maamuzi ya msingi na baadhi ya sheria, kanuni na taratibu zilizopitwa na wakati, zinaendelea kukwamisha ari ya uwekezaji nchini. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali iangalie haya yote kwa umakini ili kuwezesha sekta binafsi kuwa mshiriki mkuu wa maendeleo katika nchi. Mahusiano yaliyoanzishwa Kisheria baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi chini ya utaratibu wa *PPP,* hauna budi kuimarishwa ili kupata mitaji ya kutosha katika maeneo ya kipaumbele tuliyojiwekea katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchini Tanzania zipo benki takribani 47, lakini wananchi wengi vijijini na mijini hawajafaidika vya kutosha na huduma hii. Viwango vikubwa vya riba na masharti magumu ya upatikanaji wa mikopo imekuwa ni kikwazo kwa Watanzania wengi kunufaika na huduma za fedha. Takwimu zinaonesha chini ya asilimia 13 ya Watanzania wote ndio walinufaika na huduma hizi. Hii ni changamoto kubwa kwa Serikali.

Utaratibu wa *Mortage Financing* na *Financial Leasing* ulioanzishwa bado haujasaidia sana kuondoa adha na kero ya ukosefu wa nyumba za gharama nafuu kwa wananchi wenye

kipato kidogo. Kamati inapendekeza Serikali iweke msisitizo na usimamizi mzuri katika maeneo haya ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la miundombinu linahitaji kupewa kipaumbele cha pekee katika kuhakikisha kuwa tunapiga hatua za haraka za kukuza uchumi wa nchi. Katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Serikali imepanga kuimarisha miundombinu ya nishati, barabara, reli, bandari, usafiri wa anga na mawasiliano. Kamati inasisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za haraka za kuboresha utendaji kazi wa Bandari zetu, yaani za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara. Kamati imepitia Bajeti ya Serikali kwenye eneo hili na kuona kwamba, inaridhika na hatua zinazochukuliwa na Serikali kwenye umeme na Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Hata hivyo, kwenye Sekta ya Usafirishaji na Uchukuzi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa bandari Dar es Salaam na ujenzi wa bandari mpya ya Tanga na Mtwara, ukarabati wa Reli ya Kati na ile ya Tanga. Aidha, suala la kutumia nafasi ya kijiografia *(geographical position)* ya nchi yetu hasa katika kuhudumia nchi jirani ni muhimu kupewa kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na matatizo ya kulipa hati za malipo ya wakandarasi kwa wakati na kusababisha wakandarasi na wahandisi washauri kusitisha au kupunguza kasi ya utekelezaji wa Miradi ya barabara na ujenzi wa viwanja vya ndege. Aidha, misamaha ya kodi kwa vifaa vya ujenzi vya wakandarasi vinachelewa na hivyo kuwachelewesha kutekekeleza Miradi kwa wakati. Baadhi ya wahisani nao hawatoi fedha za Miradi kama wanavyokubaliana na Serikali. Hii ni changamoto kwa Serikali kufuatilia suala hili. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha katika kipindi hiki cha mwaka 2012/13, madeni yote ya wakandarasi yanalipwa ili kuwezesha Miradi hii ya miundombinu kukamilika kwa wakati. Aidha, ucheleweshaji wa malipo unasababisha kuwalipa wakandarasi hao madeni yao pamoja na riba. Pale ambapo Serikali ina mkataba na wahisani ambayo imewekewa masharti ya upatikanaji wa fedha *(counterpart fund),* masharti hayo yatekelezwe kwa wakati ili fedha hizo zipatikanae kwa wakati uliopangwa. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania - *TANROADS* na Shirika la *Millenium Challenge Corporation (MCC)*, kwa kuweza kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Miradi ya Barabara inayofadhiliwa na Shirika hilo ambayo inaendelea kutekelezwa kwa wakati kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa nishati ya umeme bado unaendelea kuwa kikwazo kikubwa katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na kuwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umeweka kipaumbele katika Miradi ya Uzalishaji Umeme, bado Kamati inasisitiza Sekta Binafsi ihamasishwe kuwekeza katika uzalishaji wa umeme na mkakati huo ukiambatana na uboreshaji wa mazingira yatakayotoa msukumo wa uwekezaji *(investment drive*). Nguvu zaidi zielekezwe katika Mradi wa Kiwira, unaoweza kuzalisha MW 200 katika kipindi kifupi kijacho pamoja na Mradi wa Mchuchuma MW 300 ambao unasimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC).* Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza vyanzo mbadala vya umeme kama vile umeme wa nguvu za jua, miwa na upepo, gesi, *biogas* na *geothermal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijitahidi kukamilisha Mradi wa Bomba la Gesi kwa muda uliopangwa. Hivyo, Serikali ifanye kila linalowezekana kukamilisha majadiliano kati yake na Serikali ya China ili kuwezesha Mradi huu kuanza mapema. Mradi huu ni muhimu ikizingatiwa utakapokamilika na kufika Dar es Salaam, utafanya nchi yetu kuondokana na Miradi ya Umeme wa Dharura unaotokana na mitambo ya kukodisha inayotumia fedha nyingi mno. Utekelezaji wa mpango wa dharura wa kuwezesha nishati hii kupatikana, umeigharimu Serikali kutoa fedha takriban shilingi bilioni 288 katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na taarifa ya Serikali kuwa hadi sasa kuna takribani miradi ishirini iliyowasilishwa ili itekelezwe kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP),* mfano ni Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini na ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze *(express way).* Kamati inahimiza Serikali kuongeza kasi ya maandalizi ya Miradi mingine kwenye maeneo ya vipaumbele. Kamati inaamini kuwa utekelezaji wa miradi ya ubia utapunguza mzigo kwenye Bajeti ya Serikali na hivyo kuiwezesha Serikali kuelekeza rasilimali zake kwenye huduma nyingine au maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Agosti, 2012 tunategemea kufanya Sensa ya Watu na Makazi. Upatikanaji wa takwimu hizi ni muhimu kwa Serikali kuweza kupanga mipango yake ya maendeleo na kuandaa sera mbalimbali zenye manufaa kwa jamii nzima. Kamati imeridhishwa na hali ya maandalizi ya Sensa na bado inasisitiza Serikali kufuata ratiba ya Sensa na kuhakikisha rasilimali fedha inapatikana mapema kama ilivyoainishwa kwenye Bajeti ya Sensa. Pia Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa kutoa elimu ya kutosha juu ya zoezi zima la sensa hasa katika ngazi za chini ambako ndiko kwenye wananchi. Aidha, kabla ya zoezi zima kuanza, Serikali ihakikishe inapata takwimu sahihi za maeneo ya kiutawala yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuweza kuvuka lengo la makadirio ya mapato iliyojipangia kukusanya kwa kipindi cha Julai 2011 hadi machi 2012. Takwimu zinaonesha kuwa, kiasi cha shilingi bilioni 4,765.5 kilikusanywa, hii ikiwa ni sawa na asilimia 104 ya makadirio yote. Aidha, ukusanyaji wa mapato yasiyo na kodi umekuwa siyo wa kuridhisha kutokana na baadhi ya Mashirika na Taasisi kushindwa kukusanya kiwango kilichokadiriwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi cha shilingi bilioni 272.1 tu ndiyo kimekusanywa, hii ikiwa ni asilimia 57 ya lengo lililokusudiwa. Kamati inaona haja ya Serikali kufuatilia kwa ukaribu taratibu za uendeshaji na utendaji kazi wa mashirika na taasisi hizi ili kuongeza mapato katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Vikao vya Kamati, Kamati ya Fedha na Uchumi ilipokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya Mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/13 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013. Hata hivyo, katika majadiliano, Kamati iliwasilisha hoja yake kuwa ushauri wa Bunge katika kipindi kilichopita, ilikuwa uwiano wa Bajeti ya Serikali kwa upande wa matumizi ya maendeleo iwe asilimia 35 na bajeti ya matumizi ya kawaida iwe asilimia 65 tofauti na mgawanyo wa uwiano huu wa sasa wa asilimia 30 kwa 70. Aidha, baada ya mjadala na maelezo ya kina kutoka kwa Waziri wa Fedha, Kamati ilikubaliana na Bajeti ya Serikali kwa mwaka huu kwa kuzingatia hali halisi ya mapato ya sasa, ufinyu wa muda uliopo, shughuli zinazoendelea zisizoepukika na mahitaji ya sekta mbalimbali. Kwa mfano, uendeshaji wa Sensa, Tume ya Kuratibu Maoni Kuhusu Katiba Mpya na kadhalika. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa bajeti zijazo, uwiano wa matumizi ya maendeleo uwe wa asilimia 35 ya Bajeti yote ya Serikali na uendelee kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya bajeti ya mwaka 2011/12 inaonesha uwiano wa asilimia 63 kwa matumizi ya kawaida na asilimia 37 kwa matumizi ya maendeleo. Hata hivyo, Bajeti ya sasa, kwa mujibu wa Hotuba ya Bajeti, Ibara ya 118, inaonesha kwamba hali halisi ya matumizi ya maendeleo itakuwa asilimia 22 tu badala ya 37 kama iliyotarajiwa. Hali hii inaonesha kuwa uchumi wetu utaendelea kuwa wa utumiaji mkubwa ikilinganishwa na uzalishaji *(net consumer nation)*; hii ni hatari kubwa kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mwaka ujao wa Fedha (2012/13), Serikali imepanga kukusanya mapato ya ndani na ya nje kiasi cha shilingi bilioni 15,045.8 (Trilioni 15.12); kati ya hizo makusanyo ya ndani ni shilingi trilioni 8.71 na mikopo na misaada ni shilingi trilioni 6.41. Aidha, matumizi ya kawaida yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 10,518 (Trilioni 10.5), kiwango ambacho ni kikubwa zaidi kuliko mapato yetu ya ndani. Upande wa matumizi ya maendeleo, Serikali imepanga kutumia bilioni 4,527.8 (Trilioni 4.5); kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 2,213.6 na shilingi bilioni 2314.2 ni fedha za nje. Hali hii inaonesha kuwa Bajeti ya Serikali bado inategemea zaidi misaada na mikopo kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo.

Kamati inaona kuwa mfumo iliyojiwekea Serikali unaweza kuwa ndiyo sababu ya uwezo mdogo wa Serikali wa kudhibiti vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni dhahiri vingeboresha Bajeti hii. Inaonekana Serikali bado haijaweza kufikia maeneo mengine ambayo yanaweza kuwa vyanzo muhimu vya mapato yatakayowezesha kugharamia bajeti yake na hivyo kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi. Kamati inasisitiza kuwa suala muhimu ni kwa Serikali kuwa na ubunifu, kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kuepuka kuendelea kung'ang'ania *(concentrate*) vyanzo vichache vilivyozoeleka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati bado inasisitiza umuhimu wa nidhamu ya matumizi ya Serikali na uwezo wa kuongeza mapato. Kamati inaendelea kushauri kwamba, Serikali iachane na mtindo wa kuibua matumizi mapya yasiyo ya dharura, ambayo hayakuidhinishwa na Bunge wakati wa utekelezaji wa Bajeti; kwani mtindo huo unavuruga bajeti na kupunguza uwezo wa kutoa fedha za matumizi mengineyo *(OC)* na matumizi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa. Kamati inasisisiza juu ya umuhimu wa Serikali kubana matumizi kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati bado inasisitiza Serikali kuchukua hatua zifuatazo ili kuhakikisha mapato yetu ya ndani yanaongezeka:-

Kuangalia eneo la sera na taratibu za ukusanya wa kodi; *TRA* iongeze jitihada za kutekeleza mpango mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa kodi; Serikali iendelee kujenga mazingira mazuri ya kuwezesha kuongeza uzalishaji wa bidhaa za ndani na kuweza kuuza nje ili kuongeza fedha za kigeni; Serikali ipanue wigo wa kukusanya kodi ili iongeze mapato kupitia sekta isiyo rasmi; Serikali iimarishe utaratibu wa kutoza kodi za majengo *(property tax);* na Serikali itumie Sheria mpya ya Madini ya Mwaka 2008 ili kupata mapato mengi kutokana na shughuli za Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ongezeko kubwa la uanzishwaji wa Mashirika ya Umma kupitia kivuli cha Wakala za Serikali *(Executive Agencies)* bado linahitaji ufumbuzi kutoka kwa Serikali. Kamati inaamini kuwa, fedha za Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali na Vyombo vya Udhibiti *(Regulatory Authorities),* kama zingekuwa zinaingia Serikalini, Mapato ya Serikali yangekuwa mengi kuliko sasa. Kamati inaishauri Serikali kutafuta utaratibu wa kurekebisha kasoro hii ya kutokupata mapato kutoka kwa baadhi ya Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali (*Executive Agencies*), Mifuko ya Hifadhi za Jamii na hata baadhi ya Mamlaka. Mfumo huu umesababisha Serikali kupoteza vyanzo muhimu vya mapato ambayo yangeingia Serikalini kama maduhuli. Taasisi hizi nyingi zina ukwasi wa kutosha kutokana na kutoza ada na tozo mbalimbali kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetafakari mapendekezo ya Serikali kupitia bajeti yake kwenye maeneo ya kodi na tozo mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2012/13. Kamati inayaafiki maeneo mengi yanayopendekezwa na Serikali kufanyiwa maboresho. Hata hivyo, yapo maeneo machache ambayo Kamati inaishauri Serikali kuyaangalia upya kama ifutavyo:-

Moja, Katika jedwali la ukurasa wa 62 wa Hotuba ya Waziri, tabaka namba mbili kama ilivyo namba moja, linakusanya vijana wengi wanaofanya shughuli mbalimbali zikiwemo bodaboda, mama lishe, vibajaji na kadhalika, zinazowapatia vipato halali kwa maana ya kujiajiri wenyewe. Ukizingatia kuwa ajira ni suala muhimu kwa vijana, Kamati inashauri Serikali iangalie upya eneo hili kwa maana ya kupata unafuu wa kodi kwenye tabaka hili.

Mbili, kutokana na umuhimu wa zao la pamba nchini linalotoa ajira kwa wakulima wadogo wapatao 500,000 na kuwezesha maisha ya Watanzania wapatao milioni 16. Kwa madhumuni ya kufufua viwanda vya nguo hapa nchini na hivyo kuongeza uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na pamba kama vile nyuzi, majora ya nguo na mavazi ya pamba na hivyo kukuza soko la pamba nchini, kukuza ajira hasa kwa vijana na kuhimili ushindani usio wa haki wa bidhaa za nguo za pamba zinazotoka nje, Kamati inapendekeza viwanda vya nguo nchini vipewe misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye bidhaa za nguo na mavazi. Aidha, utozaji wa ushuru kwa bidhaa za pamba zinazotoka nje utumie utaratibu wa viwango maalumu *(specific rates)* badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza ushuru kulingana na thamani ya bidhaa za nguo na mavazi *(add valorem),* ambapo kuna udanganyifu mkubwa *(under invoicing),* unafanyika na hivyo kuinyima Serikali mapato.

Tatu, Kamati imeelewa nia ya Serikali ya kutaka kuwianisha ushuru wa bidhaa ya matumizi ya muda wa simu *(air time)* kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, inatambua ushuru wa bidhaa siyo miongoni mwa kodi za Jumuiya za Afrika Mashariki; hivyo, Kamati inapendekeza kiwango cha sasa cha asilimia kumi kiendelee kutumika. Aidha, Kamati inapendekeza ianzishwe kodi mpya itakayolipwa kwa anayesajiliwa upya au kubadilishiwa *sim card*. Kamati inapendekeza tozo ya shilingi 1,000 kwa kadi.

Nne, Serikali katika bajeti hii imeazimia kutoza *export levy* kwa ngozi kwa kiwango cha asilimia 90. Kutokana na udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wa ngozi (*under invoicing)*, pendekezo hili halitatoa matokeo yanayokusudiwa. Kamati inashauri Serikali kupiga marufuku usafirishaji wa ngozi ghafi nje ya nchi kama ilivyofanya nchi jirani ya Uganda na Ethiopia. Kwa kupiga marufuku tutashawishi uanzishwaji wa viwanda vya kusindika ngozi hapa nchini na kuongeza thamani ya bidhaa za ngozi na kuongeza ajira. Uzoefu unaonesha tokea mwaka 2007 kodi za bidhaa za ngozi ilikuwa asilimia 40 kwa madhumuni ya kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kusindika ngozi hapa nchini, lakini hakuna hata kiwanda kimoja kilichoanzishwa.

Tano, Ibara ya 97(iv) ya Hotuba ya Waziri wa Fedha inapendekeza kuanzisha kodi itokanayo na uuzaji wa rasilimali ya uwekezaji *(Capital Gains Tax)* kwenye uuzaji wa hisa za kampuni za ndani unaofanywa na kampuni mama ya nje ya nchi.

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo. Hata hivyo, Kamati inashuri utekelezaji wa pendekezo hili ufanywe kwa umakini zaidi kuliko pendekezo linavyosomeka hivi sasa. Kamati inapendekeza pale panapofanyika mauzo ya hisa katika kampuni ambayo ni kampuni mama ya kampuni tanzu iliyosajiliwa Tanzania, mauzo hayo ya hisa yatachukuliwa kuwa ni mauzo pia ya hisa katika kampuni tanzu inayomilikiwa na hiyo kampuni mama hapa nchini. Hivyo, *transaction* hiyo itatozwa *capital gain tax* tofauti na utaratibu wa sasa. Ili kujenga mazingira mazuri ya uhiari wa makampuni kulipa kodi hiyo, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kushusha kiwango cha sasa cha asilimia thelathini na kuifanyia marekebisho Sheria ya Stempu ya Mwaka 1972 *(Stamp Duty Act, 1972)* ili mauziano ya hisa kwa sura iliyoelezwa hapo juu yaweze kutozwa ushuru wa stempu tofauti na ilivyo sasa.

Sita, kwa upande wa *SDL,* Kamati inashauri kwa kuanzia tozo hii ipungue kutoka asilimia sita hadi nne na wigo wa walipaji upanuliwe kwa kuhusisha baadhi ya taasisi na Wakala wa Serikali na mgawanyo uwe kama ifuatavyo: Asilimia mbili ipelekwe *VETA* na asilimia mbili ipelekwe kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, pengo litakalojitokeza, Serikali ingalie vyanzo vingine vya kuweza kuliziba. Aidha, utafiti umeonesha kuwa kuna waajiri wengi katika sekta binafsi wanaostahili kulipa kodi hii lakini wapo nje ya wigo, endapo wakiingizwa katika wigo wa kodi na wakilipa kwa asilimia 100, kiasi cha shilingi trilioni mbili kinaweza kupatikana. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali ifuatilie suala hili ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mapato. Pia, Serikali kwa kipindi kijacho, itafute namna ya kupata mapato kwa ajili ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu badala ya kutumia utaratibu huu wa sasa wa kukata asilimia nne kutoka asilimia sita ambazo zinakatwa kwenye *skills and development levy* inayochangiwa na sekta binafsi pekee.

Saba, Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria za Kodi zinazoikabili sekta binafsi. Kwa muda mrefu, wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kuwa Serikali imekuwa ikiwabebesha mzigo mkubwa wa kodi mbalimbali ambazo zinaathiri uzalishaji wa sekta zao. Kamati imeainisha maeneo ya kodi yanayolalamikiwa kuwa ni:-

- Ushuru wa Hoteli *(Hotel Levy)*: Sekta Binafsi inaomba ushuru huu upunguzwe kutoka asilimia 20 ilivyo sasa hadi asilimia 16. Kamati imetafakari ombi lao na inashauri Serikali kushusha kiwango cha kodi hiyo mpaka asilimia 18 ili iendane na kiwango cha sasa cha Kodi ya *VAT;*
- Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT):* Sekta Binafsi inaomba ipunguzwe kutoka asilimia 18 hadi asilimia 16 kama ilivyo Kenya. Kamati inaishauri Serikali iendelee kulifanyia kazi pendekezo hili pamoja na kuharakisha ukamilishaji wa zoezi la kuifanyia mapitio Sheria ya *VAT;*

- *Taxpayers' Refunds Entitlement for Other Tax Obligations:* Sheria ya sasa ya *VAT* inaipatia *TRA* haki ya kutumia marejesho *(refund)* ya mlipa kodi kujilipa kodi wanazodai kutoka kwa mlipa kodi. Sekta Binafsi inapendekeza na wao wapewe fursa kama hiyo pindi wanapoidai *TRA* marejesho yao ya kodi. Kutokana na ucheleweshaji wa marejesho haya, Kamati inaishauri Serikali ilifanyie kazi pendekezo hili;

- Kufuta *Alternative Minimum Tax (AMT).* Sheria ya Kodi ya Mapato ilifanyiwa marekebisho kuanzisha hii kodi, lengo lake lilikuwa ni kutoza kodi ya mapato kwa makampuni ambayo hayapati faida baada ya kukokotoa gharama kwa misingi ya kihasibu kwa miaka mitatu mfululizo. Kodi ya mapato inatozwa kwenye faida iliyopatikana kwa mwaka husika haitozwi kwenye mauzo. Sekta Binafsi inapendekeza kodi hii ifutwe kwa sababu imeangukia katika mauzo badala ya faida. Kamati inakubaliana na ombi hili na inashauri Serikali iifute kwa kuwa inakinzana na Sheria ya Kodi ya Mapato *(Income Tax);*

- Kupunguza mrabaha unaotozwa kwenye kamba na minofu ya samaki *(royalty rates on prawns and fish fillets).* Viwango vya mrabaha kwa kamba na minofu ya samaki ni Dola za Kimarekani 0.840 kwa kilo ya kamba na 0.120 kwa kilo ya minofu ya samaki. Kiwango hiki ni kikubwa ukilinganisha na Nchi ya Kenya na Uganda. Sekta Binafsi inapendekeza kiwango kiwe Dola za Kimarekani 0.2 kwa kilo ya kamba na 0.05 kwa kilo ya minofu ya samaki ili kujenga mazingira ya ushindani wa haki katika soko. Kamati inakubaliana na ombi hili na inaishauri Serikali ikubali kupunguza mrabaha kama ilivyoombwa;

- Kufuta ushuru unaotozwa kwenye magari kwa ajili ya utumiaji wa barabara *(Annual Motor Vehicle Road License (AMVRL) Fees):* Serikali imeanzisha tozo ya mafuta *(fuel levy)* kwa madhumuni ya kukarabati na kutengeneza barabara. Wakati wanaanzisha utaratibu wa kusajiliwa magari kwa kutumia kompyuta, walianzisha pia tozo kwenye magari kwa ajili ya utumiaji wa barabara *(Annual Motor Vehicle Road License (AMVRL) Fees)*. Hatua hii inamfanya mmiliki wa gari achangie mara mbili kwa lengo moja. Sekta Binafsi inaomba tozo hii ya magari ifutwe kwa sababu inawatoza wamiliki wa magari mara mbili hivyo inapendekezwa kurejea kwenye madhumuni ya kuanzishwa kwa *fuel levy*. Kamati inakubaliana na pendekezo hili na inaishuri Serikali ifanyie kazi suala hili;

- Kufuta ushuru wa asilimia 0.3 kwa mawimbi ya simu unaotozwa kwenye minara ya mawasiliano *(Abolish Service Levy and Refuse Collection Levy on Telecommunication Towers).* Tozo hii inatolewa kwenye mawimbi yanayopita kwenye minara iliyopo katika kila eneo la Halmashauri ya Wilaya na Miji. Sekta Binafsi inasema ni vigumu kujua kwa uhakika kiwango cha mawimbi kinachopita katika kila mnara na hivyo kupelekea kulipa tozo ya asilimia 0.3/mawimbi. Pia kuna tozo ya ukusanyaji wa uchafu unaofanywa na mawimbi yanayopita kwenye minara *(refuse collection levy)* ya 0.3. Hakuna huduma ya kusafisha uchafu wa mawimbi inayotolewa na mamlaka ya Wilaya na Miji hivyo wanaiona hii kama ni kodi ya kero. Kamati inashauri kuwa suala hili ni la kiutaalamu na kiufundi, Serikali ilifanyie kazi kupitia *TCRA;*

- Kuwasilisha *VAT Returns and Payments* kila baada ya miezi mitatu. Sekta Binafsi ambao ni walipa kodi wanapendekeza kuwa utaratibu wa sasa wa ku-*file returns* kwa kila mwezi ubadilike na wa *file returns* kila baada ya miezi mitatu. Wakati Sheria ya Kodi ya Mapato inaruhusu ku-*file returns* kila baada ya miezi mitatu, Sheria ya *VAT* inawataka wa-*file returns* kila mwezi. Hii ina usumbufu na inaongeza gharama za ulipaji kodi *(compliance costs).* Sekta Binafsi inaomba Sheria hii ya *VAT* irekebishwe ili waruhusiwe ku-*file returns* kila baada ya miezi mitatu kama ilivyo kwa Sheria ya Kodi ya Mapato. Kamati inakubaliana na hili na inaishauri Serikali ilikubali; na

- Kodi ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati katika Sekta Isiyo Rasmi *(Taxation of Small and Medium Enterprises (SMES) and the Informal Sector).* Tafiti nyingi zimefanyika na kutoa mapendekezo kuhusu suala la kupanua wigo wa mapato kupitia sekta isiyo rasmi. Hata hivyo, mapendekezo hayo bado Serikali haijaipa uzito unaostahili. Kamati inapendekeza tafiti hizo zifanyiwe kazi mapema iwezekanavyo ili kuongeza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa mbogamboga, maua na matunda *(horticultural industry),* kwa muda mrefu wanalalamikia kodi ya forodha inayotozwa kwa vifungashio (*kraft paper and starch*) ya asilimia 25 ni kubwa mno, inaongeza gharama ya uzalishaji na inaua ushindani, hivyo, wanapendekeza ifutwe. Kamati inakubaliana na ombi hili kwa sababu kama ikifutwa itasaidia kuumudu ushindani, pia itatoa motisha kwa vijana wengi kujiajiri au kuajiriwa na Sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kulifanyia kazi suala hili. Aidha, Vyandaraua vinavyotumika katika kilimo (*agro-net*) vinatozwa *VAT* ya asimilia 18 wakati viuwadudu na madawa ya kilimo hayatozwi kodi. Kamati inashauri Serikali kodi hii ifutwe kwa sababu haioni mantiki ya msimamo huo wa Serikali kwa eneo hilo hilo na kwa shabaha hiyo hiyo.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, nane, kulinda mazao yanayotoa mafuta ya kula. Tanzania inaingiza mafuta ya kula nchini kwa takriban tani 300,000 kwa mwaka. Hili ni kadirio la asimilia 55 ya mafuta yote ya kula yanayotumika hapa nchini. Kwa hiyo, tunatumia fedha za kigeni nyingi kuingiza bidhaa hii kutoka nje wakati mazao ya alizeti, pamba, karanga, mawese, ufuta na kadhalika ambayo ni vyanzo vikubwa vya mafuta ya kula yanalimwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali itoze ushuru mkubwa kwa mafuta yanayotoka nje ya nchi ili mafuta yetu kwa maana yanayozalishwa hapa nchini, yamudu ushindani kwenye soko la ndani na nje ya nchi na pia kodi zinazotozwa kwa viwanda vinavyosindika mafuta hapa nchini hasa *VAT* ziangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, hivi sasa bado kuna changamoto ya kutoza kodi kwenye mashine, vifaa vya umwagiliaji na vipuri vya matrekta ya kilimo, jambo ambalo haliendi sambamba na Dhana ya KILIMO KWANZA. Kamati inapendekeza kuwa, kodi kwenye vifaa hivi ifutwe ili kuhamasisha watu walio wengi kushiriki katika shughuli za kilimo na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya Serikali yanayotokana na vyanzo vya ndani (vyanzo vya kodi na visivyo vya kodi) ni muhimu sana katika kulijengea Taifa letu uwezo wa kugharamia kwa kiwango kikubwa, kama si chote, matumizi ya kawaida ya Serikali na hivyo kuikwamua nchi yetu katika utegemezi wa kibajeti. Taarifa za mapato kwa mwaka unaoishia Juni 30, 2011 zinaonesha kuwa, kiasi cha shilingi bilioni 1,016.3 kilikuwa ni misamaha ya kodi iliyotolewa kwa Mashirika ya Umma, Miradi ya Wafadhili, Taasisi zisizo za Kiserikali, Taasisi za Dini, Sekta ya Madini, Makampuni na Watu Binafsi, Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), misamaha chini ya Sheria ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na misamaha ya kodi katika maduka yasiyotozwa kodi *(Diplomatic Duty Free Shops)*. Kiwango hicho cha misamaha ya kodi ni sawa na asilimia 18 ya makusanyo yote kwa mwaka husika wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2011/12, Kamati ilishauri Serikali ichukue hatua za dhati za kupunguza misamaha hiyo ili ifikie asilimia moja ya Pato la Taifa kama ilivyo kwa nchi wanachama wengine katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushauri huu wa Kamati bado haujafanyiwa kazi na Serikali, badala yake katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/13, katika Ibara ya 67 ya Hotuba ya Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha amerudia kibwagizo kile kile cha mwaka jana kwamba; *"…. Serikali itaendelea kuimarisha taratibu za kukusanya mapato pamoja na kupunguza misamaha ya kodi. Sera za mapato zitakazozingatiwa kwenye Bajeti ya 2012/13 ni pamoja na; (iv) kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo…"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasema twende mbele zaidi ya maneno hayo; Kamati hairidhishwi na kasi hii ndogo ya Serikali katika kulishughulikia suala hili la misamaha ya kodi. Kamati inashauri Serikali kuonesha dhamira ya kweli kufanikisha suala hili, hivyo inaitaka Serikali ianze kulishughulikia suala hili mara moja la misamaha ya kodi na itoe *progress report* mbele ya Kamati mwezi Januari 2013. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa *D by D* ni mzuri lakini bado haujaweza kusimamia na kuimarisha ipasavyo ufuatiliaji na udhibiti wa matumizi ya fedha katika Halmashauri nyingi. Karibu asilimia 70 ya Bajeti ya Maendeleo na *OC* inaelekezwa kwenye Halmashauri za Wilaya. Utafiti unaonesha kuwa matumizi ya fedha hizi yamefunguliwa akaunti mbalimbali ambazo udhibiti wake unakuwa hauna tija. Bado Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inasimamia ipasavyo upunguzaji wa akaunti hizi ili kupunguza mwanya mkubwa wa upotevu wa fedha za Taifa na mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuelewa kuwa utaratibu wa sasa wa *D by D* unaishia juu tu kwenye Makao Makuu ya Halmashauri, kwa maana ngazi ya Wilaya. Bado ngazi

za Kata na Vijiji hazijaelewa vyema utaratibu huu na hivyo kuondoa kabisa dhana ya mipango shirikishi ya miradi na matumizi ya fedha. Tatizo hili linajenga hisia za matumizi mabaya ya fedha za Serikali pamoja na kuondoa dhana nzima ya uwajibikaji. Wizara ya Fedha iangalie utaratibu wa kujenga uwezo wa mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuhusisha ngazi ya Kata na Kijiji katika kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Fedha, Deni la Taifa katika kipindi kilichoishia Machi 2012 limeongezeka na kufikia shilingi bilioni 20,276.6 kutoka shilingi bilioni 17,578.9 kwa kipindi kilichoishia Machi 2011. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Kati ya deni hilo la nje ni shilingi bilioni 15,306.9 na shilingi bilioni 4,969.7 ni deni la ndani.

Kamati inatambua kwamba, kutokana na mahitaji makubwa ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikilinganishwa na mapato ya ndani, Serikali imekuwa ikikopa na itaendelea kukopa kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo na hivyo kusababisha Deni la Taifa kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi Duniani tena kubwa na tajiri kama USA, Japani, Uingereza na kadhalika, huwa zinakopa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo la Kamati ni kwamba, wakati Deni la Taifa linaongezeka katika kipindi husika kwa asilimia 15.4, Uchumi wa nchi yetu (*GDP Growth Rate)* tangu 2008/2009 hadi 2011/2012 umeongezeka kwa wastani wa asilimia 6.5 tu. Hii ina maana kwamba, upo uwezekano mkubwa wa Deni hilo kutokuwa himilivu iwapo Deni la Taifa halitaendana na Ukuaji wa Uchumi kwa kiwango cha juu zaidi kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kutekeleza kwa dhati Mpango wa Maendeleo wa Taifa ili malengo ya ukuaji uchumi wa nchi yetu yafikiwe na hivyo kujenga uwezo wa kulipa madeni yote ya ndani na nje. Aidha, ipo haja kwa Serikali ya kuchukua uamuzi wa makusudi ili kupunguza mikopo ya kibajeti na kuendelea kupanua wigo wa makusanyo katika maeneo mbalimbali na kurasimisha sekta isiyo rasmi**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, kwa kuwa uhimilivu wa Deni la Taifa unategemea sana masharti ya mikopo na matumizi ya fedha zinazokopwa, Serikali ihakikishe inakopa mikopo ya masharti nafuu na mikopo hiyo inaelekezwa kwenye Miradi ya Maendeleo tu hasa kwenye miundombinu ya kiuchumi na sekta zenye uwezo wa kuzalisha ajira nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nianze na hayo kwa sababu ya muda, niseme kidogo kwenye sekta zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inakadiriwa kuwa na idadi ya watu takriban milioni 40, wengi wao wanaishi vijijini. Takwimu zinaonesha kuwa, idadi ya watu inaongezeka kwa kasi ya asilimia 2.9 - 3.0. Ni dhahiri asilimia hii ya watu wengi wakiwa ni vijana, haijatumika ipasavyo kuhakikisha inasaidia uzalishaji na kuongeza uchumi wa nchi. Bado ajira inayotolewa na sekta rasmi haijaweza kukidhi idadi ya wanafunzi wanaomaliza katika elimu ya juu wanaofikia takriban 700,000 na wanaoajiriwa ni 40,000 tu kwa mwaka. Kamati inashauri Serikali ijiandae vyema kuhakikisha ajira za vijana zinapatikana kwa wingi hasa kwa kupitia mipango ya uwezeshaji ikiambatana na elimu ya ujasiriamali na kuboresha huduma za kifedha. Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi iwekeze kwenye sekta zinazozalisha zaidi kama kilimo na viwanda ili kuwajengea vijana ajira zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kuwa Serikali itafanya kila kitu katika ukuaji wa uchumi siyo sahihi; ni vyema kila Mtanzania akajitambua na kujua ana jukumu gani katika kuisaidia Serikali na kutimiza wajibu wake ipasavyo. Uchumi wa nchi huanzia kwa mtu mmoja mmoja, hivyo, mitazamo ya kitabia lazima ibadilike ili tuweze kusaidia kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba mnamo mwaka 2008, Kamati ya Uongozi iliridhia ushauri uliotolewa wakati huo wa kuweka utaratibu unaowezesha Muswada wa Sheria ya Fedha kujadiliwa na kupitishwa na Bunge mara tu baada ya Bajeti ya Serikali kuidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni ya 106 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada wa Sheria ya Fedha unatakiwa kujadiliwa na kupitishwa na Bunge baada ya Muswada wa Sheria ya Matumizi *(Appropriation Act)* kuidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilielezwa kwamba, madhumuni ya ushauri huo ilikuwa kuiwezesha Serikali kuanza kutoza na kukusanya mapato ya kodi mapema ili kuiwezesha Serikali kuanza kutekeleza mapema majukumu muhimu hasa ya maendeleo kwa wananchi; kwa kuwa mjadala kuhusu Bajeti ya Serikali kila mwaka hufanyika katika kipindi cha mwezi Juni hadi Agosti wakati Sheria ya Fedha *(Finance Act)* hupitishwa na Bunge mwishoni mwa shughuli zake mnamo mwezi Agosti kama Kanuni ya 106 inavyotamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa ushauri huo ulitolewa kwa nia njema, Kamati inaamini kuwa ushauri huo ulipokelewa na kuanza kutekelezwa bila ya kuzingatia ukweli kwamba Sheria ya *The Provisional Collection of Taxes Act, 1963* inaipa Serikali kupitia Waziri wa Fedha, mamlaka ya kuanza kutoza na kukusanya ushuru na kodi mbalimbali zinazokusudiwa kutozwa na Serikali katika mwaka husika wa fedha ambazo huwa zinatamkwa na Waziri wa Fedha kwenye Hotuba ya Bajeti ya Serikali kila mwaka. Lengo la sheria hiyo ni kuhalalisha katika kipindi cha mpito, utozaji na ukusanyaji wa kodi hadi hapo Bunge litakapojadili na kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha *(Finance Bill)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha mwishoni mwa shughuli za Bunge la Bajeti, yanatoa fursa kwa Bunge kutafakari kwa kina na kwa utulivu, hatua mbalimbali za kodi *(tax measures)* zinazopendekezwa na Serikali na hivyo kutoa ushauri wake kwa Serikali kwa madhumuni ya kuyakubali au kuyafanyia mabadiliko mapendekezo yaliyoletwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ulioanza kutumika tangu mwaka 2008 wa kuwahisha uwasilishaji Bungeni wa Muswada wa Sheria ya Fedha, haulipi Bunge lako Tukufu muda wa kutosha wa kuchambua mapendekezo ya Serikali yanayohusu kodi na wala hautoi fursa ya kutosha kwa Kamati ya Fedha na Uchumi ya kuwasikiliza wadau na kisha kuujadili na badaye kuwasilisha taarifa yake Bungeni.

Hivyo, Kamati inapendekeza utaratibu uliokuwa unatumika kabla ya mwaka 2008 na ambao ndiyo tafsiri sahihi, uliowekwa kwa mujibu wa Kanuni ya 105 na ya 106 ya Kanuni za Kudumu za Bunge uzingatiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa katika kujadili na kupitia Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013. Naomba nitumie fursa hii, kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustas Osler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amina Amour Abdulla, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Alhaji Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Subira K. Mgalu na mimi mwenyewe Mwenyekiti wa Kamati hii, Mtemi Andrew John Chenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dunstan Kitandula - Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa kunisaidia kuiongoza Kamati; Mheshimiwa Dkt.

William Mgimwa - Waziri wa Fedha na Manaibu wake; Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum; na Mheshimiwa Stephen Masato Wassira - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu). Aidha, naomba niwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara, Benki Kuu, Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, kwa kwa kuandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/13 na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu, ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Kadebe, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha lakini niseme moja kwamba, kama bei ya pamba mwaka huu haitafika shilingi elfu moja kwa kilo moja, *no cotton.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kama ilivyotolewa na mtoa hoja. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti, kwa kuwasilisha maoni ya Kamati yako ambayo imefanya kazi kubwa ya kuchambua mapendekezo haya ya bajeti kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na makofi hayo kwa Mheshimiwa Mtemi Chenge, kama alivyojitambulisha hapa leo kwa mara ya kwanza, naomba niwataje wachangiaji ambao wataanza kuchangia wakati nikimwandaa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu mapendekezo haya ya bajeti ili waweze kujiandaa. Tutaangalia muda utakavyoruhusu, tutaanza na Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuata Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Sara Msafiri; orodha ni ndefu nadhani mkitoka hapa mtaipata kwenye mbao zetu za matangazo na tutaendelea kujipanga kwa kadiri tutakavyoona. Tunatakiwa kuendesha vizuri kikao hiki cha majadiliano ya bajeti na tutapeana ushirikiano wa kutosha.

Baada ya kusema hayo, naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani aje asome mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Mpango huu wa Bajeti kwa mwaka 2012/2013.

**MHE. CHRISTINA LISSU MUGHWAI - NAIBU MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Kambi ya Upinzani imegawanyika katika sehemu mbili, ambapo mimi nitawasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Msemaji Mkuu wa Kambi katika Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Zitto Kabwe, atawasilisha Hotuba Mbadala ya Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 96(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2011/2012 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/13 kama ulivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwa hapa siku hii ya leo. Kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa, wapenzi na Viongozi wote wa CHADEMA kwa msiba mkubwa wa kuondokewa na mmoja wa Waasisi wa Chama chetu, Mzee Mohamed Ally Nyanga maarufu kama Bob Makani. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi na aipe familia ya marehemu moyo wa subira na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za pekee ziwaendee Viongozi wote wa CHADEMA, Wanachama na Wafuasi wote wa Chama, kwa kazi kubwa na yenye mafanikio makubwa, wanayoendelea kuifanya katika kukiimarisha na kukijenga chama nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mpango wowote ufanikiwe katika malengo yaliyokusudiwa ni lazima kuwe na dhamira ya dhati ya kuutekeleza. Kambi ya Upinzani imebaini kwamba, Serikali haina dhamira ya dhati ya kuutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa kushindwa kutenga fedha za kutosha kugharamia Miradi ya Maendeleo kama ilivyoainishwa katika Mpango. Rejea Mpango wa Maendeleo 2012/13 na Bajeti ya Serikali kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za Serikali zinaonesha kuwa, mwaka 2011 Pato halisi la Taifa lilishuka kwa kiwango cha asilimia 0.6 ikilinganishwa na mwaka 2010. Kwa maana kwamba, 2011 ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 6.4 na mwaka 2010 ulikuwa ni asilimia 7.0. Sekta ndogo ya Mawasiliano ndiyo iliyoongoza kwa ukuaji wa asilimia 19.0, Sekta ya Uzalishaji Viwandani asilimia 7.8, Sekta ya Kilimo ilipungua kutoka asilimia 4.2 mwaka 2010 hadi asilimia 3.9 mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura ya Kwanza ya Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa Katika mwaka 2011 inakiri kwamba, kulikuwa na ukuaji mdogo wa Pato la Taifa. Hata hivyo, Serikali inamlaumu Mwenyezi Mungu, kwa kusababisha ukuaji huo usioridhisha wa Pato la Taifa. Kiwango kidogo cha ukuaji kilitokana na hali mbaya ya ukame iliyojitokeza katika sehemu mbalimbali nchini ambapo imeathiri Sekta ya Kilimo. Hata hivyo, katika hali inayohitaji maelezo zaidi kutoka Serikalini, Serikali inadai katika aya ya 234 ya Kitabu hicho hicho kwamba, mwaka 2011, uzalishaji wa mazao ya chakula hususan ngano, mihogo, maharage, ndizi na viazi, uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2010 kutokana na hali nzuri ya hewa na mtawanyiko mzuri wa mvua kwa ustawi wa mazao. Mkanganyiko huu ni dalili ya ukosefu wa umakini katika kuandaa taarifa muhimu za Serikali na unaitia Serikali hii aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa mwaka 2010, Serikali imeendelea kukiri kuwa ukuaji huu wa Pato la Taifa haukupunguza umaskini kama ilivyotarajiwa kwa sababu sekta zilizokua haraka hazitoi ajira kwa wananchi wengi hasa waliopo vijijini ambao wanategemea kilimo. Ni lini sasa Serikali itaweka bayana mikakati inayotekelezeka itakayowafanya wananchi walio wengi wanufaike na ukuaji huo wa uchumi? Waziri Kivuli wa Fedha atakaposoma Bajeti Mbadala ataweka bayana mikakati itakayotekelezeka ya ukuaji wa uchumi kwa wananchi walio wengi na hasa wa kipato cha chini waishio vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa kasi kwa bei za bidhaa na huduma kuliathiri sana Bajeti ya Serikali ya mwaka unaokwisha. Wakati mfumko wa bei mwezi Julai mwaka wa Fedha 2011/2012 ulikuwa asilimia 13, ulifikia asilimia 19.2 mwezi Novemba mwaka huo wa Fedha. Hii maana yake ni kwamba, Bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge mwezi Juni 2011, ilipunguza uwezo wake wa kununua bidhaa na huduma kwa takriban asilimia sita. Hii ni sawa na shilingi 780 bilioni kuyeyuka katika Bajeti katika kipindi cha miezi minne tu ya utekelezaji wake. Aidha, kufikia mwezi Desemba 2011, mfumko wa bei ulifikia asilimia 19.8 na mfumko wa bei za chakula ulipanda hadi asilimia 25.6 kutoka asilimia 6.3 Desemba 2010. Kutokana na kasi hiyo ya ukuaji wa mfumko wa bei ni dhahiri kwamba, sehemu kubwa ya Bajeti na hasa Bajeti ya Maendeleo ilishindwa kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya zaidi kwa wananchi kwani mfumko wa bei za vyakula umekua kwa kasi kubwa mno. Ofisi ya Takwimu imeonesha kuwa, wakati mfumko wa bei za vyakula ulikuwa asilimia 14.8 mwezi Julai, umefikia asilimia 24.7 mwezi Novemba 2011. Ukilinganisha na bei za vyakula, mwaka 2010, mwananchi amepoteza uwezo wa kununua chakula kwa zaidi ya robo kati ya Novemba 2010 na Novemba 2011. Jumla ya vyakula ambavyo mwananchi alinunua kwa shilingi 10,000 mwaka 2010, sasa atanunua kiwango kile kile kwa shilingi 12,500. (*Makofi*)

Bei za vyakula zimeongezeka kwa kiwango hiki wakati kipato cha mwananchi kipo palepale. Mwathirika mkubwa wa mfumko wa bei ni mwananchi wa kawaida na mwenye kipato cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa undani utakuta mfumko wa bei wa bidhaa kama mchele, sukari, nyama na samaki, umekua maradufu. Bei ya mchele imekua kwa asilimia 50, sukari

asilimia 50, nyama asilimia 30 na samaki kwa takriban asilimia 40. Bidhaa hizi zote ni muhimu sana kwa mahitaji ya chakula kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa Serikali hadi muda huu imeshindwa kutoa suluhisho la mfumko wa bei ambao kwa kiasi kikubwa unachangiwa na bei za vyakula. Serikali imeendelea kutoa sababu za bei kupanda bila kutoa majawabu. Wananchi wamechoka kusikia sababu za mfumko wa bei, wanachotaka kuona ni hatua mwafaka zinachukuliwa kudhibiti mfumko huu wa bei na hivyo kupunguza ukali wa maisha kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba Mbadala ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, kwa mujibu wa *Hansard* za Bunge, tulipendekeza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za mafuta ya dizeli kwa Makao Makuu ya Mikoa kwa tarehe 16 - 31 Mei 2008 ilikuwa kama ifuatavyo; Dar es Salaam 1,654.09 *petrol* na 1,884.89 kwa dizeli kwa lita huku mafuta ya taa yakiwa 1,488.24 kwa lita; Kagera 1,748.93 *petrol* na 1,979.73 kwa dizeli kwa lita huku mafuta ya taa yakiwa 1,583.08 kwa lita; Kigoma 1,930 *petrol* na 2,080 dizeli kwa lita huku mafuta ya taa 1,550 kwa lita; Mkoa wa Mbeya 1,850 *petrol* na 2,000 dizeli kwa lita huku mafuta ya taa 1,500 kwa lita; na Zanzibar diseli ni wastani wa shilingi 1,850. Kati ya wastani wa bei ya 1800/= kwa lita, hizi ni bei za mijini, vijijini ambako kuna umaskini uliokithiri na mahitaji ya nishati kwa ajili ya usafiri, kilimo na kadhalika, wastani wa bei ni shilingi 2,200 kwa lita.

Hivyo hivyo kwa bei za bidhaa nyingine kama *cement,* mabati na kadhalika. Je, umaskini utapungua wakati sehemu kubwa ya jamii inaishi vijijini? Nchi kama India bei za vijijini na mijini ni tofauti na ndiyo maana wamemudu kuzalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi maeneo ya vijijini na vipato vyao ni vidogo. Haiingii akilini kuwa bei za bidhaa na huduma za vijijini ni kubwa kuliko za mijini kama kweli kuna nia ya kuwakwamua wananchi walio wengi wa vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunazidi kusisitiza ushauri tulioutoa kipindi hicho kuwa ufanyiwe kazi, kwani asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi maeneo ya vijijini na vipato vyao ni vidogo. Lazima sasa Serikali ipange bei maalum za nishati kwa maeneo ya vijijini ili kuongeza uzalishaji na kuwapunguzia gharama za maisha. Tuige mfumo huu kutoka nchi ya India ambao ulifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya Shilingi ya Tanzania imeendelea kushuka ukilinganisha na fedha za kigeni na hii inatokana na kukosekana kwa mikakati thabiti ya kuhakikisha kuwa shilingi inaimarika kwenye soko na hasa kutokana na sera mbovu za kiuchumi na usimamizi usio makini. Kushuka kwa thamani ya Shilingi licha ya kupanda kwa mauzo yetu nje kwa sekta zote mbili tunazotegemea sana (Madini na Utalii), kunaacha maswali mengi kuhusiana na chaguo letu kuhusu hifadhi ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaunga mkono ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwamba, sasa Benki Kuu ya Tanzania ianze kutunza sehemu ya Hifadhi ya Nchi katika Dhahabu. Benki Kuu inunue dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo na pia tuangalie uwezekano wa kutoza sehemu ya mrabaha katika Sekta ya Madini kama dhahabu safi *(pure gold).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika hotuba yake inasema kuwa, kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, ilipokea misaada na mikopo toka nje ya asilimia 85 ya makadirio ya shilingi bilioni 869.4 kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaelewa kabisa umuhimu wa fedha hizo toka nje, lakini ni kweli fedha hizo zinatumika kuleta maendeleo kwa wananchi? Fedha hizo zilikopwa kwa miradi gani hasa ya maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo yote ambayo Kambi ya Upinzani itayapa msukumo katika Hotuba ya Bajeti yake Mbadala ni mambo ambayo kwa kiasi kwa kikubwa, utatuzi wake ni lazima uhusishe mtazamo mpana wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Taifa linaonekana kuongezeka kwa kasi ya ajabu sana na hivyo kupelekea Taifa kuwa na mzigo mkubwa sana wa madeni. Kwa mujibu wa Hotuba ya Bajeti ya Mipango iliyowasilishwa Bungeni Tarehe 14 Juni, 2012, ukurasa wa 12, aya ya 25, inaonesha kuwa Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 15.4 kati ya Machi 2011 hadi Machi 2012 kutoka shilingi trilioni 17.6 hadi shilingi Trilioni 20.3. Cha kushangaza ni kwamba, Serikali inatuambia kuwa deni hilo linahimilika ilhali wananchi ambao ndiyo walipaji wa deni hilo wako hohehahe kimaisha. Aidha, hoja kwamba deni hili linahimilika inatia shaka kwa vile deni letu la nje halijawahi kupungua katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, tulipendekeza ufanyike uchunguzi maalumu kwenye Deni la Taifa ili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atuambie madeni haya tunayokopa kwa kasi ya namna hii tunayapeleka kweye miradi gani (matumizi ya madeni) na namna gani tunaweza kudhibiti Deni la Taifa. Mwaka huu pia tunarejea ushauri huo huo kwani mwenendo wa kukopa unatakiwa ujulikane na uwekewe uangalizi maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta za Kiuchumi na Kijamii ndiyo kioo cha kutolea tathmini ni jinsi gani utendaji wa Serikali kwa kipindi kilichopita ulivyofanikiwa au ulivyoshindwa. Maoni ya Kambi ya Upinzani katika hili ni kwamba, Serikali imeshindwa vibaya kuwaonesha wananchi kuwa ipo na inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji Serikali kushindwa kutoa fedha kwa Wizara za Kisekta kama ambavyo zilikuwa zimetengwa na Bunge hili ili kufanya kazi. Kwa masikitiko makubwa, fedha hizo zilishindwa kupelekwa zote na hivyo kusababisha miradi na huduma za jamii kutokutekelezwa. Hili limejidhihirisha kwa Kamati sita za Kudumu za Bunge kukataa kupitisha Bajeti za Kisekta kwa kutaka maelezo ya utekelezaji wa bajeti iliyopita. Madai ya Kamati yalikuwa ni kwa nini miradi haikutelezwa na pia ni kwa nini fedha zinazoombwa ni kidogo kuweza kutekeleza miradi na huduma katika sekta hizo kabla ya kupitisha bajeti hii mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012, Sekta ya Miundombinu ilitengewa jumla ya asilimia 20.6 ya jumla ya bajeti ya shilingi trilioni 13.5 na Watanzania wote watakuwa mashahidi; je, Reli ya Kati imekarabatiwa pamoja na injini zake na mabehewa kama tulivyoambiwa katika mwaka wa fedha unaoisha? Huku ni kulidanganya Bunge na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo zaidi kuonesha jinsi gani Serikali imeshindwa kutekeleza bajeti iliyopita, yatatolewa na Wasemaji Wakuu katika Sekta mbalimbali za Uchumi na Kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2011, Serikali inasema iliendelea na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia Mifuko ya Uwezeshaji na ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 7.1. Kambi ya Upinzani inauliza uwezeshwaji huu unafanywa kwa kutumia kigezo gani? Kutokana na utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umaskini *(REPOA),* kuhusu upeo wa elimu kwa wananchi wanaoishi vijijini ambao wanajihusisha na ujasiriamali, asilimia 16.2 hawana elimu ya shuleni bali elimu isiyo rasmi, asilimia 69.5 wana elimu ya msingi na asilimia 14.3 wana elimu ya sekondari au elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza kwa viwango hivyo vya elimu; je, uwezeshaji wa kutoa fedha bila ya kutoa mafunzo ya biashara unaweza kuleta tija? Hii ni kutokana na ukweli kwamba, idadi kubwa ya Watanzania wanaishi vijijini; hivyo, uwezeshaji kiuchumi wa namna yoyote ile ni lazima uangalie hali halisi kwa wananchi waishio vijijini. Bila mkakati wa kutoa elimu, Kambi ya Upinzani inahesabu kuwa haya ni matumizi ambayo hayakufanyiwa tafiti na hivyo ni upotevu wa fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuangalia Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati, naomba kunukuu ukurasa wa 92, kifungu cha 4.3.1, katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Toleo la Kiswahili kama ambavyo ulipitishwa na kuwekewa Azimio na Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo: *"Kwa kuelewa kuwa wakati wote kutakuwa na miradi ya uwekezaji nje ya Mpango, Serikali kuanzia sasa, itakuwa inatenga asilimia 35 ya makadirio ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kugharamia bajeti ya maendeleo kila mwaka."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana rahisi, kulingana na nukuu hiyo ni dhahiri kuwa Serikali haina fedha, kwani makusanyo yote ya mapato ya ndani ni shilingi trilioni 9.08 wakati Matumizi ya Kawaida ni shilingi trilioni 10.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeainisha Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati ambayo italeta maendeleo ya haraka hususan katika kuchochea maendeleo ya maeneo mengine na hivyo kuongeza ajira, kukabiliana na matatizo ya kiuchumi yaliyopo sasa na pia kuongeza Pato la Taifa. Ukurasa wa 25, aya ya 57, katika Hotuba ya Serikali, Taarifa ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013, inaeleza Miradi husika. Aidha, ukiangalia Hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2012/2013, ukurasa wa 46, aya ya 78(a)(i) inasema, Benki ya Exim China itatoa mkopo wa Dola za Marekani 1,225.3 utakaosimamiwa na *TPDC.* Cha kushangaza ni kuwa, kwenye Kitabu cha Miradi ya Maendeleo, fedha hizo hazionekani japokuwa *TPDC* ni Taasisi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni udhaifu mkubwa katika mfumo wetu wa bajeti, kwani unawafanya Wabunge wasijiridhishe ni nini wanapitisha. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba, Taasisi zote za Umma yakiwemo Mashirika, taarifa zao za mapato na matumizi kwa mwaka wa bajeti ziwekwe kama viambatanisho kwenye Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 78(a)(ii), katika kifungu kinachohusu usafirishaji na uchukuzi, Serikali imetenga kiasi cha shilingi trilioni 1.382.9 lakini kati ya fedha hizo, Fedha zinazohusiana na Reli ya Kati ni shilingi trilioni 134.16 tu na Wizara ya Uchukuzi imetengewa Fedha za Maendeleo shilingi bilioni 252.8. Fedha zote zinazobaki ni kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawo wa fedha kwa ajili ya kuwekeza katika Reli ya Kati ambayo ni mojawapo ya injini za uchumi zilikuwa hazitoshi na ndiyo sababu kuu kwa Waheshimiwa Wajumbe kushindwa kuipitisha Bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hadaa kubwa sana kwa Watanzania inayofanywa kwa makusudi na wale waliopewa dhamana ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma stahiki kulingana na kodi wanazolipa. Kitendo kilichofanywa na Waziri wa Uchukuzi, kuwaeleza wananchi akiwa katika Mkutano Jangwani kuwa Reli imepewa fedha za kutosha kununua injini za kisasa na kutandaza mataruma ya kisasa na kupanda treni kutoka Dar kuja Dodoma ni hadaa kubwa inayotuumiza sisi wote kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa miaka yote ya nyuma tumekuwa tukisisitiza umuhimu wa Reli ya Kati na tumetenga fedha za kutosha kwa Reli ya Kati katika Bajeti Mbadala kama itakavyosomwa na Msemaji Mkuu wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Miradi ya Kilimo kama ilivyoainishwa katika aya ya 60 ya Bajeti ya Hali ya Uchumi na Mpango, kwa kuoanisha na lengo la uwekezaji huo wa kuongeza ajira; Kambi ya Upinzani inaona kuwa uwekezaji huu utasaidia kujenga matabaka badala ya kuhamasisha vijana kuingia katika kilimo, watakuwa ni manamba katika mashamba hayo na mwisho umaskini utazidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuwa uwekezaji ufanywe kwa Serikali kuwawezesha wananchi kumiliki mashamba madogo madogo kwenye maeneo ya mabonde husika kwa kutengeneza miundombinu na kuikodisha kwa wamiliki wa mashamba hayo. Nchi nyingi zinazozalisha mpunga kwa wingi kama Vietnam hawatumii

mashamba makubwa bali ni mashamba madogo ili watu wengi wajihusishe na kilimo badala ya mtu mmoja tu na wengine kuwa vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), uliowasilishwa Bungeni mwezi Juni 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilihoji, pamoja na mambo mengine, uwezo wa utekelezaji wa Mpango huo kama ulivyopitishwa na Bunge hili Tukufu. Kwa mfano, wakati Mpango unadai kwamba gharama zinazotarajiwa kwa utekelezaji wake ni takriban shilingi trilioni 8.6 kwa mwaka au shilingi trilioni 42.98 kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango, katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wake, Serikali ilitenga shilingi trilioni 4.9 tu. Katika kujaribu kuhalalisha mgawo huo pungufu, Serikali ilijitetea kwamba mwaka 2011/2012 ulikuwa ni mwaka wa mpito wa utekelezaji wa Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa mwaka huu wa fedha, zinathibitisha kwamba, kauli ya Serikali kwamba mwaka 2011/2012 ulikuwa mwaka wa mpito kwa utekelezaji wa Mpango ilikuwa na lengo la kuwahadaa Watanzania. Hii ni kwa sababu, shilingi trilioni 4.5 zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013 siyo tu ni pungufu ya gharama tarajiwa ya shilingi trilioni 8.6 za kutekeleza Mpango kwa mwaka, bali pia ni pungufu ya fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo kwa mwaka ulioitwa wa mpito. Ni wazi kama Serikali yenyewe ilivyosema kuwa, Mpango huu ni kipimo cha ufanisi wa Serikali na uchumi kwa ujumla kwamba, Serikali hii ya CCM haijawa na ufanisi wowote katika utekelezaji wake wa Mpango na katika uendeshaji wake wa uchumi kwa ujumla! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa siyo tu katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa ujumla, bali pia imeshindwa kutekeleza ahadi yake yenyewe kwa Bunge hili Tukufu. Kwa mujibu wa Mpango, Serikali kuanzia sasa itakuwa inatenga angalau asilimia 35 ya makadirio ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kugharamia bajeti ya maendeleo kila mwaka. Kauli hii ya Serikali ilitiliwa nguvu na Azimio la Bunge hili Tukufu la tarehe 8 Juni 2011. Hata hivyo, Serikali ilianza mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango kwa kushindwa kutekeleza ahadi kwani ilitenga shilingi trilioni 1.87 au asilimia 26.2 ya mapato yote ya ndani yaliyokadiriwa kuwa shilingi trilioni 7.13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadithi ya mwaka huu ni mbaya zaidi kuliko ya mwaka jana. Hii ni kwa sababu, kati ya takriban shilingi trilioni tisa ambazo ni makadirio ya mapato ya ndani kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013, Serikali imetenga shilingi trilioni 2.2 au asilimia 24.4 ya mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Hii ina maana kwamba, badala ya Serikali kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Mpango ikilinganishwa na ulioitwa mwaka wa mpito, Serikali hii ya CCM imepunguza ufanisi ikilinganishwa na makadirio ya mwaka huo wa mpito licha ya kwamba makadirio hayo yalikuwa pungufu ya lengo la Mpango na kinyume cha Azimio la Bunge. Kwa ushahidi huu, ni wazi kwamba Serikali hii hii ya Chama hiki hiki, haina uwezo au nia ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano licha ya kuwa na nyuso tofauti katika safu za Serikali hiyo hapa Bungeni! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwamba, Bunge hili Tukufu lisimamie Azimio lake la tarehe 8 Juni mwaka jana kwa kukataa kuipitisha bajeti hii na kuitaka Serikali iongeze kiasi cha fedha za ndani zilizotengwa kwa bajeti ya maendeleo kufikia shilingi trilioni 3.15, ambayo ni asilimia 35 ya mapato yote ya ndani kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013. Kama bajeti yetu mbadala itakavyoonesha, inawezekana siyo tu kufikisha kiwango hiki bali pia kukizidisha endapo Serikali itakuwa makini katika ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, kama Serikali iliyopo madarakani inashindwa kusimamia Mpango wa Maendeleo ambao umezinduliwa kwa mbwembwe nyingi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupitishwa na Bunge hili Tukufu, ni wazi kuwa Serikali hiyo haipaswi kuendelea kuaminiwa na wananchi kwamba ina uwezo au nia ya kusimamia maendeleo yetu na uchumi wa Taifa letu. Serikali hii inapaswa kupumzishwa kwa manufaa ya nchi yetu ya sasa na ya vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti Mbadala ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ya mwaka jana ilipendekeza kupunguza misamaha ya kodi kufikia asilimia moja ya Pato la Taifa; kupunguza kodi na tozo kwenye mafuta ya petroli na dizeli ili kupunguza mfumko wa bei; kupunguza matumizi ya Serikali kwa kuondoa posho za vikao kwa Watumishi na Viongozi wote wa Umma; na kuelekeza fedha zaidi kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Kati ya mapendekezo hayo, Serikali ilitekeleza pendekezo la kuongeza fedha kwa Bodi ya Mikopo. Serikali ilipuuza au kushindwa kutekeleza mapendekezo mengine yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani ndiyo maana matatizo yanayowakabili wananchi yameendelea kuongezeka na hali yetu ya kiuchumi kwa ujumla imezidi kuwa mbaya kuliko kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, sambamba na kurejea mapendekezo yake ya mwaka jana, inapendekeza mambo yafuatayo:-

(i) Kuanzia sasa, misamaha yote ya kodi lazima iidhinishwe na Bunge hili Tukufu kupitia Kamati yake ya Fedha na Uchumi ili kuhakikisha kwamba haizidi asilimia moja ya Pato la Taifa;

(ii) Kuongeza bajeti ya maendeleo hadi kufikia asilimia 35 ya mapato ya ndani na kuelekeza nyongeza hiyo kwenye maendeleo vijijini hasa kujenga miundombinu kama vile barabara, nishati, maji safi, afya na elimu;

(iii) Kuelekeza fedha za kutosha kukarabati Reli ya Kati na kufufua njia za Reli za Tanga, Moshi na Arusha kwani usafiri wa reli ni nguzo muhimu kuinua uchumi wa nchi;

(iv) Kuongeza wigo wa kutoza tozo ya ujuzi *(Skills Development Levy)* ili waajiri wote ikiwemo Serikali na mashirika ya umma walipe tozo hiyo tofauti na sasa ambapo Sekta Binafsi tu ndiyo inayochangia. Aidha, tunapendekeza tozo hii ipunguzwe kutoka asilimia sita ya sasa mpaka kufikia asilimia nne ambapo theluthi moja itaenda *VETA* na Vyuo vya Ufundi na baki itaenda kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kukabili changamoto ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu;

(v) Kuongeza mapato ya ndani na kupunguza mikopo ya kibiashara kwa kuhakikisha mapato ya ndani yanafikia asilimia 20 ya Pato la Taifa kwa kufanya marekebisho ya kisheria na udhibiti ili kuiwezesha *TRA* kukusanya mapato zaidi kutoka kwenye kampuni za simu na kwenye shughuli za uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia.

(vi) Kuliandaa Taifa kuwa na uchumi wa gesi asilia kwa kuanzisha ama kuharakisha mchakato wa utungaji wa Muswada wa Sheria ya Gesi; na

(vii) Kupunguza au kufuta kodi kwenye bidhaa za vyakula vinavyotumiwa na wananchi walio wengi kwa muda maalum ili kushusha mfumko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo haya ni mawazo ya Wabunge walio wachache katika Bunge hili Tukufu. Katika utaratibu wa 'wengi wape' unaotumiwa na Bunge letu na katika mazingira ya ushindani wa kisiasa katika nchi yetu, ni rahisi kudharau au kupuuza ushauri wa walio wachache kwa kutumia nguvu ya uwingi ya Chama Tawala. Endapo hilo litafanyika kuhusiana na mapendekezo haya, Taifa letu litakuwa limekoseshwa fursa ya kuvuna utajiri na uzoefu wa kitaaluma wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na matokeo yake hayatakuwa mema kwa ustawi wa nchi yetu. Kama alivyosema Mahatma Gandhi: *"Mabadiliko ya kidemokrasia hayawezekani iwapo hatupo tayari kusikiliza upande mwingine. Tunafunga milango ya kufikiri wakati tunapokataa kuwasikiliza wapinzani wetu au baada ya kuwasikiliza tunawafanyia mzaha. Kutokuvumiliana kunapokuwa ndiyo mazoea, tunajiweka katika hatari ya kutokujua ukweli."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Nakushukuru Mheshimiwa Christina Lissu, kwa kuwasilisha maoni hayo.

Waheshimiwa Wabunge, mnaona Mheshimiwa Christina amechukua nusu saa, wamegawana na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kwa hiyo, tunampa sasa nafasi Mheshimiwa Zitto na yeye aje kutoa mapendekezo ya bajeti kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na atatumia nusu saa. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Serikali na hivyo kuwasilisha Bajeti Mbadala ambayo Kambi ya Upinzani kama ingekuwa Serikalini ndiyo ambayo ingeitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ninatoa Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Nchi ya Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 99(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga Mkaoni Iringa, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Vile vile nawapongeza Ndugu Saada Mkuya na Ndugu Janeth Mbene, kwa kuteuliwa kwao kuwa Wabunge na baadaye kuwa Naibu Mawaziri katika Wizara hii nyeti sana. Ninawapa pole pia maana Wizara ya Fedha siyo Wizara lelemama. Kambi ya Upinzani itaendelea kuisimamia Wizara hii kwa ukaribu sana kama ilivyofanya katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Mtakapofanya vizuri tutawapongeza ili mwongeze juhudi, mtakapoharibu tutawawajibisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, Mwaka wa Fedha uliopita ulikuwa mwaka mgumu sana kwa Watanzania. Ni mwaka ambao gharama za maisha zilipanda kwa kasi kubwa sana na juhudi za Serikali kuwakwamua wananchi na hasa wananchi wanyonge kutoka kwenye lindi la ufukara ziligonga mwamba. Kambi ya Upinzani inawapa pole Watanzania kwani hili ndilo walilochagua. Muhimu ni kuvumilia mpaka uchaguzi ujao na kufanya mabadiliko ya Serikali ili kuweka Serikali itakayoongozwa na CHADEMA na itakayoweza kukabili changamoto za sasa na za baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tufanye mapitio kidogo ya Bajeti inayomaliza muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa Bajeti Mbadala ya Kambi ya Upinzani ni vyema kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali iliyopita ili kuona ni kwa namna gani Serikali inathamini fedha za walipa kodi na dhamira yake ya kuleta maendeleo ya kiuchumi katika Taifa. Katika kufanya hivyo, tutapitia baadhi ya maeneo ambayo Kambi ya Upinzani tunaona kuwa hayakutekelezwa katika bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwaka 2011/12, Serikali ilitangaza nia yake ya kupunguza makali ya maisha. Hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwamo kupunguza kodi na tozo kwenye mafuta ya dizeli na petroli, kuanza kutekeleza mpango wa dharura wa umeme na kutoa fedha za kununua chakula kwa Wakala wa Chakula. Serikali ilitumia shilingi bilioni 296 na Dola za Marekani milioni 183 kwenye umeme. Vilevile Serikali ilitumia shilingi bilioni 27 kununua mahindi na kusambaza kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hatua hizo zilizochukuliwa, mfumko wa bei uliongezeka maradufu kutoka wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2010/11 mpaka wastani wa asilimia 17.8 mwaka 2011/12. Serikali imefeli katika lengo lake la kupunguza makali ya maisha kwa wananchi. Siyo tu kwamba, Serikali imeshindwa kudhibiti upandaji holela wa gharama za maisha bali pia hatua za Serikali zimeongeza kasi ya kupanda kwa makali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni katika Hotuba yake Mbadala ya mwaka 2011/12 iliitaka Serikali kushughulikia msingi wa mfumko wa bei hapa nchini ambao ni uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula. Tumeelezwa na Waziri Kivuli wa Mipango na Uchumi

kwamba, chakula peke yake ni asilimia 48 ya kapu la bidhaa na huduma ambazo mwanachi anatumia. Mfumko wa bei ya chakula kinacholiwa nyumbani na kwenye migahawa ilikuwa asilimia 25 mwezi Aprili 2012 *(BoT Monthly Economic Review, May 2012).* Vile vile mfumko wa bei wa nishati inayotumika nyumbani na mafuta ya dizeli na petroli ulifikia asilimia 25 pia mwezi Mei mwaka 2012. Ni dhahiri kwamba, iwapo tutadhibiti mfumko wa bei ya chakula, tutaweza kushusha mfumko wa bei kurudi kwenye tarakimu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza hatua zilezile ilizofanya mwaka wa fedha unaokwisha kwa kutoa vibali kwa Wafanyabiashara vya kuagiza mchele na sukari. Katika Hotuba yake Waziri wa Fedha anasema: "…Serikali ilitoa vibali vya kuagiza sukari bila kutoza ushuru wa forodha kiasi cha tani 200,000 ili kukabiliana na uhaba na kupanda kwa bei ya Sukari…"(ukurasa wa tisa, Ibara ya 15). Baada ya hatua hii, bei ya sukari ilipanda kutoka shilingi 1700 mpaka shilingi 2800 kwenye maeneo mengi nchini. Waziri wa Fedha katika hotuba yake anatoa suluhisho. Ninanukuu: "…Hatua za haraka ambazo Serikali itachukua ni pamoja na kutoa vibali vya uagizaji wa sukari na mchele kutoka nje…"! Serikali inachukua hatua zilezile kwa tatizo lilelile ikitegemea matokeo tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie; Serikali inachukua hatua zilezile kwa tatizo lile lile ikitegemea matokeo tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inarejea pendekezo lake la mwaka jana kwa Serikali kutoa vivutio kwa wakulima wadogo kuzalisha chakula kwa wingi. Miongoni mwa vivutio hivyo ni:-

(i) Kuwekeza kwenye barabara za vijijini ili mazao yao yafike kwenye masoko na kupata bei nzuri;

(ii) Kuwekeza kwenye usambazaji wa maji vijijini ili akina mama wasitembee mwendo mrefu kutafuta maji na hivyo kutumia muda mwingi kwenye uzalishaji;

(iii) Kuwekeza kwenye umeme vijijini ili wafanyabiashara wa vijijini waongeze thamani ya mazao. Kwa mfano, kuuza unga badala ya mahindi;

(iv) Kuwekeza kwenye miundombinu ya umwagiliaji vijijini ili wakulima wazalishe muda wote wa mwaka; na

(v) Kuwekeza kwenye elimu vijijini na pia afya vijijini ili wananchi wetu wawe na afya bora na waelimike katika mbinu za uzalishaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, hakuna mbadala wa kudhibiti mfumko wa bei zaidi ya kuongeza uzalishaji wa chakula na kuwekeza kwa wananchi wetu. Serikali inafikiria uzalishaji utaongezeka kwa kusaidia wakulima wakubwa ambao watageuza wananchi wetu kuwa manamba na vibarua ndani ya nchi yao. Tuwekeze kwa watu wetu vijijini ili waongeze uzalishaji na kwa kufanya hivyo mfumko wa bei ya chakula utakuwa historia. Hakuna mwarobaini wa kupanda kwa bei za vyakula isipokuwa kilimo.

Mhesimiwa Spika, tunatambua kuwa hatua tunazotaka Serikali ifanye ni za muda wa kati. Kwa muda mfupi tunataka Bodi ya Mazao Mchanganyiko, Wakala wa Hifadhi ya Chakula na Bodi ya Sukari, zipewe fedha kuagiza mchele na sukari na pia kununua kutoka kwa wakulima na kusagisha mahindi. Wafanyabiashara waagizaji wa chakula washindane na Taasisi hizi za Umma badala ya kuwapa vibali ambavyo hutolewa kwa rushwa na hivyo kuongeza bei za bidhaa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesema kwamba, ilichukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo la ajira kwa kuongeza fursa za ajira Kuwezesha Wananchi kiuchumi na kuongeza ajira. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuongeza mitaji katika Benki ya Rasilimali, Benki ya Wanawake, Benki ya Posta na Twiga Bancorp. Pia Serikali imetangaza kwamba,

imeajiri walimu, maafisa ugani na watumishi wa afya. Hatua kama hizi pia zimetangazwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/13 ambapo pia Serikali imetangaza kuajiri watumishi 71,756.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Duniani kote Serikali haizalishi ajira bali ajira huzalishwa na uchumi mzima ambapo Serikali ni sehemu tu ya uchumi *(jobs are created by an economy).* Takwimu zinaonesha kwamba, kila mwaka Tanzania inaingiza kwenye soko la ajira watu takriban laki saba. Shughuli za uchumi zikiongezeka ndiyo ajira zinatengenezwa. Serikali inafikiria nini kuhusu vijana takriban milioni nane walio shule za msingi hivi sasa, Vijana milioni 1.7 walio katika shule za sekondari hivi sasa, vijana 200,000 waliopo vyuo vya ufundi na wanachuo 180,000 walio katika vyuo vya elimu ya juu (takwimu kutoka Kitabu cha Hali ya Uchumi, 2012, Sura ya 19)? Serikali ambayo bado inategemea takwimu za ajira za mwaka 2006 inajitamba kwa kuajiri watu 70,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Serikali ni kujenga mazingira ya wananchi kupata ajira ama kwa kujiajiri au kwa kuajiriwa na shughuli za uchumi. Ukweli ni kwamba, Serikali imeshindwa kushughulikia tatizo la ajira na hasa ajira kwa vijana. Tatizo la ajira kwa vijana ni bomu litakalokuja kutulipukia vibaya sana kama hatutakuwa makini nalo. Hii ni nchi ya vijana, kutoshughulikia masuala yao ni kutoshughulikia masuala ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya ajira kwa vijana; Bajeti Mbadala imeiwekea mikakati mipana ya kiuchumi kwa kuanzisha miradi mikubwa ya umma itakayomeza vijana waliopo mtaani na kuanzisha kwa makusudi na kwa kasi vyuo vya ufundi stadi na vyuo vya ufundi na mafunzo vingi. Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza uwekezaji wa miundombinu vijijini kama njia ya kupunguza tatizo la ajira kwa vijana. Vilevile tunapendekeza Miradi mikubwa ya kuongeza mazao ya Kilimo hasa Pamba, Korosho na Katani ili kupanua ajira. Kambi ya Upinzani pia inapendekeza kujenga *VETA* katika kila Halmashauri ya Wilaya na Chuo cha Ufundi katika kila Mkoa ili kutoa ujuzi kwa vijana ili waweze kukabili maisha yao. Badala ya Serikali kukopa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, Serikali ikope kujenga vyuo vya ufundi stadi na vyuo vya ufundi na mafunzo. Lazima Viongozi siyo tu tuwe makini, bali tuonekane kuwa makini tunaposhughulikia suala la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni ilitangaza vipaumbele katika Sera ya Mapato ambavyo ni pamoja na kukusanya mapato ya Serikali mpaka zaidi ya asilimia 20 ya Pato la Taifa ili kuwezesha kujitegemea kupata fedha za Miradi ya Maendeleo. Pia Kambi ya Upinzani inakusudia kufanya marekebisho mbalimbali ya Sheria za Kodi ili kulinda viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi za kilimo na mifugo za hapa nchini, kupanua wigo wa mapato kwa kutunga sheria ya kulazimu kila Mtanzania kujaza fomu za marejesho ya kodi na kurekebisha viwango vya kodi ya mapato *(PAYE)*. Vile vile tunapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria za Kodi kwenye Sekta za Madini na Mawasiliano ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Serikali ilichukua hatua mbalimbali katika masuala ya kodi. Katika Bajeti Mbadala pia tulipendekeza hatua mbalimbali ambazo tuliona zitaongeza mapato ya Serikali na hivyo kutuwezesha kuendeleza nchi yetu. Baadhi ya hatua mbalimbali tulizopendekeza Serikali imetangaza kuzitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti Mbadala ya Mwaka 2011/12, ilipendekeza masuala yafutayo ili kuongeza mapato ya Serikali kuweza kukabiliana na ukwepaji wa kodi unaofanywa na makampuni makubwa ya kimataifa *(Multinational Corporations)* na hatimaye kulipunguzia Taifa mapato:-

(i) Kutunga sheria kwa kuimarisha zaidi Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 kwamba, mikopo ya makampuni kwenye uwekezaji, kwa sababu za kikodi, isizidi asilimia 70 ya mtaji wote uliowekezwa na hii ianze mara moja bila kujali mikataba iliyopo;

(ii) Kutunga sheria kuhakikisha kwamba riba kwenye mikopo kutoka makampuni yanayohusiana (*sister companies*) haitaondolewa kwenye kutoza kodi (*not tax deductible*); na

(iii) Kuhakikisha kwamba mauziano ya Kampuni yoyote ambayo mali zake zipo Tanzania yanatozwa kodi ya asilimia 30 kama ongezeko la mtaji (*capital gains*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendezo haya ni pendekezo moja tu ndilo limechukuliwa na Serikali katika Bajeti ya mwaka 2012/13 nalo ni *capital gains tax*. Hata hivyo, pendekezo la Serikali lina makosa makubwa sana ya kifundi. Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mgimwa amesema, ninanukuu: "Kuanzisha kodi itokanayo na uuzaji wa rasilimali ya uwekezaji (*capital gains tax*) kwenye uuzaji wa hisa za kampuni mama ya nje ya nchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma pendekezo letu kwa haraka utaona kama Serikali imelichukua lilivyo, lakini kwa jicho la kiuchumi pendekezo la Serikali na lile la Kambi ya Upinzani ni mambo tofauti sana. Pendekezo la Serikali linazungumzia hisa. Mamlaka ya Mapato Tanzania haitakuwa na mamlaka (*jurisdiction to tax*), kutoza kodi kwa kampuni mama (*as a source or even residence*). Mamlaka ya Mapato Tanzania ina mamlaka na mali (*assets*) zilizopo Tanzania za kampuni mama. Kwa mfano, wakati Kampuni ya Barrick inanunua Mgodi wa Bulyanhulu, haikuinunua Kampuni ya *Kahama Mining Ltd.* bali ilinunua hisa zote za Kampuni ya *Sutton Resources*. Vile vile, wakati *Zain* inanunua *Celtel,* haikununua *Celtel Tanzania Ltd.* bali *Celtel Africa BV* ambayo ilikuwa inamiliki *Celtel Tanzania BV* ambayo ilimiliki *Celtel Tanzania Ltd.* Hivyo hivyo ilikuwa kwa *Airtel* ilipoinunua *Zain.* Kukwepa mitego hii ya Mashirika ya Kimataifa *(MNCs)*, sheria itaje kwamba kodi hii itozwe kwa mali zilizopo Tanzania na siyo kwa hisa kama alivyopendekeza Waziri wa Fedha. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inatambua hatua hiyo ya Serikali kuchukua wazo hili ili kuongeza mapato ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Mwaka 2011/12, Serikali iliahidi kupunguza misamaha ya kodi mpaka kufikia asilimia moja ya Pato la Taifa. Ahadi hii haikutekelezwa na Serikali na badala yake imerejea kuahidi tena. Waziri wa Fedha ameliambia Bunge katika hotuba yake, nanukuu: "Kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo (ukurasa wa 39)". Badala ya Serikali kutuambia hivi sasa misamaha ya kodi imefikia asilimia ngapi, imeendelea kutoa ahadi isizoweza kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa ya Utafiti uliofanywa na Jopo la Taasisi za Dini hapa nchini, waliyoiita *The One Billion Dollar Question,* imeonekana kwamba Tanzania inapoteza takriban shilingi trilioni 1.7 kutokana na misamaha ya kodi, ukwepaji wa kodi, utoroshaji wa mitaji nje na udanganyifu katika biashara ya kimataifa. Fedha hizi ni zaidi ya jumla ya Bajeti za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Nishati na Madini. Fedha hizi ni zaidi ya mkopo ambao Serikali itadhamini kwa *TPDC* ili kujenga Bomba la Gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam. Fedha hizi zinazopotea kutokana na misamaha ya kodi ni zaidi ya gharama za ujenzi wa gati mpya katika Bandari ya Dar es Salaam. Kambi ya Upinzani inawapongeza Viongozi wa Dini kwa kufanya kazi hii nyeti sana, lakini tunampongeza zaidi Mtafiti Mtanzania, Dokta Prosper Ngowi, kwa kushiriki katika utafiti huu. Tunaishauri Serikali kwa kusoma Taarifa hii na kutekeleza mapendekezo yake ili kuongeza mapato ya Serikali. Lugha za kufanya mapitio kila mwaka hazisaidii, wananchi wanataka kuona misamaha ya kodi imepungua mpaka kiwango kinachostahili cha asilimia moja ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti Mbadala ya Mwaka 2011/12, ilipendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004. Tunarejea pendekezo letu na kuongeza pia kwamba, sehemu ya kodi ya mapato inayotoa fursa *(grandfathering)* kwa Kampuni za Madini kutumia Sheria ya Kodi ya Mapato iliyofutwa ya Mwaka 1973, ifutwe. Pendekezo letu lina lengo la kutaka kuweka mfumo wa *straightline method of depreciation* ya asilimia 20 badala ya sasa ambapo Kampuni za Madini hufanya *hundred percent depreciation* kwenye mitambo yao mwaka wa kwanza na hivyo kuchelewesha kulipa *Corporate Tax*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeamua kupandisha kiwango cha chini cha kipato ili kutoza kodi ya mapato *(PAYE)* kutoka shilingi 135,000 mpaka shilingi 170,000 bila kushusha kodi yenyewe. Hii haitamsaidia mwananchi hata kidogo kwani bado kiwango cha kodi cha asilimia 14 kipo juu sana. Vile vile kiwango cha chini cha pato litakalotozwa kodi kitawaathiri wafanyakazi wa Serikali maana ndiyo ambao Serikali ina mamlaka ya kutangaza kima cha chini cha mshahara wao na kuwaacha wafanyakazi wa Sekta Binafsi ambao wengi hulipwa kiwango kidogo sana cha mishahara. Kimsingi, kutokana na tangazo lake, Waziri wa Fedha ametangaza kima kipya cha chini cha mshahara kuwa kitakuwa shilingi 170,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarejea kauli yetu kwamba, kupanda kwa gharama za maisha kumepunguza uwezo wa matumizi ya wananchi walioajiriwa na kulipwa mishahara ambayo inakatwa kodi *(PAYE)*. Tunapendekeza kwamba, *PAYE* ianzie asilimia tisa kutoka asilimia 14 na kiwango cha chini cha kutoza kiwe shilingi 150,000. Tunatambua kuwa kodi hii ni chanzo kikubwa cha mapato kwa Serikali ambapo kwa mwaka huu wa fedha kinatarajiwa kuingiza takriban shilingi bilioni 1,437 (asilimia 18 ya mapato yote ya kodi yanayokusanywa na *TRA*) kutoka Idara ya Kodi za Ndani (Wafanyakazi wa Serikali shilingi 115bn, Wafanyakazi wa Mashirika ya Umma shilingi 47bn na Wafanyakazi wa Sekta Binafsi shilingi 312bn) na Idara ya Walipa kodi wakubwa (Wafanyakazi wa Serikali shilingi 450bn, Wafanyakazi wa Mashirika ya Umma shilingi 108bn na Wafanyakazi wa Sekta Binafsi shilingi 406bn). Hata hivyo, wananchi wanapobakia na pesa za matumizi, kodi nyingine kama *VAT* na Ushuru wa Bidhaa huongezeka na hivyo kupunguza kiwango cha mapato ya Serikali ambayo yangepotea kutokana na uamuzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado kuna haja ya kuangalia upya *tax brackets* na kuzirahisisha kwa kuzipunguza na kuongeza kiwango cha kodi ya mapato kwa watu wenye kipato kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza mapato kutoka kwa watu wenye kipato kikubwa, Kambi ya Upinzani inapendekeza mabadiliko katika viwango vya juu vya kodi ya mapato ambapo tunapendekeza kupandisha kiwango cha juu kabisa cha kukokotoa kodi ya mapato *(PAYE)* kiwe shilingi milioni kumi na kodi iwe asilimia 42 kutoka asilimia 30 ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza kwamba, mtu yeyote anayepata mapato ya zaidi ya shilingi 10,000,000 alipe kodi ya mapato ya shilingi 500,000 kujumlisha na asilimia 42 ya tofauti ya shilingi 10,000,000 na shilingi 3,200,000 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini. Lengo la mapendekezo haya ni kuwafanya watu wenye kipato kikubwa walipe kodi zaidi kulingana na kipato wanachopata, maana hivi sasa maskini wanalipa kodi nyingi zaidi kuliko wenye nacho.

Mapato ya kutozwa kodi kwa mwezi kwa mapato yanayozidi shilingi 720,000; Kodi *(PAYE)* ni Sh. 112,500 ongeza 30% ya kiasi kinachozidi sh. 720,000.

Mapendekezo ya mapato ya kutozwa kodi kwa mwezi kwa mapato yanayozidi shilingi 720,000 lakini hayazidi shilingi 3,199,199, kiwango kipya cha Kodi *(PAYE)* ni shilingi 112,500 ongeza 30% ya ziada ya shilingi 720,000.

Mapato yanayozidi shilingi 3,200,000 lakini hayazidi shilingi 9,999,999, kiwango kipya cha kodi *(PAYE)* shilingi 190,000 ongeza 38% ya ziada ya shilingi 3,200,000.

Mapato kuanzia shilingi 10,000,000 na kuendelea, kiwango kipya cha Kodi *(PAYE)* shilingi 500,000 ongeza 42% ya mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya hayatapunguza mapato ya Serikali, kwani wigo wa kodi utakuwa umeongezeka kwa kuwagusa wafanyakazi katika Sekta Binafsi na pia kupata kodi zaidi kutoka kwa watu wenye kipato kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kambi ya Upinzani inaendelea kupendekeza kuwa, mchakato uanze ili kila Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na zaidi awe anajaza fomu za kodi *(tax returns)* kila mwaka. Suala hili ni muhimu sana na litangazwe mwaka huu ili tuwe na mwaka mzima wa kujitayarisha ili lianze mwezi Julai mwaka 2013. Mtanzania yeyote, awe na kipato au asiwe na kipato, ajaze *Tax Returns*. Mfumo huu utatoa takwimu muhimu sana kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania na utasaidia sana hapo baadaye kupanua wigo wa mapato. Tunapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato ili mfumo huu uwepo kisheria ndani ya mwaka mmoja kuanzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuanzishwa kwa *Real Estate Regulatory Authority* kama tulivyofanya kwa mwaka uliopita na kwamba kila mwenye nyumba ya kupangisha lazima atambuliwe na kulipa kodi inavyostahili. Lengo ni kuhakikisha Sekta

ya Nyumba inatoa mapato ya kutosha kwa Serikali na kuzuia mianya ya ukwepaji kodi inayofanywa na wenye nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza mwaka 2011/12 kwamba, ushauri wa Mradi wa kuboresha mfumo wa kodi *(Tax Modernisation Project)* ambao ulishauri kwamba ipo haja ya kuainisha Kodi ya *VAT* na *Presumptive Tax*, utekelezwe. Tunashauri kuwa, kodi anayotozwa mfanyabiashara ndogondogo kabla hajaanza kufanya biashara ifutwe kabisa. Uamuzi huu utapunguza mapato ya Serikali (Shilingi bilioni 21.6 kwa mujibu wa Kitabu cha Bajeti, *Vol. I*), katika kipindi cha muda mfupi lakini itakuwa ni chanzo kikubwa sana cha mapato katika kipindi cha muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupitia vyanzo vya mwaka jana na kulinganisha na mapendekezo ya Serikali, Kambi ya Upinzani bado inapendekeza vyanzo vya ziada mwaka huu ili kuboresha mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunapenda kushukuru kuwa wazo letu la kutoza kodi ya *skills development levy* tuliyopendekeza katika hotuba yetu ya mwaka uliopita lilifanyiwa kazi na Serikali lakini kwa mwaka ujao wa fedha tunaitaka Serikali kuipitia upya kodi kwa kuongeza wigo wa wachangiaji ili kuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza kiwango cha tozo ya kuendeleza stadi *(skills development levy – SDL),* kishuke kutoka asilimia sita ya sasa mpaka asilimia nne. Tunapendekeza kuwa, waajiri wote walipe kodi hii ikiwemo Serikali na Mashirika ya Umma. Lengo ni kupunguza mzigo kwa waajiri na kuondoa ubaguzi kwani wanaofaidika na tozo hii (wanafunzi wa elimu ya juu) pia huajiriwa na Serikali na Mashirika ya Umma. Serikali ilipanga kukusanya shilingi 161bn kutoka katika tozo hii kwa mfumo wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ambayo Kambi ya Upinzani inayapendekeza, yataongeza mapato ya Serikali mpaka shilingi 320 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha katika tozo hii amesema, Serikali itapitia upya maudhui ya viwango vya tozo hii. Kambi ya Upinzani imetamka maudhui na viwango na tunaiomba Serikali itekeleze pendekezo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza mgawanyo wa tozo hii urekebishwe kwa kuongeza mapato yatakayokwenda kwenye vyuo vya ufundi mchundo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanafunzi wetu watasomeshwa na kodi hii, basi tuangalie upya mfumo wa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Fedha inayopatikana kwenye kodi hii itumike kusomesha kwa *grant* wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi darasani na kuwapunguzia mzigo wa mikopo. Vile vile tuangalie kama tunaweza kukopesha wanafunzi malazi na chakula tu na kutoa bure ada na mafunzo kwa vitendo na vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani mara kwa mara tumekuwa tukieleza jinsi wasanii wanavyoshindwa kunufaika na kazi zao kutokana na kukosekana mfumo rasmi wa Kiserikali unaozuia wizi wa kazi za wasanii. Pamoja na Serikali kukubali kuahidi kuwa na mfumo rasmi wa kuzuia wizi wa kazi hizo, haijaweka wazi mfumo rasmi utakaokuwa unatumika kuzuia wizi huo na hatimaye wasanii kunufaika na kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani katika hotuba ya Wizara ya Habari Vijana na Michezo kwa mwaka uliopita tulingumzia suala hili na tulishauri kwamba kuwe na utaratibu wa kuweka *stiker* maalumu zinazotolewa na mamlaka za serikali kuonyesha uhalali wa muuzaji wa kazi za wasanii. Serikali imetekeleza pendekezo letu. Hata hivyo, tuna maoni tofauti kuhusu namna ya kutekeleza pendekezo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, Serikali mwaka 2006 kupitia Gazeti la Serikali Na. 18 la tarehe 10 mwezi wa Februari, ilianzisha utaratibu wa *HAKIGRAM* kama *stiker* maalumu za kazi halali za wasanii zinazotolewa na *COSOTA*. Kambi ya Upinzani

tunapendekeza utaratibu huo uendelee na Mamlaka ya Mapato *(TRA),* ihusike kukusanya mapato kwa ajili ya kazi hiyo na *COSOTA* wataratibu utoaji wa *HAKIGRAM.* Hii itaenda sambasamba na kuzuia uchakachuaji wa *HAKIGRAM* hizo ili kutopoteza lengo la kuweka mfumo huo. *Stiker* zisitolewe na *TRA* bali zitolewe na *COSOTA* na *TRA* isimamie eneo la mapato tu. Hii itasaidia kwani *stiker* hizi hazitatumika kupata mapato pekee bali pia kuweka kumbukumbu muhimu za kazi za wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja na pendekezo la kuendelea kutoza ushuru wa bidhaa kwenye masuala ya huduma ya mawasiliano ya simu, jambo ambalo litamgusa mtumiaji wa huduma hiyo ambaye ni mwananchi wa kawaida na hivyo kuongeza gharama za simu. Kambi ya Upinzani inapinga kabisa kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye muda wa maongezi *(airtime)* kwenye simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya wananchi hapa ni kwamba, Kampuni za Simu za Mkononi hazilipi kodi ya kutosha na hasa kodi ya makampuni *(corporate tax)*. Waziri Mkuu alipokuwa anafunga Bunge la Bajeti mwaka 2011, alitangaza Kampuni ambazo ni walipa kodi wakubwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Katika orodha hiyo, kulikuwa na Kampuni moja tu ya Simu za Mkononi (Kampuni ya *AirTel*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wananchi wanataka kodi zaidi kutoka Kampuni za Simu, Serikali inapendekeza kuongeza kodi kwa mwananchi anayetumia simu. Kampuni zilipe kodi ya mapato na siyo kukandamiza wateja kwa ushuru wa bidhaa ilhali huduma zenyewe za simu hazina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wananchi wanalalamika kwamba, kampuni za simu za mkononi haziweki wazi mapato yake yote, hali iliyopelekea Kamati ya Bunge ya *POAC* kuiagiza *TCRA* kufunga mtambo utakaoweza kuijulisha *TCRA* mapato yote ambayo kampuni za simu zinapata. Serikali ya Ghana ilifanya hivi na kupandisha maradufu mapato yanayotokana na Sekta Ndogo ya Simu. Hivi sasa Ghana, nchi yenye watumiaji wa simu milioni 17 ukilinganisha na Tanzania yenye watumiaji 23 milioni, inakusanya asilimia kumi ya mapato ya Serikali kutoka kwenye kampuni za simu pekee.

Iwapo Tanzania ikifikia kiwango cha Ghana cha asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Serikali kutoka kwenye kampuni za simu, Tanzania itaweza kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 860 kutoka kwenye Sekta Ndogo ya Simu pekee. Hata hivyo, mazingira ya Ghana na Tanzania ni tofauti na hivyo tunapendekeza kiwango kutokana na hali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TCRA* kupitia zabuni nambari *AE-020/2010-11/C/04* imetangaza *request for expression of interest for design, development, installation and management of telecommunication monitoring system under build, operate and transfer* ili kupata chombo cha kufuatilia mapato ya Kampuni za Simu. Kwa mujibu wa ratiba zilizotangazwa na *TCRA,* chombo kitakuwa kimeanza kazi mwishoni mwaka huu wa 2012. Kwa dhati kabisa, napenda kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* na watumishi wote kwa kutekeleza maelekezo ya Kamati ya Bunge kwa haraka ili kuhakikisha mapato kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotushangaza ni kwamba, Waziri wa Fedha na Uchumi hakugusia kabisa suala hili muhimu sana kwa mapato ya Serikali, badala yake Serikali imekimbilia kukandamiza wanyonge watumiaji wa simu na kuyaacha Makampuni ya Simu yakilipa kiduchu kutoka kwenye mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi huu wa kufuatilia mapato ya Kampuni za Simu na Marekebisho tunayopendekeza ya kujenga uwezo zaidi wa *TCRA* kwa kuwa na Idara ya *Revenue Assurance* na kurekebisha Sheria ya *TCRA* kwa kuweka wazi makujumu ya *TRA* ndani ya *TCRA*, utaiingizia Serikali mapato ya takriban shilingi 660 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la Sekta ya Mawasiliano, ninaomba kurejea kuitaka Wizara ya Fedha itoe maelezo hapa Bungeni namna ambavyo hisa za Serikali katika Kampuni ya *MIC Tanzania Ltd.* inayomiliki Kampuni ya Tigo zilivyouzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikuwa inamiliki hisa asilimia 26 katika Kampuni hii. Kwa mujibu wa kumbukumbu nilizoziona, hisa hizi zote ziliuzwa kwa thamani ya dola laki saba kwa mwanahisa mwenza mnamo mwezi Februari mwaka 2004. Kampuni hii leo inapata mapato ya shilingi bilioni 20 kwa mwezi, tuliuza hisa zetu asilimia 26 kwa dola laki saba! Laki saba dola! Kambi ya Upinzani inataka uchunguzi maalumu katika mauzo haya na Taifa liambiwe nini kilitokea na hatua gani za kuchukua dhidi ya waliouza mali hii ya umma bila zabuni wala kuzingatia thamani ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia mauzo ya ngozi ghafi nje ya nchi. Kambi ya Upinzani imeshangazwa na hatua ya Serikali kuja na pendekezo la kuongeza ushuru kwenye bidhaa ya ngozi ghafi inayosafirishwa nje kutoka asilimia 40 hadi 90, lengo likiwa ni kuhamasisha usindikaji wa ngozi hiyo na kuiongezea thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi iliyo na mianya mingi ya rushwa kama Tanzania, hatua hii haitakuwa na tija kwa kuwa wafanyabiashara wengi wa ngozi ghafi wamekuwa na tabia ya kupunguza takwimu za kusafirisha ngozi ghafi na hivyo kupelekea Serikali kukosa mapato mengi sana. Serikali inafahamu kwamba, hata ushuru wa mauzo nje wa asilimia 40 haukuweza kutatua tatizo la viwanda vya ndani kukosa malighafi. Kambi ya Upinzani haikubaliani na pendekezo la Serikali kwani halitatatua tatizo la kukuza Sekta Ndogo ya Ngozi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuzuia kabisa kusafirisha ngozi ghafi kwenda nje na badala yake kuwe na mpango wa kutumia ngozi ghafi hapa nchini na kuleta tija katika uchumi wa Taifa kwa kutengeneza ajira na kuongeza thamani ya mauzo nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kuzuia ngozi ghafi kusafirishwa kwenda nje kwa Tanzania itakuwa siyo suala jipya kwa sababu Ethiopia imezuia na kuwekeza katika kiwanda cha viatu, mikanda na bidhaa za ngozi. Kutokana na Mpango wa Mendeleo ya Ethiopia *(GTP – Growth and Transformation Plan),* Sekta ya Ngozi itaingiza fedha za kigeni za thamani ya Dola za Kimarekani bilioni nne kwa mwaka. Hii ni sawa na fedha za kigeni ambazo Tanzania inapata kutoka kwenye Dhahabu na Utalii kwa pamoja. Ethiopia, nchi iliyokuwa inatembea na bakuli na kulia njaa leo inakuwa nchi ya kupigiwa mfano na sisi Watanzania! Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda pia amepiga marufuku kuuza ngozi ghafi nje. Hata nchi ya Pakistani ambayo ndiyo ngozi zetu zinakwenda, nayo imepiga marufuku mauzo ya ngozi ghafi nje. Serikali ipige marufuku mauzo ya ngozi ghafi nje ya nchi ili kulinda viwanda vya ngozi nchini, kuongeza ajira na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Maziwa hapa nchini inahitaji kuwekewa maazingira ya kukua ili izalishe ajira na mapato ya kodi kwa Serikali. Wakati Tanzania ndiyo nchi ya Afrika Mashariki inayoongoza kwa kuwa na ng'ombe wengi lakini inaongoza kwa kuagiza maziwa kutoka nje yenye thamani ya Dola za Kimarekani 3.6m. Wakati Kenya imelinda soko la maziwa na bidhaa za maziwa kwa kuondoa *(zero rating)* kodi ya *VAT* kwenye bidhaa za maziwa, Waziri wa Fedha hajaonesha kabisa juhudi zozote za kuijengea uwezo Sekta Ndogo ya Maziwa hapa nchini na hivyo kuweza kuondolewa kabisa katika ushindani na kujikuta wafugaji wanakosa kabisa soko la kuuza maziwa yao hapa nchini. Nchi za Rwanda na Uganda pia zimelinda maziwa na bidhaa za maziwa kwa njia hii. Ni muhimu Serikali kuwianisha kodi hii na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kufanya *zero rating* kwenye maziwa na bidhaa za maziwa zinazozalishwa hapa nchini kwa kipindi cha miaka mitano ili kufikisha uzalishaji wa angalau lita 500,000 za maziwa kwa siku kutoka lita 123,000 za sasa na kuweza kutoa ajira kwa Watanzania zaidi ya elfu tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zote za kuongeza mapato tulizopendekeza pamoja na hatua za Bajeti Mbadala iliyopita ambazo tunarudia kuzipendekeza, zitaongeza mapato ya Serikali kwa takriban shilingi bilioni 2,885 kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni nyongeza ya vyanzo vya mapato mbadala 2012/2013.

| Chanzo cha Mapato | Makisio - Bilioni |
|---|---|
| Marekebisho ya kodi za misitu ikiwemo Mkaa | 130.8 |
| Kupunguza misamaha ya kodi, kuzuia ukwepaji kodi na udanganyifu wa Biashara ya Nje | 742.74 |
| Mauzo ya hisa za Serikali | 415.55 |
| Marekebisho ya kodi Sekta ya madini (kodi ya Mapato, Kodi ya *CGT* na ushuru mbalimbali) (25% ya Mauzo ya Madini Nje) | 578.36 |
| Marekebisho ya Kodi na Usimamizi bora wa Mapato Kampuni za Simu | 502.26 |
| Marekebisho ya Kodi ya *SDL* | 243.52 |
| Mapato ya wanyamapori | 61.64 |
| Kuondoa msamaha wa ushuru wa mafuta-kampuni za madini | 44.9 |
| Usimamizi wa mapato ya utalii | 51.75 |
| Kuimarisha biashara katika *EAC* kwa kuongeza mauzo | 114.15 |
| JUMLA | 2,885.67 |

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo juu, vyanzo hivi vya mapato ni mjumuisho wa vyanzo ambavyo katika hotuba zetu mbadala za nyuma tumekuwa tukipendekeza, ambapo tumevifanyia marekebisho kulingana na hali halisi ya uchumi ulivyo kwa sasa, pamoja na kupendekeza baadhi ya marekebisho ya sheria za kodi ili kuongeza mapato zaidi kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitika kwa Serikali kuendelea kutengeneza madeni kwa Taifa kwa kuendelea kukopa zaidi kwa matumizi ya kawaida ya Serikali. Wakati Serikali inasisitiza kwamba, Deni letu linastahimilika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anaonesha mashaka makubwa sana kutokana na kasi ya kukua kwa Deni la Taifa. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa, Deni la Taifa linazidi kuongezeka kwa asilimia 38 kutoka shilingi trilioni 10.5 mwaka 2009/2010 hadi shilingi trilioni 14.4 mwaka 2010/2011.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, Deni la Taifa limefikia shilingi trilioni 20.3 mpaka ilipofika mwezi Machi mwaka 2012. Ukisoma taarifa ya mwezi Mei 2012 ya Benki Kuu ya Tanzania, Deni la Taifa sasa limefikia shilingi trilioni 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hapa siyo ustahimilivu wa Deni kama inavyodai Serikali bali ni kwamba tunakopa kufanyia nini? Bajeti ya Mwaka 2012/13 inayopendekezwa inaonesha kwamba, Serikali itakusanya shilingi trilioni 8.7 kama makusanyo ya ndani na itatumia shilingi trilioni 10.6 kama matumizi ya kawaida. Ni dhahiri kwamba, sehemu ya mikopo ambayo Serikali inachukua sasa itakwenda kwenye matumizi ya kawaida. Hatutaki mikopo kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya posho, kusafiri, magari na kadhalika. Tuchukue mikopo kuwekeza kwenye Miradi itakayokuza uchumi na kuzalisha kodi zaidi. Bajeti inaonesha kwamba, Serikali itakopa shilingi takriban trilioni tano mwaka 2012/13. Serikali ikubali kutekeleza mapendekezo ya Kambi ya Upinzani ya kuimarisha ukusanyaji wa kodi na kupanua wigo wa kodi katika maeneo muhimu kama Sekta ya Madini na Mawasiliano, kuzuia misamaha ya kodi, kutokomeza ukwepaji kodi na kuepuka matumizi mabaya ili kuepuka madeni yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapenda kusisitiza kwamba, Bunge lifanye ukaguzi maalumu kuhusu Akaunti ya Deni la Taifa ili kuweza kubaini ukweli kuhusu ustahimilivu wa Deni na mikopo ambayo Serikali inachukua kama inakwenda kwenye maendeleo na Miradi ipi na kama Miradi hiyo ina tija. Vilevile tumependekeza kwamba, mikopo yote ambayo Serikali inachukua iwe inapata idhini ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi au Bunge litunge sheria ili kiwango cha juu cha kukopa ambacho Serikali haipaswi kuvuka. Kuiacha Serikali inaendelea kukopa bila mpango ni kuliweka Taifa rehani na kupeleka mzigo wa kulipa madeni haya kwa kizazi

kijacho. Hatuwezi kukubali Wazee wetu waishi maisha yao, waishi maisha yetu na pia wakope maisha ya watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangali sura ya Bajeti ya Serikali, inaonesha kuwa Serikali itakopa fedha zenye masharti ya kibiashara ndani na nje yenye thamani ya shilingi trilioni 2.89 kwa kipindi hiki cha 2012/13. Athari ya mikopo ya kibiashara ya ndani ni kubwa sana kwa Watanzania, kwanza, inawafanya wananchi hasa wajasiriamali wanaokopa kushindana na Serikali yao, kwani mabenki yatashindwa kuwakopesha wafanyabiashara au wakikopa watakopa kwa masharti magumu na hasa riba kuwa kubwa. Jambo hili linapunguza uwezo wa wazalishaji kuongeza uzalishaji hasa viwandani kwa kukosa mikopo ya uendeshaji. Kama tulivyoshauri hapo juu, Serikali ijiepushe na mikopo ya masharti ya kibiashara kwa kuongeza makusanyo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya Serikali kuwa imepata Mshauri Mwelekezi atakayeishauri katika kujiandaa kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa madeni. Serikali ilieleze Bunge ni lini na kwa namna gani zabuni ya kumpata mshauri huyu ilitangazwa na kama Sheria ya Manunuzi ilifuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza Bajeti ya Shilingi za Tanzania trilioni 15 *(USD 8.75 Billion)* katika mwaka 2012/13 kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi wiki iliyopita. Uchambuzi wa Vitabu vya Bajeti unaonesha kwamba, mafungu ya juu matano yatakayoongoza kwa matumizi kwenye Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

1. Huduma kwa Deni la Taifa shilingi 2.7 trilioni *(USD 1.69 Billion);*
2. Wizara ya Ujenzi shilingi trilioni moja *(USD 625 Million);*
3. Wizara ya Ulinzi shilingi 920 bilioni *(USD 575 Million);*
4. Wizara ya Elimu shilingi 721 bilioni *(USD 451 Million);*
5. Wizara ya Nishati na Madini shilingi 641 bilioni *(USD 400 Million);*

Jumla shilingi *5.982* trilioni *(USD 3.74 Billion).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chanzo ni Vitabu vya Bajeti kwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya mafungu haya ni sawa na asilimia 40 ya Bajeti yote, kwa hiyo, asilimia 40 ya Bajeti yote imepangwa kwa mafungu matano tu na kati ya hayo Wizara ni nne tu za Ujenzi, Elimu, Ulinzi na Nishati na Madini. Wizara ya Kilimo wala Afya hazimo kabisa katika Wizara tano zitakazopata fedha nyingi zaidi katika Bajeti. Fungu lenye kiwango kikubwa zaidi ya Bajeti kuliko vyote ni Fungu 22 ambalo ni malipo kwa Deni la Taifa. Pia sehemu kubwa ya fedha zilizotengwa kwa Ujenzi na Nishati ni madeni kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya miaka ya nyuma. Shilingi bilioni 40 ambazo zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Kiwira katika Wizara ya Nishati na Madini ni kwa ajili ya kulipia Madeni ya Kampuni ya *TanPower Resources* ambayo iliuziwa Mgodi wa Kiwira na kushindwa kuundeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ya Deni la Taifa yanaonekana hapa katika matumizi ya Serikali ambapo tunapokuwa tunalipa madeni tunachukua rasilimali fedha nyingi kutoka kwenye Miradi ya Maendeleo. Wakati Bajeti ya Maendeleo ni shilingi trilioni 4.5, Bajeti ya kugharamia Deni la Taifa ni shilingi trilioni 2.7 (sawa na nusu ya Bajeti nzima ya Maendeleo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya 2012/13 ni ya kulipa madeni zaidi kuliko Bajeti ya kuchochea maendeleo ya Taifa letu. Bajeti hii pia yaweza pia kuwa ni Bajeti ya kukopa zaidi maana jumla ya shilingi 5.1 trilioni *(USD 3.19 Billion)* zitachukuliwa na Serikali kama mikopo kutoka vyanzo mbalimbali. Mikopo ya kibiashara ambayo ni mikopo ghali sana itachukuliwa kwa wingi zaidi kuliko mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa rasilimali za nchi kwenye sekta za kipaumbele (miundombinu ya usafirishaji kama reli, bandari, ndege viwanja vya ndege na kadhalika), barabara, nishati, kilimo na mifugo, ili kuinua uchumi, zimetengewa fedha kidogo sana kuweza kuleta tija kulingana na malengo ya Mpango wa Maendeleo kama ulivyopitishwa na Bunge lako Tukufu.

Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya nishati imeshuka kwa kiwango cha shilingi 40 bilioni, pia kwa mwaka uliopita fedha zilizotengwa kwa ajili ya miundombinu, reli na TEHAMA, zilitengwa shilingi 2,781.4 bilioni kwa 2011/12 ikilinganishwa na shilingi 1,505.1 bilioni kwa mwaka 2010/2011; hili lilikuwa ni ongezeko la asilimia 85. Kwa bajeti ya mwaka huu, inaonesha sekta zilezile za vipaumbele, bajeti iliyotengwa ni shilingi 1.394.5 bilioni ambayo ni pungufu ya asilimia 49.86 kwa kulinganisha na mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Fedha analiambia Bunge kuwa ametenga shilingi bilioni 1,383 kwa ajili ya usafirishaji na uchukuzi, Wizara ya Ujenzi imetengewa shilingi bilioni 1,000, kati ya hizo, Wizara ya Uchukuzi yenye Reli, Bandari, Viwanja vya Ndege na Usafiri wa Maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Viktoria imetengewa chini ya shilingi bilioni 380. Serikali pia haijasema fedha ambazo zilitengwa na Bunge katika Bajeti inayomaliza muda wake na kuzielekeza kwenye Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Uchukuzi zimetumikaje maana bado wakandarasi wanadai na fedha za reli hazikutoka zote kama ilivyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara nyingi hazikupata fedha za maendeleo kama zilivyopitishwa na Bunge. Halmashauri za Wilaya ndiyo zilipata hali mbaya zaidi katika kupata fedha za Maendeleo ambapo kwa wastani ni asilimia 47 tu ya Bajeti ndiyo ilipelekwa katika Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa. Kutokana na hali hii Wabunge kama wawakilishi wa wananchi walihoji Serikali kwenye Kamati zao na kupata majibu ambayo siyo ya kuridhisha hivyo kupelekea Wabunge kugomea baadhi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi wa hayo ni baadhi ya Kamati za Kudumu za Bunge kukataa kukubali Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa baadhi ya Wizara zilizo chini ya Kamati hizo. Wizara ambazo hazikupitishiwa au kukubaliwa makadirio yake ni pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Uchukuzi na nilishangaa kumwona Waziri wa Uchukuzi akiwaahidi wananchi pale Jangwani kwamba Reli inakarabatiwa vya kutosha ilhali Kamati haijapitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara yake kwa kuwa haikupewa fedha za kutosha na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla Bunge lako Tukufu halijajadili Makadirio ya Matumizi ya mwaka unaokuja ni vyema Serikali itueleze kwanza fedha zilizotengwa mwaka uliopita na hazikufika hatima yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano wa bajeti iliyotengwa kwa matumizi ya kawaida ambayo ni asilimia 70 wakati bajeti ya maendeleo asilimia 30 haiwezeshi nchi kupiga hatua ya haraka ya maendeleo. Kama ilivyooneshwa na Waziri Kivuli wa Mipango na nitakavyohitimisha hotuba hii, Serikali imetayarisha Bajeti hii bila kuzingatia masharti yaliyowekwa na Mpango wa Maendeleo uliopitishwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, ibara ya 63(3)(c), kwa kutotenga asilimia 35 ya mapato ya ndani ya Serikali kwenye Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo katika Miradi ya Maendeleo katika bajeti zake. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*, matumizi ya kawaida ya Serikali yanaongezeka huku matumizi katika shughuli za maendeleo yanapungua mwaka hadi mwaka. Zifuatazo ni takwimu zinazoonesha matumizi ya kawaida yanaongezeka na matumizi ya maendeleo yanapungua:-

Fungu: Fedha za matumizi ya kawaida; mwaka 2009/2010, Sh). 6,251,629,581,428, asilimia 73; mwaka 2010/2011, Sh. 7,587,424,923,903, asilimia 77.

Fedha za matumizi ya maendeleo; mwaka 2009/2010, Sh. 2,299,010,652,135, asilimia 27, mwaka 2010/2011, Sh. 2,223,684,150,465, asilimia 23.

Jumla 2009/2010 Sh. 8,550,640,233,563, asilimia 100; na 2010/2011 Sh. 9,811,109,074,368, asilimia 100. Chanzo ni Ripoti ya *CAG*, ukurasa wa 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa miaka miwili iliyopita, yaani 2009/2010 na 2010/2011, kumekuwa hakuna uwiano wa fedha za Maendeleo kama bajeti zilivyopitishwa na Bunge dhidi ya fedha zinazotolewa na Hazina kwa ajili ya maendeleo katika Wizara na Idara. Tazama mchanganuo ufuatalo:-

Mwaka 2009/2010, Bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa Sh. 2,825,431,400,000; fedha halisi zilizotolewa Sh. 2,299,010,652,135, tofauti Sh. 526,420,747,865, sawa na asilimia 19.

Mwaka 2010/2011, Bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa Sh. 3,750,684,569,000; fedha halisi zilizotolewa Sh. 2,223,684,150,465, tofauti Sh. 1,527,000,418,535, sawa na asilimia 41.

Chanzo ni Ripoti ya *CAG*, ukurasa wa 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na takwimu hizi, jumla ya Sh. 1,527,000,418,535 au asilimia 41 ya fedha zilizoidhinishwa kwa maendeleo hazikutolewa katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na kiasi cha Sh. 526,420,747,865 au asilimia 19 ya fedha zilizoidhinishwa mwaka 2009/2010 hazikutolewa pia. Hii ina maana kuwa, shughuli za maendeleo za kiasi hicho cha fedha hazikutekelezwa kwa miaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatafsiri hali hiyo kama utovu mkubwa wa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa upande wa Serikali. Vilivile inaonesha ni jinsi gani Serikali yetu haithamini maendeleo, ndiyo maana kila mwaka Serikali inazidisha matumizi yake na kuhakikisha kuwa inayapata kwa wakati huku ikipunguza bajeti ya maendeleo na kutotoa fedha zote kama zilivyoidhinishwa na mbaya zaidi hata zile zinazotolewa hazitolewi kwa wakati mwafaka. Hii inafanya kukaa hapa Dodoma na kupitisha Bajeti kuwe hakuna maana kwani Bajeti haitekelezwi kama ilivyopitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi kinachotengwa kwa ajili ya maendeleo kimeshuka kutoka shilingi trilioni 4.9 katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12 hadi kufikia kiasi cha shilingi trililioni 4.5 Mwaka huu wa Fedha wa 2012/13. Pamoja na Serikali kushindwa kutekeleza miradi ya maendeleo katika bajeti iliyopita, bado imeendelea kupunguza bajeti ya maendeleo katika bajeti hii. Ni dhahiri Serikali haizingatii swala la maendeleo ya mwananchi, pia kutoona njia ya kuweka mkazo katika maendeleo na kuendelea kupuuzia maazimio ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti Mbadala, Kambi ya Upinzani imetenga asilimia 36.06 na kukidhi matakwa ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kutoka katika mapato ya ndani kwa matumizi ya maendeleo kama Mpango wa Maendeleo ya Taifa ulivyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliamua kama Taifa kwamba, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ndiyo safina yetu ya kuelekea nchi ya ahadi *(middle income country)*. Mpango ukapitishwa na Bunge na kuwekwa sahihi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Inasikitisha kuona kuwa, Serikali inatoboa kisirisiri safina hii wakati tupo katikati ya maji! Ninaamini wananchi wanawaona wanaotoboa safina yetu na watawatosa kabla hawajazamisha Taifa zima kwa kushindwa kutekeleza Mpango unavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fedha za maendeleo kutolewa kidogo kulinganisha na bajeti inayopitishwa na Bunge, bado kumekuwepo na matumizi yasiyo na tija na ubadhirifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu wa fedha za umma umeendelea kuwa kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi. Uchambuzi wetu juu ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa mwaka 2010/2011 pekee, umebaini takriban jumla ya shilingi bilioni 12.9 (12,968,168,985) za fedha za umma zimepotea kama ongezeko kutoka shilingi bilioni 11.9 (11,152,048,065) ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 14 ya upotevu wa fedha za Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

Hii inaonesha kuwa Serikali inaona ni jambo la kawaida kupoteza viwango hivi vya pesa za Serikali na Kambi ya Upinzani kuwasisistiza wananchi kuendelea kuitathmini Serikali yao sasa ili kuweza kufanya maamuzi sahihi dhidi ya Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kambi ya Upinzani juu ya Sera ya Matumizi 2012/2013 ni kuwa lengo kuu la Bajeti Mbadala ni kuhakikisha uchumi unakua katika maeneo ya vijijini kwa kati ya asilimia sita na nane ili kuleta maendeleo ya wananchi na kutokomeza umaskini.

Kwa njia hiyo ni dhahiri wananchi wapatao milioni 30 waishio vijijini watanufaika na matumizi ya rasilimali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya bajeti ya matumizi ni kama ifuatavyo:-

(i)Kujenga mazingira ya ukuaji wa uchumi vijijini *(Rural Growth)* kwa kuboresha miundombinu ya umeme, barabara, maji na miundombinu ya umwagiliaji. Tunapendekeza kutumia Shilingi bilioni 600 kila mwaka (Shilingi bilioni 150 kwa kila sekta niliyoitaja). Fedha hizi zitasimamiwa na Mamlaka ya Maendeleo Vijijini *(Rural Development Authority – to be established)* itakayokuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

(ii) Kukarabati Reli ya Kati na matawi yake ya Tanga/Arusha na Mpanda. Tutatenga Shilingi bilioni 443 kwa *RAHCO* kwa ajili ya reli. Lengo ni kuhakikisha Reli ya Kati inafikia uwezo wa kusafirisha tani 1.5m kwa mwaka na hivyo kulipatia Taifa fedha za kigeni katika Sekta ya Usafirishaji kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Tunataka Sekta ya Usafirishaji iliingizie Taifa fedha za kigeni mpaka Dola za Kimarekani bilioni 1.5 kutoka Dola bilioni 0.5 za sasa.

(iii) Kuboresha Elimu na Afya hasa kwa Shule na Zahanati/Vituo vya Afya vya Vijijini kwa kutoa motisha kwa wafanyakazi wa Sekta hizi walio kwenye Halmashauri za Wilaya. Tunapendekeza posho za Mazingira ya Vijijini kwa Walimu, Madaktari na Manesi sawa na mara moja na nusu ya mishahara yao. Vile vile tunapendekeza kuongeza mishahara ya Walimu, Manesi na Madaktari kwa asilimia 50, pamoja na kuboresha stahili nyingine za kazi ili kuvutia Watanzania wengi zaidi katika maeneo haya na kuboresha huduma zao kwa wananchi. *(Makofi)*

(iv) Tunapendekeza kuongeza kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa umma mpaka Sh. 315,000/= kwa mwezi. *(Makofi)*

(v) Tunapendekeza kuanzisha Pensheni ya uzeeni kwa wazee wote nchini wenye umri wa zaidi ya miaka 60.

(vi) Tuapendekeza kujenga uwezo wa viwanda vya ndani ili kuuza nje bidhaa za kilimo na mifugo zilizoongezewa thamani. Tutazuia kuuza nje korosho ghafi na ngozi ghafi kwa kuanzia. Lengo ni kufufua viwanda vyote vya nguo na kuanzisha viwanda vipya kwa kutoa motisha kwa wawekezaji watakaotumia malighafi za hapa nchini. *(Makofi)*

(vii) Kupunguza mzigo wa matumizi ya magari ya Serikali kwa kupiga mnada baadhi ya mashangingi na kuweka mfumo wa kukopesha magari kwa watumishi wote wa umma wanaostahili magari kama alivyofanya Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Katika Taarifa yake, kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, Waziri wa Fedha alitamka: "Kufanya mapitio ya stahili za aina za magari kwa viongozi wa ngazi mbalimbali na kuandaa mwongozo wa kugharamia ununuzi wa vyombo vya usafiri ili kupunguza matumizi ya magari, mafuta na matengenezo ya magari", kama hatua za kubana matumizi. Hatua hii ya kupunguza gharama za magari Mheshimiwa Waziri hakuisema kabisa katika hotuba yake Bungeni. *(Makofi)*

(viii) Kuendelea kusisitiza kufutwa kwa posho za vikao katika mfumo mzima wa malipo na stahili kwa watumishi wa umma. Katika Taarifa yake kwa Kamati ya Fedha, Waziri wa Fedha alitamka: "Kufanya mapitio ya posho na stahili zote kwa lengo la kuziwianisha." Suala hili nalo Waziri hakulizungumza kabisa katika hotuba yake Bungeni.

(ix) Kuanzisha Chuo Kikuu cha Mtwara *(Mtwara University for Petroleum Studies)* ili kuzalisha wataalamu wa kutosha wa Sekta ya Mafuta na Gesi na kuliandaa Taifa kuwa na wasomi mahiri wa maeneo hayo na hivyo kufaidika na utajiri wa mafuta na gesi uliopo nchini kwetu. Tunapendekeza Shilingi bilioni 200 mwaka huu katika Bajeti ya Wizara ya Elimu kwa ajili ya Mradi huu wa Chuo Kikuu cha Mtwara. Hatutaki kurejea makosa tuliyoyafanya kwenye Sekta ya Madini, tunataka kumiliki gesi yetu vizuri. *(Makofi)*

(x) Kutunga sheria mpya ya Mashirika ya Umma *(Public Corporations Act)* ili kujengea uwezo Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kusimamia vyema Mashirika yote ya Umma ambayo Serikali inamiliki kwa zaidi ya asilimia 100 na kutoa nguvu za kisheria kwa Shirika la *CHC* kuweza kusimamia hisa za Serikali katika Kampuni na Mashirika ambayo Serikali inamiliki chini ya asilimia 50.

(xi) Kupunguza gharama za safari za nje kwa kupunguza ukubwa wa misafara na madaraja ambayo viongozi wanasafiria. Eneo hili la safari za nje limekuwa likiigharimu Serikali fedha nyingi sana. Unakuta Sekretari wa Serikali yuko *Business Class,* Balozi anayetoa misaada kwa Tanzania yuko *Economy*. Hali hii tunataka kuipiga marufuku mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hatua mbalimbali za kikodi tulizozichukua, Kambi ya Upinzani inapendekeza Bajeti ya Shilingi trilioni 15 ambazo zitapatikana kwa mapato ya ndani ya Shilingi trilioni 11.9 na misaada na mikopo ya kibajeti ya Shilingi trilioni 3.2 kama ilivyopendekezwa na Serikali. Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali kutokukopa kibiashara ili kudhibiti ukuaji wa deni la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba Serikali itatumia Shilingi trilioni tisa katika matumizi ya kawaida na Shilingi trilioni sita kama matumizi ya maendeleo. Katika fedha za maendeleo, asilimia 35 ya mapato ya ndani yameelekezwa huko kama ilivyoagizwa na Mpango wa Maendeleo ya Taifa ulioidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba.

**SURA YA BAJETI MBADALA YA MWAKA 2012/2013**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **MAPATO** | | **SHILINGI MILIONI** |
| **A** | **Mapato ya ndani** | | **11,889,078** |
| | i)mapato ya kodi (TRA) | | |
| | ii)Mapato yasiyo ya kodi | | |
| **B** | Mapato ya Halmashauri | | |
| **C** | Mikopo na Misaada ya kibajeti (GBS) | 842,487 | |
| **D** | Misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo nay a kisekta | 2,314,231 | |
| | i)Misaada | 1,465,461 | |
| | ii)Misaada na mikopo kisekta | 415,137 | |
| | iii)MCC(MCA-T) | 433,634 | |
| | **Jumla ya Misaada na mikopo ya kibajeti** | | **3,156,718** |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE.** | | **15,045,796** |
| | **MATUMIZI** | | |
| **E** | **Matumizi ya Kawaida** | | **9,000,000** |
| **H** | **Matumizi ya Maendeleo** | | |
| | (i)Fedha za ndani | 4,161,177 | |
| | (ii)Fedha za Nje | 1,884,619 | |
| | **Jumla ya matumizi ya maendeleo** | | **6,045,796** |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE.** | | **15,045,796** |

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wakati Kamati za Bunge zilipokaa kujadili taarifa ya Serikali kuhusu Mfumo wa Mapato na Matumizi, Waziri wa Fedha na Uchumi alitoa Taarifa kuhusu fedha za rada zilizorejeshwa, jumla ya Shilingi bilioni 72.3 ambazo zilipokelewa tarehe 26 Machi, 2012. Kwa mshtuko wa Wabunge, Waziri aliiambia Kamati kuwa mchakato wa manunuzi ya vitabu na

madawati kwa kutumia fedha hizi ulikuwa umeanza chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI. Fedha hizi hazijawahi kupitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuzitumia fedha hizo kabla ya kupitishwa na Bunge ni kuvunja Sheria za Fedha kuhusiana na masuala ya Bajeti. Wakati Waziri akiwasilisha hotuba yake, hakugusia kabisa suala la fedha zilizorejeshwa kutokana na ununuzi wa rada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inataka maelezo ya Serikali juu ya fedha hizi na utaratibu wa kuzitumia. Kambi inataka kufahamu vigezo vilivyotumika kuteua Mikoa ya Mwanza, Morogoro na Dar es Salaam peke yake kutumia fedha hizi. Kambi pia inapenda kufahamu Deni lililochukuliwa kununua Rada hii iliyoleta kashfa kubwa sana hapa nchini limefikia kiasi gani hivi sasa na tutakapokuwa tumemaliza kulilipa na tutakuwa tumelipa jumla ya kiasi gani kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uumbaji wa bajeti ya Serikali umekuwa ni ule ambao unapendelewa zaidi na wale wavivu wa kufikiri, yaani mfumo rahisi, wataalamu wanauita *Incremental Budgeting*. Mfumo huu hujikita zaidi katika kutizama ukuaji wa mapato na kugawa mapato hayo kwa mtindo wa nyongeza ya asilimia fulani toka katika bajeti iliyotangulia. Mfumo huu huacha kuzingatia mambo mengi mtambuka. Mfano, tunaweza kutazama sekta mojawapo ya umeme ambapo tukifanya uumbaji wa bajeti kwa mfumo wa kiasi cha nyongeza *(incremental budget),* kuna thamani halisi ambazo ukizitazama kwa bei wazi ya soko, tayari zimepaa sana ndani ya miezi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni, tukiwa ni Serikali ambayo tunasubiri kukabidhiwa dola, tunapendekeza kwamba ni vyema tukaanza kutazama uwezekano wa matumizi ya *Zero Budgeting* ambapo, japo ni mfumo ambao unahitaji kazi ya ziada, lakini una faida sana kwani hutazama mipango ya matumizi kulingana na wakati uliopo huku ikifanya rejea ya wakati uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia inapendekeza kwamba Bajeti za Mashirika ya Umma ziwe sehemu ya Bajeti Kuu ya nchi kwani kuna masuala mengi yanayotekelezwa na Mashirika haya na wananchi kupitia Bunge hawayajui. Ni vyema katika mfumo mpya wa Bajeti tutakaokuwa nao kufuatia mapendekezo ya Spika wa Bunge ambapo kutakuwa na Ofisi ya Bajeti ya Bunge na Kamati ya Bunge ya Bajeti, Sheria ya Bajeti *(Fiscal Responsibility Act/Budget Act)* izingatie suala la kuziweka kama viambatisho Bajeti za Mashirika ya Umma katika Bajeti ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Serikali ya mwaka huu kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Fedha, imewasahau kabisa wananchi wa vijijini na haina mkakati wowote wa kuwakomboa Watanzania walio wengi wanaoishi huko. Mipango mingi ya kikodi katika Sera ya Mapato ya Serikali itasaidia wakazi wa mijini ambao ni asilimia 25 tu ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapenda kuweka msisitizo kwamba Tanzania bado ni nchi ya Wakulima, maana robo tatu ya Watanzania wanaishi vijijini ambapo hawajui hizi hadithi za uchumi kukua tunazoimba na kupewa sifa kila siku. Hawa ni watu milioni 30 ambao hawana maji, hawana umeme, mazao yao hayafiki sokoni maana hawana barabara nzuri, shule wanazosoma watoto wao hazina Walimu maana wanakimbia mazingira magumu*. (Makofi)*

Hawa Watanzania wa chini milioni 30 *(The Bottom 30m)* tunaowawakilisha hawana bima mazao yakiharibiwa na wala hawana pensheni wanapokuwa wamezeeka na kupoteza nguvu za kufanya kazi. Hawa '*The Bottom 30m'* bado wanaishi maisha waliyoshi babu zetu. Hawa Watanzania milioni 30 tumewasahau. Tunajenga mataifa mawili ndani ya nchi moja; moja la mafukara (wanavijiji) na moja la wanaojiweza (wa mijini). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kujibu kitendawili cha kuwa na uchumi unaokua kwa kasi lakini haupunguzi umasikini, inabidi kuelekeza nguvu zetu vijijini walipo Watanzania wengi. Kukuza uchumi wa vijijini kwa kuwekeza kwenye misingi ya kujenga uchumi imara, ndiyo njia pekee ya kutokomeza ufukara wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti Mbadala ya Kambi ya Upinzani mwaka huu ni Bajeti ya ukombozi wa mwananchi. Licha ya kwamba tunahitaji ukuaji wa kasi zaidi wa uchumi, changamoto sasa ni namna gani ukuaji huu wa uchumi unawafikia wananchi milioni 30 wa vijijini na kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliwasilishwa Bungeni na Serikali na kupata pongezi nyingi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini cha kushangaza, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kuutekeleza kwa vitendo Mpango huu wa Taifa. Mwaka wa kwanza Mpango haukuwekewa fedha kwa kuwa ulikuwa wa Mpito wanavyodai wao. Mpango unahitaji angalau Shilingi trilioni nane kila mwaka ili uweze kutekelezwa. Mpango ulipata Shilingi trilioni moja tu mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Bunge liliazimia namna ya kuhakikisha tunapata fedha za kuendeleza nchi yetu sisi wenyewe, naomba kunukuu ukurasa wa 92 kifungu cha 4.3.1 katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, toleo la Kiswahili kama ifuatavyo: "Kwa kuelewa kuwa wakati wote kutakuwa na miradi ya uwekezaji nje ya mpango, Serikali, kuanzia sasa, itakuwa inatenga asilimia 35 ya makadirio ya mapato yake ya ndani, siyo makadirio ya bajeti, makadirio ya mapato ya ndani kwa ajili ya kugharamia bajeti ya maendeleo kila mwaka." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali imetenga asilimia sifuri ya mapato ya ndani kwa ajili ya kugharamia Bajeti ya Maendeleo, Serikali hii imeshindwa kusimamia ahadi zake yenyewe kama inavyoonekana katika Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano. Serikali hii ya CCM imeshindwa kuheshimu uamuzi uliopitishwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(c ) madaraka ya Bunge ni pamoja na "Kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo", Bunge liliidhinisha Mpango kwa mujibu wa ibara tajwa ya Katiba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungmzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti ya mwaka 2012/2013 iliyowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Uchumi haikukidhi matakwa ya Mpango wa Maendeleo kama ambavyo ulipitishwa na Bunge...

**MWENYEKITI*:*** Mheshimiwa Zitto ni kengele ya pili.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iiondoe *(withdraw)* Bungeni Bajeti iliyoileta ili ikatayarishwe upya ili ikidhi matakwa *(compliance)* ya Mpango wa Maendeleo kama ulivyoidhinishwa na Bunge na kusainiwa na Rais wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, hayo uliyoyasema mwisho hayajaingia kwenye *Hansard*. Waheshimiwa Wabunge hayo yaliyosemwa mwisho, hayajaingia kwenye *Hansard*. Mimi ndiyo ninayeongoza Kiti na mimi ndiye ninayetunza muda wa kuongea, na tayari nilishatoa taarifa ya mwisho wa hotuba hii kufikiwa na kama Mheshimiwa Zitto alikuwa na lengo hilo ilimpasa ajali huu muda na kuutumia muda wake vizuri kama tulivyou-*control* katika wasemaji wengine.

Kwa hiyo kwa kuwa mambo haya hayajaingia kwenye *Hansard* na muda ulikwishapita, ninaomba sasa tuendelee na utaratibu kama unavyotakiwa na utaratibu wetu unaotakiwa sasa ni kumsikiliza mchangiaji wetu wa kwanza, Mheshimiwa Richard Ndassa na hotuba hii ya hotuba hii ya bajeti itapitishwa rasmi siku ya Ijumaa, kwa hiyo, tunaendelea na mchango wa mawazo na maamuzi ya hotuba hii yatafanyika siku ya Ijumaa wiki hii.

Mheshimiwa Richard Ndassa atafuatiwa na Mheshimiwa Shekifu atafuatiwa na Mheshimiwa Sara Msafiri.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya awali na mimi nichangie katika bajeti hii. Kwanza niseme tu kwamba naiunga mkono Bajeti ya Serikali kwa asilimia mia moja. Kwa sababu bila kuiunga mkono, yapo mengi ambayo yamejielekeza mle ndani, yote ni ya kwenda kuyatekeleza kwa mwaka huu wa fedha. Ndugu yangu, mdogo wangu Mheshimiwa Zitto, nakuomba na kukushawishi pamoja na Kambi ya Upinzani tuiunge mkono bajeti hii ili kusudi haya tuliyoyasema yaende kutekelezwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kawaida ya wenzetu kufanya hivyo, lakini tunawasamehe bure. Leo ni tarehe 18 Juni, kawaida kwa zao la Pamba ndiyo msimu ulitakiwa uanze leo. Lakini cha ajabu mpaka leo hii, bei ya kuanzia kwa kilo haijatangazwa. Nashangaa, sijui ilikuwa ni kwa sababu gani, lakini kauli mbiu ambayo nasema Wabunge wenzangu wanatoka kwenye zao la Pamba, bila Sh. 1,000/= hakuna Pamba. Pamba haiozi! Narudia, bila Shihubi, hakuna pamba! *(Makofi)*

Nawaomba wakulima wa zao la Pamba katika Wilaya 42 kwa Watanzania wanaotegemea zao la Pamba zaidi ya milioni 16, tusipuuze zao la Pamba. Naomba wakulima wa zao la pamba na mnaonisikia msiwe na haraka ya kuuza Pamba kwa sasa mpaka bei itakapokuwa nzuri na bei ya kuanzia na tuiombe Serikali, nimesema watu milioni 16 sio wachache, bei ya kuanzia lazima iwe Sh. 1,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mwenyekiti wangu wa Kamati Mtemi Andrew Chenge na niungane naye kwa kuzisemea zile kero ambazo wananchi wetu, wafanyabiashara wadogo wenye pikipiki kwa jina maarufu boda boda walikuwa wanasumbuliwa kweli kweli kutaka kulipa Sh. 35,000/=. Lakini pia Mama Lishe, maduka madogo madogo yaliyoko Nyambizi, Kadashi, Mwembeshimba na sehemu nyingine walikuwa wanakimbizwa, wanachukuliwa mizani zao, Mama Ntilie wanabebewa sahani zao, boda boda wananyang'anywa piki piki zao, lakini naiomba Serikali kwa sababu biashara zao hazizidi Shilingi milioni tatu, tusiwasumbue, na hili liwe Azimio la Bunge kwamba tukiona wanasumbuliwa, basi wale wanaohusika wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anazungumzia kuhusu uimarishaji wa viwanda na niombe Serikali kwa sababu imetozwa Shilingi bilioni 128.4, naomba sana kwa sababu tunalo zao la Pamba, hebu angalau kwa kuanzia, pesa hizi ziende zikajenge kiwanda cha Pamba, nyuzi. *(Makofi)*

Nimesema mwanzo kwamba Wilaya 42 zinalima zao la Pamba, lakini vinu vya kuchambulia Pamba ni vichache sana kwa hivi sasa, lakini hatuna kiwanda cha Pamba nyuzi, pesa hizi tuzielekeze huko.

Pili, zao la Korosho kwa pesa hizi tukizipanga vizuri, Shilingi milioni 128.4 tukazielekeza kwenye Pamba, Korosho angalau kwa kuanzia tutakuwa tumeongeza ajira, lakini mazao yetu yatakuwa hayaendi tena ghafi kama ilivyo sasa. Naomba sana Serikali, pesa hizi isizitawanye, eti kila Mkoa ziende huko, hapana. Tuanze na viwanda vitatu vikubwa; cha Pamba, Korosho pamoja na Kahawa. *(Makofi)*

La tatu, ni usimamizi wa fedha za umma. Hapa ndipo penye tatizo kubwa sana. Nidhamu ya matumizi haipo, malipo hewa ni mengi mno, taratibu hazizingatiwi, lakini zipo Wizara mama au vinara zinazoongoza kwa kutofuata taratibu Wizara ya Fedha yenyewe, Wizara ya Kilimo, pamoja na TAMISEMI. TAMISEMI kule kuna mianya ya miradi hewa. Tulipokuwa kwenye *RCC* tulimwomba

Mkaguzi Mkuu; ipo miradi ya umwagiliaji katika kijiji cha Shilanona, Mahiga, pamoja na Kimiza. Mradi wa Mahiga, una mabilioni ya pesa, lakini kinachofanyika ukienda kuangalia hakuna kinachofanyika. Kwa mfano, hiyo miradi imekuwa kama uchochoro wa pesa kupitia. Lakini walimu hewa wanatoka wapi? Wizara ya Elimu wanafahamu. Naiomba Serikali na vyombo vyetu vitatu; Tume ya Maadili fanyeni kazi yenu! TAKUKURU, fanyeni kazi yenu! TAKUKURU wamekuwa kama vile vinyago vya kwenye majaruba, ndege wanakuja wanatua kwenye bega wanakutikisa kama unatikisika, kama hautikisiki wanaanza kula mpunga na wewe uko pale, pale. *(Makofi)*

Imekuwa kama Mbunge sasa, eti mpaka Bunge liseme, ndiyo TAKUKURU waamke huko waliko. Kazi ya Bunge ni kazi nyingine, lakini TAKUKURU ni kazi yao kuangalia: Je, hivi haya mambo yanayosemwa, hivi rushwa zinazotembea, wao hawazioni mpaka Bunge liseme? TAKUKURU fanyeni kazi yenu, lakini Usalama wa Taifa umesisinzia na tunajua Usalama wa Taifa ndiyo chombo kikuu kinachoweza kuisaidia nchi hii. Hivi leo inapofikia Twiga kusafirishwa bila wao kujua, lakini wakimbizi kutoka Namanga wanapakiwa kwenye lori, wanakwenda kukamatwa Mbeya, Iringa, hivi, usalama wa Taifa haupo?

**WABUNGE FULANI:** Haupo!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana vyombo vitatu hivi, fanyeni kazi yenu, maana yake tumezoea huku ndani Waheshimiwa Mawaziri kuwajibika Wabunge kuwajibika, lakini na ninyi wakubwa zetu huko siyo vizuri kusema vyombo hivi, lakini itafikia kipindi na ninyi muwajibike kwa sababu hamtimizi wajibu wenu kwa nchi yetu. Mambo mengi yanafanyika, lakini ninyi hamyaoni, lakini kama mnashauri na ushauri wenu hautekelezwi mara ya kwanza, ya pili, basi tafuta njia ya kutokea, acha! Kwa sababu haiwezekani ukawa unashauri tu, lakini ushauri wako hautekelezwi. Lakini nina uhakika na imani na vyombo hivi, nawashauri sana tufanye kazi ambayo sisi tumepangiwa.

La mwisho, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuna Shilingi bilioni 300…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili hiyo!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, msemaji wetu wa pili ni Mheshimiwa Henry Shekifu, lakini nikiangalia humu ndani ya Ukumbi sijamwona. Sasa nitampa nafasi Mheshimiwa Sarah Msafiri na atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MJUMBE FULANI:** Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Nani anaomba mwongozo?

**MBUNGE FULANI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Baadaye, ngoja aendelee kuchangia.

**MHE. SARAH MSAFIRI ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili kuwa mchangiaji wa pili katika hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kwanza kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam na hatimaye Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yangu kwa sababu moja kubwa, mgawo wa umeme ilikuwa ni gumzo kubwa kwenye nchi hii na ilipelekea kupunguza uzalishaji kwenye viwanda. Kwa hiyo, kuwepo kwa umeme wa kutosha ambao ni umeme wa gesi, naamini kabisa

kama siyo kumaliza kabisa, lakini itapunguza kwa kiasi kikubwa mgawo wa umeme, itaongeza uzalishaji viwandani na itapunguza makali ya gharama za maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, napenda kuongelea kwenye Sekta ya Kilimo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyoiwasilisha Bungeni, tunaona kwamba kwenye sekta nzima ya kilimo imetengwa Shilingi bilioni 67 tu kwenye masuala ya maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hizo, Shilingi bilioni 67 kuna mabonde ya Kilombero na bonde la Ulanga ambalo lipo Mkoani Morogoro ambapo kila bonde limetengewa Shilingi bilioni moja tu na fedha iliyotengwa ni kwa ajili ya upembuzi yakinifu na mchoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najiuliza, kama sasa tupo mwaka 2012 tunaelekea mwaka 2013, bado Serikali inatenga fedha kwa ajili ya masuala ya upembuzi yakinifu na michoro, tutalima lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilombero tumepewa jukumu la kuzalisha Mpunga wa kutosha kuwalisha Watanzania wote zaidi ya milioni 40, katika taarifa zote zilizosomwa zimeeleza. Sasa najiuliza, kwa shilingi bilioni moja ya upembuzi yakinifu, tutaanza kuwalisha Watanzania lini? Tutalima lini? Lakini Kilombero tuna tatizo la daraja la Kilombero, kile kivuko ni kibovu na hakiwezi kuhimili kuhakikisha kwamba huduma za usafirishaji zinaboreshwa. Sasa nasema kwamba hii fedha kwanza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati unavunja kanuni kwa kukatisha mbele ya mzungumzaji. Naomba utulie mpaka atakapomaliza.

Mheshimiwa Sarah Msafiri endelea!

**MHE. SARAH MSAFIRI ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema, hizi Shilingi bilioni saba zilizotengwa kwa ajili ya mabonde haya kwenye kilimo, ni ndogo sana na tunaamini hiki ndiyo kipaumbele chetu cha kwanza kwenye kilimo, na tunaamini gharama za maisha za wananchi zinapanda kutokana na ukosefu wa chakula. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ikae na itazame upya bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata wasiwasi sana na suala la kuboresha kilimo na kuhakikisha tunazalisha vyakula vya kutosha, kwa sababu naona bajeti nzima ya kilimo kwenye masuala ya maendeleo imetengewa Shilingi bilioni 67, lakini hapo hapo Serikali imetenga Shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kulipa fidia kwenye mradi wa *EPZ* Bagamoyo na Kigoma. Sasa najiuliza, hii miradi ya *EPZ* ni *private sector,* Serikali inatoaje fedha za wananchi na walipakodi, watu wa chini kwenda kulipa fidia kwenye miradi ya *EPZ* wakati Watanzania wana njaa? Miradi ya kilimo imetengewa Shilingi bilioni 60 tu na Shilingi bilioni 50 nzima inakwenda kuwapelekea wawekezaji ambalo ni suala *private sector?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hapa ni lazima busara itumike. Hawa wawekezaji kama wamekuja kuwekeza kwenye nchi yetu, ni lazima wajue kwamba kuna gharama za kulipa fidia kwenye maeneo ya uwekezaji na kama kutakuwa na kulipana, wakishawekeza tutalipana mbele kwa mbele, lakini hii Shilingi bilioni 50 kuwalipa fidia wananchi katika miradi ya *EPZ* ambayo ni *private sector* itolewe, iletwe kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kuongeza gharama za simu kwenye muda wa maongezi. Tumeambiwa kwamba kutokana na haya ni maazimio ya soko la pamoja na *East Africa* kupandisha gharama za simu. Lakini siwezi kukubaliana na hili. Tunaelewa gharama za simu siyo anasa, wananchi vijijini wanatumia simu kuulizia bei ya mazao kwenye masoko, wanafunzi mashuleni na vyuoni wanatumia simu kutafuta taarifa mbalimbali kuwasaidia kwenye masomo yao na kama tunavyojua kwenye shule na vyuo vyetu hakuna vitabu vya kutosha. Lakini vilevile wananchi wanatozwa huduma za M-pesa na huduma mbalimbali kwenye mitandao ya simu, na katika pato la Taifa makampuni ya simu Tanzania yanachangia 2.5% tu, Uganda yanachangia 5% na Kenya wenzetu yanachangia 9%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhahiri kabisa kwamba Serikali haijaweza kudhibiti mapato kwenye makampuni ya simu, tunaibiwa. Halafu leo badala ya kupeleka hili ongezeko ambalo wameridhia kwenye Shirikisho la pamoja na *East Africa* kupeleka kwenye makampuni ya simu wanamletea mlaji ambaye ni mtu wa chini. Hii siyo sawa sawa na haikubaliki. Ni lazima Serikali idhibiti mapato yake, siyo kila jambo unampelekea Mtanzania wa chini kwenda kulipia gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeongeza kodi kwenye vinywaji, mpaka vinywaji baridi. Leo tena mnakwenda kupandisha gharama za simu! Lakini kila Mtanzania anayepiga simu anakatwa 18% ya *VAT* ambayo hii inakwenda Serikalini, sasa tena leo mnakuja mnapandisha gharama za *excess duty* kutoka 10% hadi 12%, mimi nasema hilo haliwezekani, nitaunga mkono baada ya marekebisho ya haya niliyoyaongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Henry Shekifu hayupo, sasa nitamwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, ningemwomba Mheshimiwa Waziri azingatie sana mapendekezo ya Kamati na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani katika kupanua wigo wa kodi. Kumekuwa na tabia ya mapendekezo mazuri kupuuzwa. Nakumbuka wakati mmoja tulipendekeza kwamba meli zilizopo baharini nyingi zikamatwe na zikatwe mapato, tukapuuzwa baadaye ikakamatwa meli tukaona mazao ya Samaki yaliyopatikana na fedha ngapi zimepotea. Mheshimiwa Zitto kasahau kidogo kuiweka hiyo na kuna meli nyingi bado 67 Wawi zinavua, zikamatwe nazo ili tupate mapato. Kwa hiyo, naomba mapendekezo haya Mheshimiwa Waziri uyafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ningemwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie katika suala zima la Kikatiba na mgawanyo wa mapato ya Muungano ambayo katika Kamati nilimweleza. Bunge lililopita Mheshimiwa Waziri aliahidi atakuja na *formula* ya mgawanyo wa mapato ya Muungano kwa mujibu wa Katiba. Sasa naomba hilo uliweke kabisa, utapenda kupata maelezo yake.

Tatu, kwa sababu ya muda, sisi tunapenda wawekezaji waje nchini lakini hatupendi wawekezaji waje nchini wawanyanyase Watanzania wala hatupendi waje hapa wachukue raslimali za Tanzania bila ya sisi kupata chochote.

Kuna mwekezaji mwenye kampuni ya *Mineral Extraction Technology Limited* ana *passport* tano. *Passport* tatu ni za Ubelgiji, *passport* mbili ni za Burundi. Aliwahi hata kwenda Wizarani Mambo ya Ndani na Waziri Shamsi wakati huo akampiga *PI*, sasa sijui alitumia *passport* gani ya kurudi nchini na yupo nchini bado. Amewahi hata kumtukana Kamishna wa Madini ambaye sasa hivi ni Mbunge, lakini hata juzi tulipopata taarifa zake ambazo tunadhani ni za kijasusi kidogo, tukazipeleka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri akachukua hatua, mwekezaji huyo alikodi chumba hoteli ya *Holiday Inn*, vyumba viwili, Askari walipokwenda kile chumba ambacho alitakiwa kuwepo hakuwepo na akatoroka baadaye watu wakazungumza naye na Askari wakazungumza naye sijui lugha gani lakini bado yupo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa nitaileta rasmi kwa Mheshimiwa Spika, nimeipeleka Wizara ya Mambo ya Ndani, naomba sana Bunge hili tukatae watu wanaokwepa kodi, wanaokwenda kutumia nafasi zao vibaya na kuwanyanyasa Watanzania. *(Makofi)*

Nitaomba kabisa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Kamati ya Nishati na Madini na Kamati ya Fedha na Uchumi, tuchague watu wawili wawili kwa amri yako ili tulishughulikie jambo hili haraka, kwani ndani yake nina wasiwasi kuna *element* ya ujasusi. *That is one.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Kamati ya Mheshimiwa Bomani wamemwita huyu katika kulipa kodi ya Shilingi bilioni tano, bado hajakwenda na anasema hakuna mtu yeyote wa kumfanya lolote. Sasa tunapozungumzia suala la mapato ya nchi na raslimali za nchi, na

tunawaachia watu wanachezea uchumi wetu kiasi hiki, halafu maendeleo yanapata 30%, ni aibu! Huyu mtu mmoja peke yake anatakiwa angalau alipe kodi isiyopungua Shilingi bilioni tano au sita, kwa sababu kila wiki anasafirisha *gold* kilo 15 na anafanya *under valuation* katika hiyo *export* yake anayofanya na *yet* Serikali *is not calculating taxes of it.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili tulishughulikie haraka sana tusiliache hata siku moja, kwa sababu huyu jamaa anasema yeye amewamiliki Watanzania wote, atafanya analotaka. Tunataka kuona Bunge hili linadhibiti mali ya Serikali, linawaheshimu Watanzania, anawanyanyasa watu vijijini kule, likomeshwe ndani ya Bunge hili mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, kuna viwanda hapa tayari vinaweza kuzalisha mazao na bidhaa zinazotosheleza bila kuagizwa nje. Viwanda vya *lubricants*, bado kampuni za madini zinaagiza *lubricants* nje lakini viwanda vyetu vya ndani vinaweza kuzalisha na kuuza nje. Hivyo, tungeweza kupunguza urari wa biashara kama makampuni ya madini yangenunua bidhaa hizo hapa nchini. Ninaomba sana, lakini moja ni *Geita Gold Mining* wananunua *lubricant* Dola 500,000 nje, lakini viwanda vyetu hapa vinazalisha *lubricants* za kutosha. Tudhibiti haya ili tupate mapato na tuongeze ajira, tusiwaachie watu wakachezea mali zetu hapa hovyo hovyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, vipo viwanda hapa Tanzania vinazalisha vya kutosha, lakini bado tumeviwekea utaratibu wa kushindana kwa bidhaa hafifu zinazokuja nchini na vijana wetu wanakosa ajira na viwanda vinashindwa kulipa kodi. Hili naomba nalo lisimamiwe.

La tano, tuiombe *NDC* na mashirika ya mifuko ya jamii haraka sana waanzishe kiwanda cha nyuzi katika mikoa inayolima Pamba. Kungoja wahisani wafanye kazi, hakuna. Uchumi wa China unaendelea kwa mashirika ya Serikali. Ni mashirika ya Serikali yanayofanya kibiashara ndiyo yaliyopo hapa Tanzania yanafanya kazi. Tuiambie *NDC* ikaanzishe viwanda vya nguo haraka sana ili tuokoe zao la Pamba. Leo wakulima wa Pamba wamelipwa Sh. 700/=, ni uuaji! Gharama za mzalishaji wa Pamba siyo chini ya Sh. 1,300/=. Unamlipa bei ya Sh. 700/=, ni uuaji. Haiwezekani! Lakini dawa peke yake ni kuwa na viwanda vinavyoweza ku-*process* Pamba tukapata nyuzi na nguo. Hilo linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye *operation* maalum ya viwanda vya Korosho, vinahitaji Dola milioni 60 tu kumaliza matatizo yao. *Let us sit down,* ni kazi ya miezi sita tu hii, tutatua tatizo la bei ya Korosho. Hili suala la risiti na kadhalika *is just wasting of resource*, suala ni ku-*process* mazao tukauza *finished products* ndiyo tutatua matatizo yote lakini hayo mengine yote ni kuongeza hadithi na kuongeza gharama ambazo hazina sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la mipango. Tulipozindua mpango *St. Gasper* na Rais alikuja tukaambiwa mpango ule ni wa mpito. Kwa hiyo, bajeti iliyopita ya mwaka tukaambiwa kwamba huu upo katika *strategy* ya mpito, tukiamini kwamba sasa tutakaporudi tutakuwa tumefanya kazi nzuri zaidi, lakini kwa bahati mbaya, bado tumekuja na tatizo lile lile la kwamba Mpango haukupata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, *performance* ya Serikali siyo nzuri. Ukisoma bajeti yetu utakuta ni 62% ndiyo uwezo wa Serikali wa kutekeleza bajeti yake. Kwa hiyo, hata ukifikia kiwango cha asilimia 35% ya *development,* bado kuna tatizo la uwezo wa kutekeleza. Ni sawa sawa na motto, ana uwezo wa kula nusu kilo, unampelekea kilo moja. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa sana ya kufanya kuisimamia bajeti yenyewe kwamba je, tunao watu wa kuweza kuitekeleza? Ni sawa sawa na fedha inayokwenda kwenye Halmashauri, lakini unakuta watu kwenye Halmashauri hawana uwezo wa kuisimamia hiyo fedha iliyopo. Kwa hiyo, unapeleka hivyo fedha, lakini hupati matokeo.

Sasa wasiwasi wangu ni mmoja kwamba inawezekana Tume pamoja na matatizo yote yaliyokuja, imekuwa *realistic* kwamba hii ndiyo hali halisi tuliyonayo, lakini hata hiyo iliyopo inaweza kutekelezwa? Ndiyo maswali ya msingi yanayoulizwa hapa kwamba mwaka jana tulishindwa kuitekeleza, yaani mwaka huu tunamalizia. Hali yetu ikoje katika utekelezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni kwamba, hebu sasa tujipange. Kamati yetu ya Fedha na Uchumi isimamie na iisaidie Serikali katika utekelezaji wa bajeti. Tuwe na taarifa ya Serikali na taarifa ya Kamati juu ya suala zima la *management* ya bajeti ya nchi. Kuiachia tu Serikali peke yake kila siku tutakuwa tunakuja kupiga hadithi humu ndani. *It is high time* sasa Kamati zetu za Kisekta na Kamati ya Fedha na Uchumi tuisimamie Serikali katika utekelezaji wa miradi yetu, moja, ikiwa ni kusimamia mapato ya Serikali. Mapato ya Serikali hayasimamiwi vizuri na matumizi ya Serikali hayasimamiwi vizuri. Hii kazi ni lazima tuifanye ili kuifanya Serikali iwajibike kikamilifu kwa umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, bahati mbaya Waziri kachelewa sana kuchaguliwa. Mimi nilipomwona Bungeni hapa, mara ya kwanza aliposoma hotuba yake, *I was impressed* kwamba amekuwa *serious* katika kusimamia hiyo kazi. Lakini ukishaumwa na nyoka mara moja, unaogopa. Kuingiliwa kwa Serikali katika bajeti ni mchezo wa kawaida. Tunaomba hilo limalizike ili kuisimamia Serikali.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwongozo Mheshimiwa Msigwa!

**MHE. REV. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Bunge ni chombo cha juu kabisa ambacho wananchi wa Tanzania wanategemea kifanye maamuzi yenye busara na kwa kuwa wananchi wanatuheshimu kama Wabunge, naomba mwongozo wako. Mbunge anaposimama anasema anaunga mkono hoja, halafu katika maelezo yake anapingana kabisa na maneno yake: Je, si kuwahadaa na kuwadanganya wananchi na kulidanganya Bunge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kwanza hata hujaniambia unatumia kanuni namba ngapi. Yaani umejisikia tu kusema hicho ambacho unataka kukisema. Halafu kwa hali halisi ilivyo, kuunga mkono hoja ama kutokuunga mkono hoja hiyo ni hiari ya Mbunge mwenyewe katika jambo hilo analolisema.

Hata wewe Mheshimiwa Msigwa ukilazimishwa kuunga mkono hoja na wewe utakasirika. Sasa na wewe usimlazimishe mtu kutokuunga mkono ama kuunga mkono hoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Msigwa kwa kweli hapo hakuna mwongozo, kanuni hujasema, lakini ulichokifanya ni kueleza yale unayoyapenda yasikike. Huna mwongozo wowote!

Waheshimiwa Wabunge, hakuna mwongozo katika hoja ya Mheshimiwa Msigwa.

Sasa niseme tu kwamba tutakaporudi saa 11.00 jioni tutaendelea na michango ya bajeti hii na tutaendelea kuona Waheshimiwa Wabunge mnashauri nini katika maeneo mbalimbali ili Serikali iweze kutathmini na kwenda kujipanga nayo.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge, tukutane tena saa 11.00 jioni ndani ya Ukumbi huu.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu kama tulivyoanza asubuhi. Naomba niwataje wale ambao tutaanza nao sasa hivi. Tutaanza na Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Moses Machali atafuata na Mheshimiwa Omari Rashid Nundu ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya bajeti. Japo nilikuwa naangalia Kanuni ya ngapi tuone kama *quorum*

inatosha humu ndani, lakini naomba niendelee, wenzangu watatupatia ni Kanuni ya ngapi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee, muda wako unakwisha.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na picha halisi ya bajeti. Naomba niseme moja kwa moja kwamba, kuunga mkono bajeti hii ni kuwasaliti Watanzania ambao wana maisha magumu na wanategemea kupitia kipindi hiki cha bajeti, basi maisha yao yapate unafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti ya Kambi ya Upinzani, na naomba Serikali isisite kuchukua yale mazuri ambayo yameainishwa katika Bajeti yetu Mbadala ambayo imeonyesha dira ya kukomboa hawa Watanzania ambao kupitia bajeti hii ya Serikali sidhani kama wanaweza wakapata matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu bajeti ya Shilingi trilioni 15 ukiangalia mchanganuo wake unaweza ukasikitika na kujiuliza kwamba, ni lini Tanzania tutaendelea? Ni lini Tanzania tutapanga fedha zetu za ndani kwa ajili ya maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti nasema haifai na Wabunge wenzangu bila kujali itikadi za vyama vyovyote vile, ni vizuri tukaungana tukaikataa kwa sababu haiwezekani bajeti ya Shilingi trilioni 15, trilioni mbili tunalipa madeni. Lakini pia mishahara Shilingi trilioni tatu, fedha za matumizi ya kawaida *(OC)* Shilingi trilioni 4.0. Lakini wakati huo, wenzetu wa Mikoa wamepangiwa Shilingi bilioni 49, Halmashauri Shilingi bilioni 704, huko ambako ndiko kuna wananchi wengi, sekta nyingi na mambo mengi yanatekelezwa.

Katika bajeti hii ya Shilingi trilioni 15 wanatengewa Shilingi bilioni 700, ni sawa na Wizara moja tu. Lakini TAMISEMI hiyo Shilingi bilioni 700 kwa ngazi ya Halmashauri, ni fedha ndogo sana! Hawa Watanzania watapataje maendeleo kupitia bajeti hii? Ndiyo maana nilikuwa naifananisha hii bajeti kuwa ni sawa na kuchukua pulizo ukajaza hewa likajaa lakini mle ndani pamejaa hewa tu hakuna cha maana. Shilingi trilioni 15, wakati huo bajeti ya maendeleo imetengwa pesa za ndani Shilingi trilioni mbili, za nje Shilingi trilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui itakuwa ni picha ya namna gani kwa Watanzania wanaotuangalia tukisema tunaunga mkono bajeti hii? Hali halisi hata kwa hizi pesa ambazo zinatengwa, mwaka jana ukiangalia walitenga Shilingi trilioni 4.0 kwa ajili ya pesa za maendeleo lakini hali halisi, fedha hizi zinazotoka nje ambako Serikali inajificha kwamba kuna Wafadhili, kuna Wahisani, ni Shilingi trilioni 1.4 tu ndiyo zilitolewa. Kuna sababu gani ya kuiamini hii bajeti ya Shilingi trilioni 15 wakati hata za mwaka jana zilitoka kidogo? Za Wahisani hao, za maendeleo Shilingi trilioni tatu, zimetoka Shilingi trilioni 1.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatufiki kwa hali hii. Lakini hata hizo pesa za ndani, mwaka jana za maendeleo tulizotenga mwaka wa fedha uliopita Shilingi trilioni 1.8 Serikali ilitoa asilimia nne, fedha za ndani. Shilingi trilioni 1.2 ndiyo zilitolewa asilimia 64. Ndiyo maana nasema, hii bajeti inafanana na pulizo. Tunachukua pulizo, tunajaza upepo tukidhani kwamba kuna *content*, kuna kitu humo ndani tumebeba, lakini tumebeba pesa za *per diem*, za posho za safari za kulipana, maendeleo hayapo.

Ndiyo maana naomba Waheshimiwa Wabunge tuikatae hii bajeti kwa nguvu zetu zote kama tumewawakilisha Watanzania, na wao wanahitaji tuwasemee ili wapate maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei umeathiri Taifa letu, umeathiri kila Mtanzania. Kwenye maelezo haya, mfumuko wa bei umeelezwa kwamba umesababishwa na bei ya vyakula kupanda. Vyakula tu vimesababisha mfumuko wa bei kwa asilimia 24.7, lakini Serikali hii hii inasema kwamba ili kukabiliana na mfumuko wa bei itawekeza katika kilimo. Ukiangalia Sekta ya Kilimo wameitengea Shilingi bilioni 227.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu si utani! Yaani kule ambako unategemea kwamba tutapata ajira na asilimia 70 ya Watanzania wanaishi huko, kwa bajeti ya Shilingi trilioni 15 tunawatengea Shilingi bilioni 200 Sekta ya Kilimo! Lakini wakati huo huo Serikali inashauri kwamba watahakikisha wanawekeza katika mabonde ya Kilombero, tutalima huko mpunga, miwa, ili tuhakikishe kwamba mfumuko huu unakwenda kuondoka katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *implementation* angalia nini kimetengwa kwenye Sekta hii ya Kilimo. Hakuna! Shilingi bilioni 200 ni pesa gani katika Sekta ya Kilimo kwa Watanzania ambao wako katika Sekta hiyo? Ndiyo maana nasema ni vizuri tukajitafakari kama Bunge, tukaacha masuala ya *three whip systems* katika vyama vyetu, tukaangalia ni kwanini tuko hapa? Ni kwa ajili ya Watanzania na si kwa ajili ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri kivuli wa Fedha kutoka Kambi ya Upinzani, asubuhi amesema hapa kwamba, Wizara zaidi ya sita, bajeti zao zilikwama. Nitoe mfano, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu, mpaka hapa Dodoma tunaendelea kuhangaika kwamba hii bajeti haifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukulie mfano kwenye vile vipaumbele Wizara ya Elimu ni ya nne kama sikosei, lakini ukiangalia bajeti ya Wizara ya Elimu ni Shilingi bilioni 700 na kuendelea, bajeti ya maendeleo ni Shilingi bilioni 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni aibu kwa Watanzania kutuona tunapitisha tu fedha za kula, fedha za kulipana safari wakati Walimu kule hawana nyumba za kuishi, huko katika Halmashauri watoto na wanafunzi wetu wanakaa kwenye nyumba za makuti, wanafinyanga udongo na kutengeneza tofali ili watumie kama madawati. Ni aibu kupitisha hii bajeti na ninaendelea kusihi Wabunge wenzangu kwa kweli tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la kusema tunaagiza vyakula kutoka nje ya nchi, mliona mwaka jana mkasema kwamba, ili ku–*control* bei ya Sukari mkatoa maelekezo kwa Wakuu wa Wilaya kwamba kilo ya sukari iwe Sh. 1,700/= na isizidi hapo. Hakuna kilichotekelezwa, lakini pamoja na kuagiza tani 200 za sukari kutoka nje, bado bei ya sukari ikaendelea kupanda ikafika Sh. 2,400/=. Serikali hii itatuambia nini tena? Lugha hiyo hiyo, *chorus* hiyo hiyo, kwamba itadhibiti bei ya sukari, bei ya vyakula! Mimi nasema hapana, na hii bajeti haifai hata kidogo kupitishwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, misamaha ya kodi inaiaibisha nchi yetu. Watanzania hatuwezi kuendelea kuvumilia Serikali ambayo inatoa misamaha ya kodi wakati huo huo Deni la Taifa linakuwa trilioni 22. Mwaka huu tunakwenda kuchukua Shilingi trilioni tano kwa mkopo. Wakati huo huo, juzi mmesikia utafiti kwamba, Mashirika na Taasisi za Dini wamefanya utafiti na kugundua kwamba misamaha ya kodi tu kwa mwaka jana ilikuwa ni Shilingi trilioni 1.7. Hii ni zaidi ya bajeti za Wizara tano. Hii ni aibu na ni vizuri Serikali ikafungua macho ikaangalia bajeti mbadala ambayo Kambi ya Upinzani tumeitoa kuliko kung'ang'ania vitu ambavyo havitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie hata Halmashauri zetu, zile fedha zinazokusanywa. Mwaka jana Halmashauri walipangiwa wakusanye Shilingi bilioni 350.5, lakini mwaka huu wamepangiwa wakusanye Shilingi bilioni 362, wakati mwaka jana tu mpaka Aprili mwaka huu wa fedha unaomalizikia, wamekusanya Shilingi bilioni 143 ambayo ni asilimia 40.8 ambazo Halmashauri ndiyo wamekusanya. Serikali badala ya kuona kwamba wapunguze wigo huu na waachie watu kile ambacho wanaweza kukusanya au waangalie kwanini hawakusanyi, wao wanapuliza pulizo Shilingi trilioni 15. Bajeti haitekelezeki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haikubaliki. Hii bajeti inawezekana mmeandaa kwa zimamoto, ni bajeti ambayo haijaweza kuangaliwa kwa karibu. Naomba muiangalie kwa karibu, hatuwezi tukapitisha bajeti kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata zile kodi kwenye ngazi za Halmashauri wameachiwa mawakala. Mawakala wanajichukulia fedha wanavyojua wao. Tumepewa mwongozo katika kitabu hiki cha bajeti kwa Wafanyabiashara kwamba, mfanyabiashara ambaye mauzo yake

hayazidi Shilingi milioni 14 kwa mwaka, alipe kodi Sh. 575,000/=. Lakini ukienda kwenye ngazi za Halmashauri kinachofanyika ni kitu kingine. Kuna Wafanyabiashara hapa wameandikiwa wachangie Shilingi milioni 2.4. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, muda wako umekwisha. Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Moses Machali, na Mheshimiwa Omar Nundu ajiandae.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia katika hoja ya bajeti iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa naomba niseme, siungi mkono bajeti ya Serikali ambayo imetangulizwa, na ambayo iliwasilishwa na Waziri wa Fedha *last week*. Sababu za kutokuiunga mkono; moja, ni kwa sababu sina imani kwamba Serikali itaweza kutekeleza bajeti hiyo. Lakini sababu ya pili ni kulingana na aina ya uongozi ambao tunao ndani ya Serikali yetu, sina imani na baadhi ya Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, ukijaribu kuangalia, bajeti leo inakuja *figure* ya Shilingi trilioni 15 kama bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013. Serikali inaliomba Bunge hili liweze kupitisha bajeti kama ilivyofanyika mwaka jana wakati inaelewa fika kabisa kwamba ukienda kwenye Wizara mbalimbali bajeti ya mwaka jana ilikuwa ni changa la macho kama Mheshimiwa Kigwangala alivyozungumza *last time*. Haiingii akilini!

**MWENYEKITI:** Naomba ufute neno changa la macho.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tafsiri. Ninamaanisha nini ninaposema changa la macho? Kwa sababu fasihi ni dhana ambayo ni pana. Kwanini ninasema ni changa la macho? Ni changa la macho kwa sababu tunadanganyana mahali hapa na ninasimamia kauli yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Ukijaribu kuangalia Wizara tatu ambazo tunasimamia, na tumekuwa tukishughulika nazo, inasikitisha na kufedhehesha sana, na wakati mwingine sioni sababu ya sisi Wabunge kuendelea kukaa mahali hapa. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia hadi mwezi Mei, Bajeti ya Serikali ambayo ilipitishwa mwaka jana ilikuwa imetekelezwa kwa takribani asilimia 29.7. Hapa tunachezeana! Tunategemea kwamba Wizara watafanya kitu gani? Katika bajeti hiyo, asilimia nane kati ya asilimia 38 ndiyo fedha za Miradi ya Maendeleo zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Wizara hiyo. Sasa tunakuja mahali hapa, halafu tunasema tunapitisha bajeti hii: Kwa misingi gani? Ni fursa ya kusema hapana kila mahali pa kuweza kusema hapana kwa maslahi na mustakabali wa maisha ya Watanzania. *(Makosi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Wizara ya Uchukuzi ambayo ukiangalia kwa sehemu kubwa inawezekana ndiyo Wizara ambayo ina sekta ambazo ni mtambuka kwa ajili ya uchumi wetu. Mwaka jana walitengewa fedha za Miradi ya Maendeleo takribani Shilingi bilioni 262. Mwaka huu Serikali inakuja kuomba kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Wizara ya Uchukuzi, takribani Shilingi bilioni 252 ambapo kumepunguzwa zaidi ya Shilingi bilioni 10 . Mlituambia hapa mwaka jana kwamba mtahakikisha hali ya reli inarudi katika hali iliyokuwepo miaka ya 80 na 90. Leo tunapiga kelele kwamba Bandarini kumesheheni mzigo mkubwa na hata watu wengine wanakimbia kuweza kupitisha mizigo yao kwenye Bandari ya Dar es Salaam kwa sababu kui-*shift* mizigo pale kwenda mahali, mingine haiwezekani. Tunakuja hapa tunasema kwamba tuunge mkono bajeti hii: Kwa misingi gani kama hatutaki laana kutoka kwa Mwenyezi Mungu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, NCCR - Mageuzi tunasema daima hatutakubali kuunga mkono bajeti ambazo hazina mwelekeo na daima mambo yanakuwa ni yale yale. Ni lazima tufikirie, na ni lazima tuseme. Naiomba Serikali wakati wa kuhitimisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha atueleze ni sababu gani ambazo zimepelekea fedha ambazo zilitengwa mwaka jana, 2011 hasa za Miradi ya Maendeleo zisiweze kutolewa? La sivyo ,Waheshimiwa Wabunge mkipitisha bajeti hii, basi wale ambao wamekuwa hasa upande wa pili, chonde chonde, hakuna sababu ya kuponda halafu

mwisho unasema: “Naunga mkono hoja.” Tunafanya vitu gani? Watanzania wanatuona, Watanzania wa leo siyo Watanzania wa jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuangalia, kuna misamaha chungu nzima ya kodi. Serikali inapoteza mapato makubwa sana. Serikali inapoteza fedha nyingi sana hasa kwenye hizi *multinational companies* ambazo zimekuwa ziki-*deal* na masuala ya madini na chanzo cha yote hayo ni sheria mbovu tulizonazo. Serikali hamwoni sababu ya kuweza kuhakikisha kwamba imefika fursa ya kuleta Muswada hapa Bungeni ili kusudi turekebishe Sheria ambazo zimekuwa zinawapa baadhi ya watu uwezo wa kutoa *tax exemptions* kwenye makampuni ambayo yamekuwa yanasababisha Serikali ipoteze pato kubwa sana, na matokeo yake tunajikuta utekelezaji wa programu mbalimbali ambazo Serikali imekusudia hatuzipati.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba utusaidie, tunajua kwamba pale *TRA* kuna watu ambao kwa mujibu wa sheria wamepewa mamlaka ya kutoa *tax exemptions.* Ni lini mtaleta *amendment* ili kusudi tuweze kupunguza mianya ya kuwasamehe watu kodi ili *deal* ziache kupigwa na Serikali kupoteza fedha nyingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadhi ya watu wanasema *east, west*, *home is best.* Narudi kwanza nyumbani kwetu Kigoma.

Mheshimiwa Mwenhekiti, nimesema siungi mkono bajeti hii kwa sababu sina imani na baadhi ya viongozi wa Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi (CCM). Juzi taarifa za *CAG* zimebainisha ubadhirifu mkubwa sana wa fedha. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu nayo ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zinakabiliwa na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka nilichokifanya, nili-*request* taarifa kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Hakunipa taarifa, nikafuatilia nikaamua kumwandikia Mkuu wa Polisi wa Wilaya *(OCD)* amkamate na kumfungulia mashitaka kwa kosa la ku-*abuse power*. Lakini nakutana na Waziri mmoja mwenye dhamana ya TAMISEMI anakuja kunieleza kwamba, eti tena anamwambia Mheshimiwa Waziri mwingine pembeni yake, huyu amemwomba *OCD* amkamate Mkurugenzi. Ebo! Sasa nikajiuliza kwamba tatizo ni nini? Kama mtu ume-*commit crime* unategemea tukufanye nini? Kama Mawaziri ndio ambao wamekuwa wanawalinda watu ambao wameonekana wakati mwingine wana matatizo wanasababisha *serious problems* kwenye Halmashauri halafu wao wanapopata taarifa wanawatetea hapa, ndipo ambapo imani yangu na Serikali hii, sioni jipya ambalo mtalifanya katika bajeti hii.

Namwomba mama yangu, Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa sababu nilimwandikia nikamwomba, naomba unieleze hivi, ulikuwa *serious* ulichokuwa unaniambia au ulikuwa unatania? Inaonekana moja kwa moja ninam-*term* na kumtuhumu kabisa kwamba yeye atakuwa ni chanzo cha kuwalinda watu katika Halmashauri zetu na matokeo yake matumizi mabaya ya fedha yataendelea ku-*exist* kwa sababu ameonyesha wazi kabisa kwa kunieleza, siyo kwamba nimeambiwa. Anakuja kuniuliza kitu ambacho binafsi ninaomba niseme kwamba, mtu yeyote mwenye kukudharau atakwambia kitu cha kijinga akiamini kwamba hujui. Anataka kunifanya mjinga! Mimi sio mjinga! Nina uelewa wangu timamu na nina shule yangu nzuri tu na ninaweza nikafanya *analysis* katika vitu vingi hapa*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, chonde chonde watu wote ambao wana tabia ambayo inakera kama ya mama yangu, dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia, kuanzia leo i-*stop.* Kama mnataka tuheshimiane, ni lazima tuambiane vitu ambavyo vinakuwa na tija kwetu. Tunawaheshimu sana kwa umri wenu pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina imani na Serikali. Hii bajeti Waheshimiwa Wabunge naomba tusiiunge mkono kwa sababu hata bajeti mbili ambazo zimetangulia hapo nyuma utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua. Fedha hazijakwenda kwenye Wizara nyingi, ndiyo maana Wizara ya Elimu, Kamati zimezuia kupitisha bajeti kwenye *level* ya Kamati. Kwa hiyo, ukijaribu kuangalia ni kiashiria kabisa kwamba bajeti hii pia itaendelea kuwa vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho nilikuwa napitia taarifa moja ambayo imeandaliwa na *Policy Forum Tanzania,* wameonyesha kwa kutumia vigezo vya kiuchumi tatizo ambalo linalikabili Taifa la Tanzania la kifedha, lita-*exist* hadi mwishoni mwa mwaka 2012 na hata baada ya mwaka 2015. Kwa hiyo, hebu mkae na pengine mpitie taarifa hizi mje mtuone, tutawaelekeza mwone mnafanyaje? Vinginevyo....

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Omari Nundu, na Mheshimiwa Amina Makilagi atafuatia na halafu Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran ajiandae.

**MHE. OMARI RASHID NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika mjadala unaoendelea. Awali ya yote, naomba kuanza kuisifu Serikali kwa kazi ambayo wameifanya mwaka uliopita, ya kuweka mpango, bajeti, halafu kujaribu kuitekeleza bajeti hiyo. Ni kweli katika utekelezaji, kuna mambo mengi yamejitokeza na mambo haya yameainishwa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na mengi ambayo wameyasema kule, nakubaliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa wakati tulionao ukiangalia mazingira ambayo yametuzunguka ya ushindani, ukiangalia jinsi nchi ambazo zinakwenda mbele, bajeti ambayo tunatakiwa tuwe nayo hapa ni lazima kwa kiwango kikubwa iwe inashughulikia maendeleo. Mwaka jana Serikali kwa ridhaa ya Bunge iliweka asilimia 35 kwenda kwenye maendeleo, lakini hatukufikia hivyo na mwaka huu wamerudisha kwenye asilimia 30. Ombi langu ni kuwa, tujaribu kupeleka sio kwenye asilimia 35, lakini ikiwezekana hata kwenye asilimia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Nchi ambazo tunapewa mifano ya kuwa zimeendelea zikiwemo Malaysia, Korea na Singapore ilifika wakati ni lazima watu wasamehe vitu na kwenda mbele. Ukitoa mfano wa Korea Kusini, ilifika wakati akina mama waliweka rehani hata pete zao za ndoa ili nchi iende mbele. Hatutaki kwenda huko, lakini tulivyonavyo ambavyo tunaweza kujibana kama ambavyo Serikali imesema, itabidi tujibane kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye matumizi tunapotumia fedha kwa safari, natoa mfano mmoja tu au kwa posho ambazo hata ukilinganisha na zile za Umoja wa Kimataifa ni kubwa sana. Halafu hapo hapo, tunarudi tunawaambia wafanyabiashara wadogo wadogo wakikusanya *revenue* na si faida, Shilingi milioni tatu zikipita kidogo, waanze kulipa kodi. Inakuwa uwiano wa nani anajitolea, hauko sawasawa. Hatua tuliyofika inabidi sote tujitoletee, sote tukaze mkanda, twende mbele. Kwa hiyo, tungependa kabisa Serikali ionyeshe waziwazi ni sehemu gani za matumizi ambazo wanazifanyia kazi? Mimi ningetaja moja kwa moja *per diem* za Dola 500 ambazo mtu akisafiri kwa siku nne tayari ana Dola 2,000/=. Hizo zingefanyiwa kazi zikarudi kwenye *per diem* za Kimataifa na zirudi katika mfumo wa zamani ambapo kule unakokwenda kunatathminiwa na kuonekana ulipwe *per diem* kiasi gani. Hayumkini leo ukienda Nairobi ulipwe *per diem* kama ambayo umekwenda *New York*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetajwa hapa Taasisi za Mashirika ya Umma kuchangia bajeti; Taasisi zinachangia kutokana na mapato yao. Serikali iangalie mapato ya Taasisi hizo zinavyotumika. Hayumkini katika Tanzania hii iwe katika Taasisi moja, Mkurugenzi Mkuu alipwe mshahara ambao ni sawasawa na mshahara wa kima cha chini ya Watanzania wengine mia moja, haviendi sawa. Kwa hiyo Wizara ya Fedha ningeomba sana, walitathmini hilo na waangalie uwiano wa mishahara katika Taasisi zetu na ndani ya Taasisi zenyewe ili hii tofauti kubwa isiwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Serikali ilisema ingejikita sana kwenye kuvutia wawekezaji na Sheria ya *PPP* hapa ilipitishwa Julai, 2010. Huu ni mwaka wa pili sasa. Hapa tunachosikia ni kuwa, bado kuna kazi zinafanyika ili Sheria hiyo ya *PPP* ipitike na tunaambiwa kutakuwa na majaribio. Siyo kwamba tunakwenda kwa dhati kuweka ni miradi gani iingie kwenye *PPP*, lakini tunakwenda kwa majaribio. Sheria ya *PPP* yenyewe ukiiangalia huko nilikokuwa, tulifanya tathmini Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam kazi ambayo tunatakiwa kuifanya. Ukiifuatilia Sheria ya *PPP* mpaka miaka mitatu inapita hujafanya chochote, hatuwezi kwenda kwa *speed* hiyo. Tukienda hivyo, wenzetu Mombasa wanajengwa bandari mpya, *Mozambique*

wanajenga bandari upya, sisi miaka mitatu tunapita tu katika mlolongo wa kufikia mahali ambapo tutaitumia *PPP;* hatuwezi kwenda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kuwa, uharaka wa utumikaji wa *PPP* ufanyiwe kazi, ule mlolongo wa tathmini na mlolongo wa kanuni na sheria na mlolongo wa haki zinazotakiwa zitendeke ili *PPP* ifanyiwe kazi, uondolewe. Tuondoe vikwazo vyote ambavyo vitawakatisha tamaa wawekezaji ambao tunawaita kuja kuwekeza kwenye nchi yetu. Papo hapo tuwatie tashwishwi Watanzania, kuna miradi ambayo ninaamini kabisa kwa Watanzania wenyewe wakianza *special vehicle purposes* miradi hiyo itaweza kufanywa na fedha za Watanzania na tija inayopatikana ipatikane humu ndani ya Tanzania na ni miradi ambayo ina tija kubwa sana. Kwa hilo pia tungelifikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuchangia lilichangiwa wakati wa Bunge lililopita ni lile la kilimo. Kilimo kinaweza kuleta mapinduzi ya viwanda nchini kwetu. Lakini ili hili litokee ni lazima uangalie kilimo kwa ncha mbili. Uangalie mapinduzi ya viwanda kabla ya ukulima na mapinduzi ya viwanda baada ya ukulima. Mara nyingi tunavyoongelea ni mapinduzi ya viwanda baada ya kulima. Tu-*process* vyakula, tutengeneze nyuzi kabla wakulima hatujalifanyia kazi. Bado mpaka leo tunaagiza matrekta kutoka nje na yamekaa jirani hapo hayafanyi kazi mpaka sasa na tunajisifu kuwa tunataka tuweze kutoa nafuu ya kuleta pembejeo hizo. Ni vizuri tukalifikiria kwa makini sana hilo ili pembejeo zikatengenezwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewekeza sana kwa wataalamu nchi hii. Tuna wataalamu Wahandisi waliobobea takriban 8,000 lakini mpaka leo baiskeli pia tunaletewa za kuoza kutoka Uchina. Hii ni aibu. Hawa wataalamu wanatakiwa wawezeshwe. Kwa wenzetu ukienda Canada; kwa mfano, kijana akimaliza Chuo Kikuu, Mhandisi anakopeshwa Dola 15,000 kuweza kujiendeleza. Hapa, hilo halitendeki. Naona Serikali imefanya juhudi kuanzisha Benki za kuwakopesha watu mbalimbali, lakini kikundi hiki ambacho tayari kina uwezo, kinachohitaji ni kuwezeshwa kiende mbele, hakijafanyiwa kazi.

Sasa kama hakutatengwa Kitengo Maalum cha kuwashughulikia hawa, nadhani Mfuko kama huo imefika wakati ambao itabidi tuuanzishe. Hawa sio kuwa tu watajiajiri wenyewe, wataajiri wenzao, watatengeneza nyenzo hapa ambazo tunazihitaji kwa shughuli mbalimbali. Nchi hii haiwezi kuendelea kwa kutegemea kuagiza kila kitu kutoka nje. Umefika wakati sasa *SIDO* ambayo tumeianzisha, na tunaishukuru sana Serikali kwa kufanya hivyo na wataalamu hawa niliowataja wapewe uwezo wa kufanya hivyo. Nimetaja wataalamu Wahandisi tu, kwa sababu ndio ambao nimekutana nao muda mwingi, lakini kuna wengi wengine Wafamasia, ukienda nchi za jirani za wenzetu kama Uganda unakuta kule wanatengeneza madawa wenyewe, mengi tu. Hapa Tanzania naambiwa kuna Wafamasia wakubwa watatu tu, hatuwezi kwenda hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu sio wakati wa malumbano, na huu sio wakati wa kampeni, nawaomba Wabunge wenzangu wote tuiangalie bajeti iliyoletwa na Serikali kwa upeo chanya, tuone pale ambapo panahitaji kurekebishwa parekebishwe. Tukiendelea kulumbana, tutalumbana mpaka jua litazama, hatutakwenda popote. Tuboreshe bajeti, twende mbele. Niliyoyasema na mengi nitayaweka kwenye maandishi, nitaiomba Serikali iyafanyie kazi katika kipindi kijacho. Kazi tuliyonayo sasa hivi ni kuangalia hiki tulichonacho tunakiboresha vipi ili tuanze kupiga hatua. Nchi zinakwenda mbele, hatuko peke yetu. Mifano ya nchi ambazo zimetuzunguka, na zinafanya bidii ya kutupiku sisi kwenda mbele, ni nyingi. Hatuwezi tukabaki tunalumbana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Amina Makilagi na Mheshimiwa Mansoor Sanifu Hiran na Prof. Kulikoleya Kahigi wajiandae.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo katika hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, naomba niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika Bunge letu hili Tukufu. Vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa

Rais kwa kuwateua Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa ajili ya kuongoza Wizara hii nyeti kwa mustakabali wa Taifa letu la Tanzania. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ametambua uwezo wa akinamama na ameweza kuwateua Manaibu Waziri wote wanawake. Pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na timu yake yote kwa kuandaa bajeti nzuri iliyolenga kuwakomboa Watanzania na hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba nianze kusema kabisa kwamba mimi Amina Nassor Makilagi, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja kwa sababu bajeti hii inalenga kuwakomboa Watanzania, hasa wanawake, vijana na wazee. Mara baada ya pongezi hizo, naomba sasa nitoe ushauri wa mambo kadhaa ambao nimeyaona ambayo Serikali inatakiwa kuyafanyia kazi.

Jambo la kwanza, pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali yetu ya kuhakikisha inakusanya mapato, maana ukiangalia kwa mujibu wa taarifa tuliyopewa, kazi nzuri imefanyika ya kukusanya mapato. Lakini nilichokigundua hapa, bado inahitajika kuongezeka kasi kwa sababu baadhi ya Watanzania bado wanakwepa kodi. Mfano, kuna watu wanaagiza magari nje ya nchi, anapofikisha hapa Tanzania anashusha thamani na kwa sababu huyu mnunuaji wa gari anakula na baadhi ya Watendaji ambao sio waaminifu, anakadiriwa kiwango cha chini na hivyo kupoteza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wapo baadhi ya Watendaji wachache katika Serikali yetu ambao Serikali imewaamini na kuwakabidhi dhamana ya kukusanya mapato. Badala ya kukusanya mapato na kuyafikisha katika Mfuko wa Taifa, mapato yale wanayaingiza katika mifuko yao. Nafikiri sasa umefika wakati Serikali iwe macho na iwe makini ihakikishe inawafuatilia Watendaji wa aina hiyo na kuwachukulia hatua zinazostahili na katika maeneo hayo yenye matatizo ni maeneo ya bandari na maeneo ya viwanja vya ndege na maeneo ya mipakani. Kuna matatizo makubwa sana, baadhi ya Watendaji ambao tunawaamini tumewakabidhi dhamana, wamekuwa sio waaminifu kwa Serikali yao. Naomba Serikali ifanye utafiti wa kina na ichukue hatua kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulichangia, naomba Serikali ichukue hatua kwa baadhi ya Watendaji wetu ambao pia tumewakabidhi dhamana ambao wao wanakula na wafanyabiashara wakubwa na hata wadogo. Unamkuta Amina Nassor Makilagi anao mradi na anayo biashara, kwa mujibu wa taratibu alipaswa alipe kodi ya Shilingi pengine milioni 100, lakini kwa sababu ya ubinafsi wa baadhi ya Watendaji wetu, anakadiriwa kiwango cha chini. Alipaswa kulipwa Shilingi bilioni 100, analipa Shilingi milioni 10, matokeo yake Serikali inapoteza mapato yake yaliyo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba sana Serikali, pamoja na kazi nzuri sana inayoifanya ya kukusanya mapato, lakini naishauri iendelee kuongeza vyanzo vipya vya mapato. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameainisha vizuri sana, mimi nasema bado havitoshi tuendelee kuangalia katika maeneo mengine. Mfano, katika majengo, unakuta kuna mtu ana nyumba yake analipwa kodi na wapangaji wake pengine kwa mwaka Shilingi milioni 12, lakini hana anachokilipa kwa Serikali. Majengo yako katika nchi hii, wanakusanya kodi, lakini Serikali hakuna inachokipata. Nilikuwa nafikiri hiki ni chanzo kizima cha mapato. Ni vizuri Serikali iangalie na kuhakikisha inaweza kuongeza mapato katika maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nitakalochangia katika bajeti hii, tumefurahi sana kuona bajeti ya mwaka huu pia imelenga kuhakikisha kilimo chetu hiki kinaleta tija kwa Watanzania. Lakini na mimi naomba niendelee kutoa masikitiko yangu kwamba katika fedha zilizotengwa katika Sekta ya Kilimo, bado hazitoshelezi. Nilikuwa naomba pamoja na hizi ziada zilizowekwa na hizi fedha zilizotengwa, ni vizuri Serikali pia ikaangalia uwezekano wa kuongeza fedha katika Sekta ya Kilimo na hasa katika kilimo cha umwagiliaji. Nimefurahishwa sana na mpango uliokuwepo wa kuinua kilimo katika ule ukanda wa Nyanda za Juu Kusini.

Mhesimiwa Mwenyekiti, Nyanda za Juu Kusini haiwezi kutosheleza mahitaji ya Tanzania nzima. Lakini kuna Ukanda wa Ziwa na Ukanda wa Kati, nilikuwa nashauri tuongeze uwezo katika hii Sekta ya Kilimo na tuongeze fedha ili kutumia mito yetu ile ya Mara, Kagera, Simiyu na

wananchi wa Kanda ya Ziwa waweze kulima kilimo cha kutosha na waweze kujitosheleza kwa chakula na vilevile kusaidia katika Mikoa ya Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka niishauri Serikali katika msukosuko huu wa hali ngumu ya uchumi. Ni vizuri Serikali ingejielekeza katika kufidia utaratibu wa kubana matumizi, maana huwezi ukazungumza kwamba hali ya uchumi ni mbaya, na sio Tanzania peke yake, ni nchi nzima, halafu Serikali inaendelea kutumia sana. Watendaji wetu, zile ambazo hazina tija, hebu tuzipunguze. Lakini nilikuwa nashauri, kuna kodi za pango za nyumba za Watendaji wetu, Serikali inaingia gharama ya kulipa kwa mfano hapa Dodoma kuna nyumba za Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali na Wakurugenzi mbalimbali zipo hapa Dodoma, lakini wanazitumia tu mara wanapokuja kwenye kipindi cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaonaje tukarekebisha kwamba badala ya Serikali kuwa inamlipia nyumba Dar es Salaam, inamlipia Dodoma, nyumba ambayo haikai kwa mwaka mzima Serikali ingeangalia utaratibu wa kuiacha ile nyumba ya Dodoma ikae inamlipia ya Dar es Salaam na hiyo fedha ikaunganishwa ikaingizwa katika kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Tanzania hauwezi kukua kama viwanda vyetu vya ndani hatujaviimarisha. Nimefurahishwa sana na mpango uliopo, lakini naishauri sana Serikali hebu ijaribu kuangalia sasa hivi viwanda vya kubangua korosho, viwanda vya kuzalisha pamba, vya kuchambua pamba ambavyo kwa dhamira nzuri ya Serikali tuliwapa watu wanaoitwa wawekezaji wa ndani. Kwa bahati mbaya sana viwanda hivi havifanyi kazi. Nilikuwa nashauri Serikali kwamba sasa umefika wakati kuviangalia vizuri sana viwanda vyetu, kuangalia wale waliopewa kama wanaviendesha ipasavyo na kama hawaviendeshi ipasavyo virejeshwe ndani ya Serikali na Serikali iwatafute Watanzania wengine walio tayari kuendeleza viwanda hivi kwa ajili ya manufaa ya Tanzania. Viwanda hivi viko vingi, mfano pale Kibaha kuna kiwanda, kule Mtwara kuna baadhi ya viwanda, imefika wakati nafikiri virudi kwa Watanzania walio tayari kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nishauri katika bajeti hii, nimeona Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kuweka misamaha katika baadhi ya maeneo kadhaa katika bajeti hii. Nilikuwa naona jambo nyeti sana limesahaulika. Nashauri tuliongeze hilo eneo. Kuna kodi ya madawa ya maji, hii ni kero kubwa sana. Mamlaka za Maji nchini zinashindwa kununua madawa kwa ajili ya maji kwa sababu kodi yake ni kubwa. Baadhi ya Mamlaka za Maji kwa sababu kodi ya maji ni kubwa, matokeo yake sasa wanaamua kuwapa wananchi maji yasiyo safi na salama. Nilikuwa naomba hebu na hii kodi ya maji tuiangalie na sio kodi ya maji peke yake, vilevile tuangalie pia na kodi ya mazao, hasa mazao ya mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia katika bajeti hii, naomba niungane na Wajumbe wenzangu badala ya kuongeza fedha katika watumiaji wa simu, hebu tuongeze fedha katika Makampuni ya Simu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo ajiandae na Mheshimiwa John Momose Cheyo atafuatia.

Basi naomba nimwite Mheshimiwa Mussa Haji Kombo kwa sababu Mheshimiwa Prof. Kulikoyela amesema atachangia kesho.

**MHE. JOHN. M. CHEYO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niende moja kwa moja kwenye Bajeti. Mimi naona mpaka hivi sasa tangu tumeanza Kamati na sasa tunazungumza Bajeti hii tunazungumzia matatizo, tunazungumza kutopata pesa, tunazungumza miradi kutofanya kazi na kushindwa kwa Serikali, kuweza kuendeleza na kuwapa wananchi maendeleo ambayo wanayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tatizo kubwa ambalo lazima tuanze kulishughulikia sasa hivi ni mfumo wetu wa namna ya kuwa na Bajeti. Bajeti za siku hizi ambazo ndiyo mchakato wa karibu dunia nzima ni *participatory*, yaani watu washirikishwe na zaidi Bunge hili lishirikishwe. Lakini Bajeti sasa hivi tunaanza mwezi wa Nne, hatujui vitabu viko wapi, hatujui Serikali ina mkakati gani, mwishoni tunaanza kukutana hapa na manamba tu ambayo mwisho wa mwaka hayatekelezeki

na Waziri wa Fedha amesema wazi kabisa kwamba miradi ambayo haitekelezeki ni Miradi ya Maendeleo ambayo ametuambia ni kama asilimia 47 tu ambayo imeweza kutekelezeka. Kwa kuangalia mfumo wa Bajeti hii tunakokwenda ni mambo hayo hayo.

Sasa Bunge hili litakuwa linakutana hapa kila siku linatengeneza namba, linawaambia wananchi tutawapa hivi, tutawapa maji na mwisho wa safari ni kidogo tu ambacho kinatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kama tulivyokaa kule Bagamoyo Waheshimiwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti, basi mfumo mpya uanze ili bajeti hii, badala ya kumalizika mwezi Septemba au Agosti, tuanze mapema mwezi Aprili ili tuzungumze Bajeti vizuri, tunapofika tarehe 1 Julai, mambo yote yamekamilika na kila mmoja anapewa ruhusa ya kwenda kukusanya pesa na pia kuanza kutumia fedha. *This is the best practise.* Kwa hiyo, tusiendelee tu na utaratibu wa miaka yote ile ambayo babu zetu walipitisha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni Pamba. Nimefurahi sana kuona kwamba hata Ndugu yangu Chief Chenge na Mheshimiwa Ndassa wamesema, bila Sh. 1,000/= hakuna Pamba na huo ndiyo utaratibu. Hakuna buku hakuna Pamba. Hatuwezi kuendelea kuwa na watu takribani milioni 16 ambao kazi yao ni kubeba kila mtu. Ukitaka kura, unakwenda kwenye wakulima wa Pamba, wanakubeba wanakufanya Rais. Ukitaka kuwa Mbunge unakwenda kule wanakubeba unakuwa Mbunge, ukitaka kuwa tajiri unakwenda kwa wakulima wa Pamba, bei ya juu ikiharibika, wenyewe ndiyo wanakubeba. Wewe wewe ukiwa msindikaji wa mafuta, unapata pesa na yeye anazidi kupata hasara. Sisi ndiyo Wawakilishi wa wakulima. Duka letu ni Pamba. Unataka pamba, lete buku, huna buku nenda ukakae kule na sisi tutaangalia, Pamba yetu haiozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inaweza kutusaidia kwa mambo mbalimbali. Kwanza, kuhakikisha kwamba viwanda vyote vile ambavyo vinashirikiana na Pamba, kiwe kiwanda cha kusindika mafuta, kiwe cha kuchambua Pamba, kiwe *textile* na mambo kama hayo, zinakuwa na upendeleo wa kodi. Watu wa madini tunawapendelea na kwa hili la madini namwambia Waziri mpya tutakwenda Mahakamani. Hatuwezi kuwa na makampuni katika nchi hii ambayo yapo juu ya Sheria, kwamba tunaweza kuwabana watu wote kwa kodi. Tunaweza kuchukua kodi kwenye sigara na vinywaji, lakini tukifika kwa *special baby* 'madini', hapana. Hii haiwezekani! Hizi *MDA's* ni *unconstitutional*. Haziendani kabisa! Kwa hiyo, nashauri Serikali itulinde kwa upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inaweza kutulinda kwa kuidhibiti Bodi ya Pamba. Bodi ya Pamba inatuletea Sheria nyingi mno. Mara kilimo cha mkataba, mara tunaambiwa lazima tulime mbegu fulani kwa bei ya Sh. 1,400/=, mimi sijaona hilo. Kama kuna Mzungu ambaye anataka kutengeneza mbegu kule Kanda ya Ziwa, mbona kuna watu wengine ambao wanatengeneza mbegu za mahindi wana-*promote* wao wenyewe na hakuna Serikali ambayo inaweka mkono wake kwamba lazima hii mbegu inunuliwe. Huu utaratibu Serikali inaweza kutusaidia. Nina hakika kwamba Serikali isiendeleze huu utaratibu wa wanunuzi wa Pamba kukaa na kuweza ku-*fix* bei. Sasa hivi wako Mwanza wanajadiliana mkulima yuko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ka-*group* kadogo tu ka wakulima ambako kako kule. Mimi naona iwe *open market* ambayo mwanzo wake unasemwa na Serikali kwamba msimu utaanza tarehe fulani, lakini iachiwe. Kusiwe na kikomo cha msimu. Kama kuna msimu ambao unaweza kuendelea mpaka Oktoba, uendelee tu, labda katika kuendelea kule, bei itaweza kupanda. Kwa hiyo, hiyo watusaidie tusiwe na Bodi ambayo ni ya kutengeneza Sheria tu. Tuwe na Bodi inayosaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye Bajeti. Tatizo mojawapo ambalo tupo nalo kwenye Bajeti ni *transparency* au uwazi. Sasa Mheshimiwa Waziri umepanga hela nyingi kwa ajili ya maendeleo, kama barabara, lakini hujatuambia madeni uliyonayo katika miradi hiyo ya maendeleo ni kiasi gani? Mwaka jana tulipanga hapa trilioni moja kwa ajili ya barabara. Mpaka Februari, sisi Kamati ya *PAC* tulipoangalia tulikuwa tumepata Shilingi milioni 374 tu na Shilingi milioni 420 ilikuwa ni madeni. Sasa madeni ya *certificate* za hii miradi ni kiasi gani? Kwanini Serikali haituambii walimu wanatudai Shilingi bilioni 48, sijui nani anatudai hiki, ili tunapopitisha bajeti

tunaona kweli kule tunakokwenda ni mbele kuliko kurudi nyuma? Kuliko sisi kupitisha hapa Bajeti ambayo kazi yake ni kulipa madeni tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwanini hamtupi matumaini? Sasa hivi tuna gesi, mbona Mheshimiwa Waziri hamjatuambia kwamba jamani angalau tumeona *a little light in the tunnel?* Tutakapokuwa na gesi tutapata mapato kiasi hiki na hili liletwe Bungeni. Mimi najua kwamba kuna baadhi ya watu ambao wamepata gesi, kama vile *Mnazi Bay* pale wanailipa Serikali asilimia 70 ya mapato. Hatuzungumzii faida. Sasa kwanini hatuambiwi hilo? Najua kuna *British Gas* ambayo imepata gesi nyingi sana. Yenyewe imeambiwa sijui ni *fifty fifity.* Kwanini iwe *fifty fifty* na huku iwe asilimia 70?

Kwa hiyo, nasema, Serikali yetu tumeiachia huru mno. Kwa kuikaba Serikali hii ambayo inatufikisha mahali ambapo wanapokuwa wametengeneza mikataba yao wameibana Serikali, sisi ndiyo kwamba hatuna vyanzo vya mapato. Kumbe vyanzo vya mapato tunavitupa njiani. Tunataka sasa mikataba yote ya gesi iletwe hapa Bungeni tuelewe ninyi mnatarajia kitu gani kabla haijafungwa na utaratibu huu wa kuiachia Serikali kila kitu ifanye, umepitwa na wakati. Hii ni *participatory*. Nchi hii ikianguka, ni sisi wote tumeanguka. Kwa hiyo, tunataka sasa Serikali muamini Bunge lenu, ili mhakikishe kwamba mnaleta mambo haya na kila mmoja wetu anaweza kufahamu. Juzi hapa tumesema mambo ya *TBS* yanachukua karibu Dola milioni kumi. Leo nimeona kwenye matangazo inaendelea tu. Ukisitisha na kufanya huu ukaguzi hapa utapata mapato ya zaidi ya Shilingi bilioni 15 ambayo wewe unaweza kuendesha sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoshauri, Serikali iwe wazi zaidi na ikiwa wazi zaidi, mimi nina hakika mambo mengi tutaweza kuyasawazisha ili tuhakikishe kwamba, kweli bajeti ambayo tunaitunga hapa inatekelezeka.

Mheshimiwa Waziri, nakupenda sana, wewe ni mtu ambaye ni msomi. Kwa sasa hivi mimi ninavyoona, na baada ya kusoma yale makabrasha, kusema kweli hatutafika mahali popote. Ni vizuri ukatusikiliza na kama kuna marekebisho yanaweza kufanyika kabla huja-*wind up* yafanyike ili kweli tuwe na bajeti ambayo inaweza kutekelezwa. Zaidi ya yote, angalia matumizi. Serikali kila mwaka inakwenda juu tu. Wewe unafanya biashara gani? Mapato Shilingi trilioni nane, matumizi Shilingi trilioni kumi, sasa hata mtu wa kawaida tu ukimweleza anasema, jaman,i hivi wasomi wetu wamekwenda shule gani? Hawawezi kuelewa kwa kusema kwamba kama tunapata Shilingi trilioni nane, matumizi ya ndani angalau hayatazidi Shilingi trilioni nane, *full stop*. Ulie, ufanye nini, inakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tukienda katika uwazi na kuambiana ukweli, hatutakuwa tumeelemewa na janga la kuambiwa bajeti kama hii ikataliwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LETICIA A. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Bajeti ya Taifa letu. Naomba niende moja kwa moja kwenye pato la Taifa. Kama tunavyoona, hizi takwimu za Serikali kila mwaka kumekuwa na *tendency* ya kushuka pato la Taifa. Tukianzia mwaka 2010 pato la Taifa lilikuwa kwa 7% lakini kufukia mwaka 2011 pato la Taifa limeshuka kwa 0.6% maana lilikuwa 6.4%.

Sasa hivi Serikali yetu inatuambia kwamba inatarajia kupandisha pato la Taifa kwa 6.8% ifikapo mwaka 2012/2013 na vilevile wamesema itakapofika mwaka 2016 huenda pato la Taifa litapanda kwa asilimia 8.5. Lakini Serikali yetu imekuwa na visingizio vya kushuka kwa pato la Taifa, yaani *GDP*.

Moja ya sababu au visingizio ambavyo Serikali inapenda kuvitumia ni kupanda kwa uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme. Naamini Serikali ina wachumi ambao wamebobea, ukirudi nyuma ukaangalia bajeti kumi za nyuma, kila bajeti ilipewa kisingizio cha umeme kama ndiyo tatizo kubwa ambalo nalo limesababisha kushusha pato la Taifa letu. Sasa mimi nashangaa, hawa wachumi wanafanya kazi gani? Kwanini wasije na *solution* ya kudumu kuhusu hili tatizo la umeme? Nashangaa kila mwaka wa bajeti tunaambiwa umeme ilikuwa ni moja ya changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nishati mbadala, yaani *alternative energy* ambayo inahusisha kwa mfano *solar energy.* Kuna *solar energy* ambayo Serikali haijaitilia maanani kuiwekea kipaumbele. Inaendelea tu kuzungumzia umeme ambao unapatikana kwa kutumia mafuta ambayo ni ya ghali sana. Vilevile kuna hata *wind power* ambayo Serikali ingeweza ku-*invest* pesa kwenye hizi nishati mbadala na hatimaye Taifa likaweza ku-*solve* tatizo la umeme kwa muda mrefu. Inasikitisha kuona nchi yetu haisongi mbele hasa ukizingatia kwamba kila mwaka wa bajeti pato la Taifa linashuka. Kisingizio kingine ambacho Serikali inatupa ni ukame.

Huo ukame umeimbwa miaka nenda rudi, mimi tangu nipo *Primary School* nilikuwa nasikia tatizo ambalo linasababisha kushusha *GDP* ya Taifa hili ni pamoja na ukame. Kwanini tusitafute *permanent solution* kwenye tatizo hili la ukame? Kuna *irrigation system*, kwanini hatu-*invest* pesa kwenye *irrigation system*. Wengine watadai kwamba labda maji hayatoki, lakini siyo kweli. Kuna ile *irrigation system* ya matone ambayo inaitwa *drip micro irrigation.* Kuna *sprinkler* ambayo pia inaweza kutumika kwa nchi hii ambazo hazitumii maji mengi. Sasa mimi nashangaa hivi tunafanya nini? Kwa sababu kama walivyosema wazungumzaji wengine, ni aibu hata kuchangia bajeti kama hii ambayo kila mwaka inakuja na visingizio hivyo hivyo vya kurudi nyuma kimapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie jambo lingine ambalo halizungumzwi sana. Huenda na lenyewe linachangia kwa hali ya juu sana kushuka kwa pato la Taifa letu. *Manpower productivity*. Nchi hii haitumii au hai-*calculate* vizuri *manpower productivity* ili upate *figures* ambazo ni sahihi na zinaridhisha katika uchumi wa nchi yoyote. *Manpower productivity*, yaani masaa ambayo yanatumiwa na mfanyakazi ni lazima uchukue masaa yote ambayo anatakiwa kufanya kazi kwa siku uondoe masaa ambayo anatumia kuongea kwenye simu, uondoe masaa ambayo anatumia kuwa kwenye mtandao kuzungumzia majungu, uondoe masaa ambayo anakwenda kula, ndiyo ukipata hiyo *figure* unaweza uka-*calculate man power productivity*. Lakini bila ya kufanya hivyo, tutaendelea kudanganyana na kurudisha Taifa hili nyuma. Kwa sababu tunakwepa ku-*address* matatizo ambayo yametufikisha hapa, na Serikali kwa bahati mbaya imekuwa mstari wa mbele ku-*support* uzembe na inakuja na visingizio kuweza kufunika na ku-*justify* uzembe unaofanywa na Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii bajeti tunayoizungumza, mimi kwangu sioni kama ni bajeti, kwa sababu kwanza naomba ni-*declare* kwamba mimi niko kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, lakini kuwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi haimaanishi kwamba nitakubaliana na Bajeti ambayo inagandamiza Taifa hili ukizingatia kwamba asilimia 25 tu ya Wabunge wa Upinzani ndiyo tuko kwenye hiyo Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono Bajeti hii. Hii ni Bajeti gandamizi na ni hatari sana kwa Taifa, hasa Taifa linaloendelea kama Taifa letu. Ahsante sana.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia mchango wangu kwenye Bajeti hii. Kwanza napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri wa Fedha kwa kazi nzito aliyoifanya na leo hii sisi Wabunge tumepata nafasi tuweze kuijadili hii Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokifurahia sana katika mpango huu kabla Waziri wa Fedha hajawasilisha, kwanza umesomwa Mpango na Utekelezaji wa mwaka wa nyuma. Ukisoma kile kitabu cha Mpango cha mwaka 2012/2013 ni mipango ambayo imetoa vipaumbele kwa Watanzania ambayo ni mahitaji ya Watanzania wote.

Kwa hiyo, napenda kushukuru sana kwa hilo. Pia wameweza kutoa maelekezo kwamba mwaka wa nyuma wamefanya nini. Kwamba tunapopanga lazima ueleze mwaka jana mpango wako umetekeleza vipi na nimeona maeneo makubwa wamefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, naweza kutoa *quotation* kwenye Jimbo langu, kuna kijiji kidogo tu kimepata umeme nayo ni hatua kubwa sana kwa sababu ni mpango ambao sisi Wabunge tukifika hapa, tuka-*demand* kwamba vijiji vile ambavyo wanalinda nyaya waweze kupewa umeme. Kwa hiyo, wamepewa umeme.

Sasa nasema, ni mpango mzuri kama, Serikali itakuwa inatusikiliza sisi Wabunge tukiwa tunaulizwa maswali halafu yale maswali yanajibiwa kama inavyotakiwa. Lakini sehemu kubwa kwenye Jimbo langu, naishukuru Serikali imefanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, tunapoangalia Bajeti, lazima tunaangalia makusanyo ambayo tumekusanya, halafu tunapanga, halafu ukishakusanya, unaanza matumizi. Lakini mimi napenda kuishauri Serikali kwamba katika Bajeti ya mwaka huu, ukiangalia makusanyo, kwa sababu tumepanga zaidi Shilingi trilioni 15, lazima tukusanye zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwaka jana tumeshindwa kukusanya, basi mipango ya mwaka huu ambayo inalenga kukusanya ili tuweze kufanikisha, lazima tuweke mipango sahihi.

Nataka niseme kwamba, kwa mfano, nimeona kuna maeneo makubwa ya kusamehe kodi na siwezi kukubaliana kwamba unaweza ukasamehe kodi, halafu watu wasilipe kodi. Matokeo yake, unakusanya kidogo, halafu huwezi ukafikia malengo.

Kwa hiyo, lazima ukusanye zaidi. Bahati mbaya sana tunasamehe kodi kwenye maeneo nyeti ambayo yanainua uchumi wa Taifa letu. Kwa mfano, ukisamehe kodi kwenye madini, maana yake hutaendelea kabisa. Wale itabidi walipe kodi. Sasa huwezi ukasamehe kodi kwenye madini au ukasemehe kwenye sehemu inayotoa uzalishaji mkubwa, halafu ukasema unaongeza kodi kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye kitabu chetu kinasema kwamba mishahara itaongezeka lakini watu wataongezewa na kodi. Kwa hiyo, ile *size* ya kuongeza mshahara na kuongeza kodi bado hujamsaidia yule mfanyakazi. Napendekeza maeneo ya wafanyakazi siyo tuwaongezee kodi ili tuwakamue. Wale wawekezaji wakubwa ni lazima walipe kodi, wasikwepe kulipa kodi ndiyo tutapata mapato sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili limezungumzwa sana ni kwenye matumizi ya simu. Ukiangalia matumizi ya simu, wanatumia watu wangapi Tanzania hii, unaweza ukaona watu walio wengi sana wanatumia simu. Ukisema unaongeza kodi kwenye matumizi ya simu maana yake bado sasa unataka kudidimiza maisha ya mtu, kwa sababu mtu yeyote akitaka kufanya biashara kwa njia rahisi ya kuongea hata biashara za kawaida ni lazima unatumia simu na ukiangalia katika *East Africa*, Tanzania watu wengi sana wana simu kuliko nchi nyingine. Kwa hiyo, napendekeza lile eneo la kuongeza kwenye kiwango cha simu tusiongeze ibakie kama ilivyokuwa zamani, isipokuwa kama tunasema mashirika yaliyowekeza kwenye simu inabidi walipe kodi yalipe kodi, lakini siyo tumuue mtumiaji aweze kumlipia mwenye kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tumesema kwamba kuna mfumuko mkubwa sana wa bei ambapo tunalenga kwanza kwenye kilimo, ukikosea kwenye kilimo kweli mfumuko wa bei utakuwepo, ni lazima bajeti yetu ielekezwe kwenye kilimo, maana yake tumpe maisha nafuu huyu mkulima. Kwa mfano, sasa hivi ukiangalia pembejeo, wakulima wanashindwa hata kununua pembejeo kwa sababu bei iko juu sana, tukihakikisha mbolea ya ruzuku inapatikana kwanza bei inapungua, tukishapunguza bei, yule mwananchi wa kawaida siyo tunampangia eka moja, tunampa mfuko mmoja, bado hujamsaidia. Napendekeza ile sehemu ya mbolea mtu apewe kulingana na uwezo wake wa shamba analolima, kama mtu ana shamba ekari kumi basi apewe mifuko ya mbolea kulingana na uwezo wake wa kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nimeliona kwenye bajeti, kuna maeneo mengine ni nyeti sana, kwa mfano kwenye bajeti unaweza ukaona masuala ya maji, maji ni muhimu. Ukiangalia bajeti yetu masuala ya maji ni ndogo sana, Watanzania walio wengi wana shida kubwa sana ya maji na maji tunayoongea mara nyingi Serikali inajikita sana labda Dar es Salaam. Kwa mfano juzi lile bomba la Dar es Salaam lilivyopasuka Serikali ilijikita pale, lakini ukiangalia vijiji vingi sana havina maji. Kwa mfano unaweza ukaona vijijini huko watu wengine wanatembea kilomita kumi wanatafuta maji, lakini pale ni lazima tupeleke bajeti kubwa. Bajeti ya kwenye maji ukisema unategemea mfadhili maana yake mfadhili asipoleta fedha za maji basi watu hawatapata maji, hebu tujikite sisi wenyewe Watanzania kwamba tunaweza tukakusanya

pesa yetu na tukapeleka kwenye mradi wa maji, tutakuwa tumeokoa Watanzania wengi sana, ndiyo maana kila Mbunge akisimama hapa huwa anauliza masuala ya maji. Naiomba Serikali kwenye bajeti hii ni lazima tuhakikishe mwaka huu tatizo kubwa la maji tunalitatua na tunalitatua wenyewe, kama kuna msaada tunaupata kutoka nje ya nchi iwe unasaidia tu, lakini siyo kwamba tunasema tunategemea msaada moja kwa moja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upande wa dawa, ukitaka kuangalia kwenye *dispensary* za kwetu hata hospitalini dawa zimepungua sana, watu hawana dawa. Kwa mfano siku moja nilifanya ziara moja kwenye zahanati moja kwenye Jimbo langu ya Kasanga, watu wanatoa *order* ya dawa kwa bajeti ya shilingi milioni tano, analetewa za shilingi milioni moja, unaweza ukaona hazisaidii kitu chochote. Ninaiomba Serikali kwenye masuala ya dawa ihakikishe kwamba wananchi wetu wanapata matibabu sahihi na dawa zinakuwepo hospitalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba niongelee kuhusu wafanyakazi. Tumeona katika mapendekezo ya Waziri amesema kwamba mtu ataruhusiwa kulipa kodi kuanzia mshahara wa laki moja na sabini na tano elfu, kuna mashirika mengine yanalipa mshahara mdogo sana, wanasema Serikali kwa sababu haijapandisha mshahara na wenyewe hawawezi kupandisha mshahara. Kama mwekezaji atashindwa kumlipa mfanyakazi mshahara ambao anaweza akajikimu katika maisha yake, huyo siyo mwekezaji anakuwa kama anakuja kutonyonya. Ninapendekeza kwamba mashirika makubwa ambayo yanafanya uzalishaji mkubwa basi kiwango cha mshahara kiwe juu ya hii laki moja na sabini na tano elfu, kama kuna shirika litalipa chini ya kiwango cha laki moja na sabini na tano elfu, maana yake lile shirika limeshindwa kufanya kazi, ni nafuu washindwe kuwekeza waturudishie sisi Watanzania tuweze kuendesha. Unaweza ukaona kuna mashirika mengine yanafanya uzalishaji mkubwa sana lakini ukiangalia mishahara inayolipwa kwa wafanyakazi ni mishahara midogo. Unaweza ukaona mtu anamlipa mshahara elfu tisini na tano ukiangalia uzalishaji wake ni mkubwa. Kwa mfano kuna makampuni mengine yana zaidi ya miaka hamsini hapa kwetu, bado wanalipa mshahara mdogo sana wanasema mbona Serikali haijapandisha mishahara. Naishauri Serikali itunge sheria kwamba hata haya makampuni ya watu binafsi waweze kulipa mishahara mikubwa kulinga na kiasi ambacho tumekiweka cha kukatia kodi siyo chini ya laki moja na sabini na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tumesema sasa hivi asilimia sabini ni matumizi ya kawaida na matumizi ya kawaida maana yake ni mishahara na mambo mengine ya kwaida kama posho na vitu vingine, lakini sisi kama tumeweka asilimia sabini kwa ajili ya kulipa mishahara na mambo mengine, ninaiomba Serikali iwaangalie hata wale Wenyeviti wa Vijiji, kwa sababu Wenyeviti wa Vijiji ndiyo mwanzo wa kuleta maendeleo. Mtu yeyote hapa anapofanya mkutano wowote ni lazima amwone Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Kijiji akusanye watu muongelee masuala ya maendeleo, mkae pamoja mpange. Sasa hiki kiasi ambacho tunasema asilimia sabini ni lazima na wale waguswe, hizi pesa ni lazima ziende na wale wapewe, siyo kwamba ni wale walioajiriwa tu, wale wanafanya kazi kubwa sana katika kuleta maendeleo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Kilufi ajiandaye na Mheshimiwa David Ernest Silinde ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nashukuru kwa kupata fursa hii na kabla sijasahau na ili nisije nikaonekana nina nongwa maana katika mambo mia moja ni lazima kuna moja zuri. Kwa niaba ya vijana waendesha bodaboda, naomba nitoe shukrani kwa kuwaondolea ushuru, kwa sababu unapoondoa kodi kwa waendesha bodaboda, unawalenga vijana walio wengi, maana baada ya kupata changamoto ya ajira wengi wamejikita huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie bajeti, kwa upande wangu sijaona jipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona jipya kwa sababu moja, mwaka jana wakati tunachangia bajeti, Wabunge humu ndani tulizungumzia fedha nyingi kwenda kwenye matumizi ya kawaida, tulizungumzia Serikali kuendelea kutegemea fedha za wafadhili katika miradi ya maendeleo, tulizungumzia Serikali katika masuala mazima ya msamaha wa kodi. Mwaka huu hayo mambo yapo na ninasikitika kwenye Mpango wa Miaka Mitano ulikuwa unazungumzia kuepukana na matumizi yasiyokuwa na lazima, lakini leo hii trilioni kumi zimewekwa kwenye matumizi ya kawaida, mwaka jana ilikuwa trilioni nane, Mpango wa Miaka Mitano unasema utapunguza, sisi Wabunge wawakilishi wa wananchi tulitarajia ingeanza kwenye bajeti hii lakini badala ya kupunguza au mara mia mngeacha zilezile trilioni nane, mmeongeza trilioni mbili zaidi, sasa sijui wenzangu watanisaidia mmepunguza kama mlivyoahidi au mmeongeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwenye matumizi ya kawaida ya trilioni kumi, sina tatizo na deni la Taifa ingawa tunahitaji mchanganuo zaidi tujue hizo fedha zinaenda kulipwa katika kitu gani. Sina tatizo na ongezeko la mishahara ingawa haijaongezeka sana kwa sababu mishahara sasa hivi ni shilingi trilioni 3.7 na mwaka jana mishahara ilikuwa shilingi trilioni 3.2 ni kama shilingi bilioni mia tano lakini kwenye matumizi mengineyo mwaka huu ni shilingi trilioni nne, mwaka jana matumizi mengineyo yalikuwa shilingi trilioni tatu. Katika matumizi mengineyo shilingi trilioni moja imepelekwa kwenye matumizi mengineyo, shilingi trilioni moja imepelekwa kwenye Wizara, mwaka jana kwenye Wizara ilikuwa shilingi trilioni 2.7 sasa hivi ni shilingi trilioni 3.3. Ni ongezeko la shilingi bilioni mia sita arobaini na sita, wenzangu watanisaidia. Hizi fedha zilizoongezwa kwenye Wizara hazihusiani kabisa na miradi ya maendeleo na huku kwenye Wizara ndiko kwenye ufujaji wa fedha, tuliona hapa posho hewa zilizogawiwa pale kwenye Wizara ya Nishati na Madini, wakati Wizara zinaongezewa shilingi bilioni mia sita arobaini na sita, kwenye fedha nyingine zimeongezwa shilingi bilioni 646, Wizara peke yake wanapata shilingi bilioni mia tano themanini na tatu lakini kwenye mahitaji mengi, Mikoa na Halmashauri ongezeko ni shilingi bilioni 62 tu. Wakati kwenye Mikoa kuna ongezeko dogo nikitolea mfano Mkoa wa Mara mwaka jana kwenye fedha za maendeleo bado mpaka leo hii hazijaenda zote karibia shilingi bilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunalalamika suala la vipaumbele kwenye bajeti zetu, wakati tunawarundikia fedha za kula Wizara shilingi bilioni mia tano themanini na tatu leo hii tunaambiwa kwenye miundombinu, reli, bandari, barabara zimetengwa shilingi trilioni 1.3, ambayo ni nusu ya fedha ambazo zimepelekwa kwenye matumizi mengineyo, shilingi bilioni mia sita arobaini na sita. Wakati hizo fedha zinapelekwa huko, tunasema tunataka kuondoa tatizo la maji safi na salama, tunatenga tu shilingi bilioni mia tano, matumizi mengineyo shilingi bilioni mia sita, ongezeko la kwenye Wizara shilingi bilioni mia tano themanini na tatu. Wakati tunalalamika haya, kwenye vitu vya msingi unapozungumzia kukuza uchumi unazungumzia reli, unazungumzia bandari, tumetenga shilingi trilioni 1.3 na kati ya hizo shilingi trilioni moja ndiyo imeenda kwenye barabara. Sasa hatujui huko kuna kulipa madeni maana bajeti iliyopita kama ndiyo hivyo miradi haikutekelezeka. Kwenye vitu vya msingi tulivyovipigia kelele vilivyochangia Wizara ya Uchukuzi kurudishwa mwaka jana wametengewa shilingi bilioni mia tatu tu na themanini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii namwonea huruma Mheshimiwa Mwakyembe sijui atawaambia nini Watanzania kama reli isipoanza kufanya kazi, hamkumpa fedha. Tunapozungumzia ukarabati wa reli hapo imehusisha mabehewa, imehusisha na ukarabati wa injini, hakuna suala la kukarabati njia za reli kwa kiwango kikubwa wala ujenzi wa miundombinu mipya ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mmoja tu, unapozungumzia ukarabati wa reli ya Kilosa, ambayo ilisombwa na mafuriko miaka iliyopita, mahitaji ya ukarabati wa ile reli ni shilingi bilioni 38, lakini cha kusikitisha fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni nne tu. Leo hii tunajitapa tunataka kurudisha usafiri wa reli kwa ajili ya kukomboa uchumi wa nchi hii tunatenga shilingi bilioni nne kati ya mahitaji ya shilingi bilioni 38! Hii haikubaliki, bado hapo hatujagusa viwanja vya ndege, hatujagusa bandari, bajeti hii siyo *realistic*. Ni lazima tuwe na vipaumbele vichache ambavyo tutavitengea fedha za kwetu za ndani ambazo tuna uhakika wa kuzipata kwa maslahi ya nchi

yetu, tusije tukaongea tukaonekana wakorofi, tunajua kule wananchi wa chini wanahitaji nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la *EPZ*, wananchi wa Bunda wamechoka na kilio hiki. Mwaka jana niliuliza kwenye Bunge hili, Waziri akaji- *commit* lakini leo kwenye Mpango unagusa Kigoma na Bagamoyo. Sasa wananchi wa Bunda wanashangaa, ilikuwa ni ahadi ya kuwatuliza au ahadi ya kuwatekelezea jasho lao halali baada ya kupisha mradi wa *EPZ*. Hili halikubaliki, nitahitaji majibu sahihi. Mimi vijana wenzangu wameniambia hawatakuwa na tatizo kama watapata majibu sahihi, wameniambia kabisa! Mwakilishi wetu huna haja ya kwenda kuunga mkono hiyo hoja mpaka upate majibu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina cha kuunga sasa hivi bila kumsikia Waziri ananijibu nini kwa haya niliyochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia suala la mfumuko wa bei, ni umeme, chakula vinachangia mfumuko wa bei kwa asilimia 24, tunaomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa, ahsante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Silinde ajiandae na Mheshimiwa Ali Khamis Seif ajiandae.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kupewa fursa hii ya kuweza kuchangia katika bajeti hii ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mbarali, nimeombwa niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti nzima ni shilingi trilioni kumi na tano, matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni kumi na kwenye maendeleo ni shilingi trilioni tano, yaani katika hali ya kawaida huwezi kueleweka kwa sababu unatumia kuliko unavyowekeza. Kwa sababu kama tungewekeza kwa shilingi trilioni kumi kwenye miradi ya maendeleo na tukatumia shilingi trilioni tano walau ingeleta maana, lakini katika hali hii kwa kweli mwenendo huu hatuwezi kufika na hao Watanzania maisha bora tunayoyazungumza itakuwa ni ndoto. Kama ingekuwa ni ridhaa ya Waheshimiwa Wabunge wote, kwa maoni yangu ningesema kwa sababu fedha hizi hatuwezi kuzipata nje ya bajeti hii, hizi *OC's* ambazo Serikali wamejirundikia basi ziingie kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta mahali pengine kwa mfano nichukulie Wizara moja kwenye *OC* tu peke yake wamejiwekea shilingi bilioni mia moja na thelathini, ukienda kwenye miradi ya maendeleo wameweka shilingi bilioni 67, sasa kwa nini tusipunguze kwenye *OC* tukaongezea kwenye miradi ya maendeleo ili walau bajeti yetu iwalenge hao Watanzania wengi ambao siku zote wanapata shida? Kwa hiyo, kama ningekuwa ni mimi badala ya kugomea bajeti, ningesema hizi zote walizojilundikia kwenye *OC* ziende kwenye miradi ya maendeleo, naamini kabisa walau tungepiga hatua ili kuwatendea haki hawa Watanzania walio wengi. Nasema hivyo kwa sababu Serikali kama Serikali ambayo ndiyo inasimamia mapato ya nchi, kwenye kutumia wao wanajipangia vizuri tu, tatizo ni sisi Wabunge ambao tunawakilisha wananchi ndiyo tunaopata shida, kwa hiyo kuunga mkono matumizi hayo ya Serikali maana yake tunawasaliti Watanzania ambao tunawawakilisha. Nilikuwa nashauri kama inawezekana sasa Serikali badala ya kuwashika wananchi ishikwe yenyewe, tuchukue *OC* kila Wizara nusu ya *OC* yake iingie kwenye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini penye ukweli ni lazima useme ukweli, yapo ya kushukuru. Wilaya ya Mbarali Jimboni kwangu ina eneo la hekta milioni moja na laki sita, kati ya hizo hekta 77.76 zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, niishukuru sana Serikali kwamba Mbarali kuna *scheme* zaidi ya 80 ambazo tayari zinatumika kwa kilimo lakini kati ya hizo, 30 Serikali imeingiza mkono wake ili kusaidia kuboresha miundombinu yake. Tatizo sasa inapokuja kwenye bajeti hii ambayo Watanzania na Wanambarali walitegemea kwamba ingeweza kuboresha miundombinu hii, katika

themanini, thelathini ndiyo imeboreka walau Serikali imeingiza mkono wake, ina maana hamsini yote wananchi wanahangaika tu. Nataka niwaambie ndugu zangu, Mbarali tunazalisha mpunga sana na ni chakula kinachopendwa sana nchi hii. Leo hii ukifika Mbarali tunasafirisha zaidi ya *semi teller* 15 kila siku kupeleka Dar es Salaam kwa ajili ya kulisha Jiji la Dar es Salaam lakini kama Serikali haitaunga mkono *scheme* hizi 50 kwa maana ya kuziboresha tunapoteza mapato mengi sana yanayotokana na zao la mpunga ambalo lingeweza kusaidia kupunguza mfumuko wa bei kwa sababu tungeweza kuzalisha zaidi tukiungana na maeneo mengine ambayo yametajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu gani? Nina miradi kama ya Uturo, Mashala na Gwiri, mwaka jana ndio *scheme* pekee zilizopata fedha kwa ajili ya kuziendeleza lakini hizi *scheme* zingine zote zilizobaki ambazo tunatarajia Serikali ituunge mkono kwa mfano *scheme* ya Igomelo, Lwanyo, Madibila, Majengo, Mashala inayotakiwa kuboreshwa, Mpungammoja, Mwendamtitu, Nyanalila, Uturo hizi ni *scheme* ambazo tunategemea bajeti hii ituunge mkono ili tuweze kuziboresha na tumeombea zaidi ya shilingi bilioni sita. Sasa kwa bajeti hii ni wazi kwamba hii itakuwa ni ndoto. Sasa wananiangalia huyu bwana anaunga mkono kutumaliza au anaunga mkono kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikipata majibu ya uhakika namna gani wananchi hawa wa Mbarali ambao wanahangaika na hizi *scheme* ambazo hazijaboreka basi nitakuwa tayari kuunga mkono. Tunayo *scheme* ya Mwendamtitu ambayo Serikali imekuwa ikiahidi mara kwa mara kwamba itatoa fedha lakini hadi sasa ninavyozungumza bado haijapewa fedha. Kwa mwaka huu tulikuwa tumeiombea shilingi milioni 763 licha ya zile shilingi milioni 500 ambazo tuliahidiwa kwamba zitapelekwa na mpaka sasa kazi ile haijaanza. Mimi nitaunga mkono tu pale nitakapoona kwamba nimepata majibu ya kuridhisha kwamba ni namna gani hizi *scheme* ambazo Serikali ilishaahidi zinatekelezwa na zinapewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha hiyo, nije upande wa mifugo, bajeti hii haionyeshi kabisa kutoa majibu ya kuendeleza sekta ya mifugo. Sekta ya mifugo ni sekta nyeti katika nchi hii, ni sekta ambayo imetengewa shilingi bilioni 54 pamoja na matatizo makubwa ambayo sekta hii inayo. Sekta ya mifugo kama ingesimamiwa vizuri ingeweza kuinua pato la taifa. Viwanda vile ambavyo tulikuwa tunategemea vya ngozi ambavyo ni zao la mifugo navyo vyote sasa hivi havifanyi kazi hasa baada ya kuwapa wawekezaji. Wafugaji wanahangaika na mahali pengine wanafikia mpaka kuuana lakini bajeti hii haionyeshi kabisa kwamba kuna *seriousness*, kuna umuhimu wa kutaka kukomboa jamii ya wafugaji. Kwa hiyo, mimi bado naomba nipate majibu ya kuridhisha kwamba ni vipi tutaboresha sekta hii ya wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye Wizara ya Maji, ukizungumzia maji maana yake kila Mtanzania ana matumaini makubwa kwamba bajeti hii ingeweza kusaidia watu wakaepukana na shida ya maji lakini kwa bajeti hii bado inaonyesha kwamba huenda ikawa bado ni kitendawili kuweza kuwasaidia Watanzania hawa kupata maji ya uhakika. Hii ndiyo inayowapelekea vijana wengi sana kukimbilia mjini kwa sababu maeneo ya mjini walau huduma hii inapatikana na huduma nyingine mfano umeme zinapatikana. Hawa vijana unataka wakae kijijini wafanye nini? Kilimo ndio hicho hakina bajeti ya kutosha kuandaa miradi mingi ya kuweza kujiajiri, wao waende wapi? Kama hatutaweza kutumia nguvu kazi ya vijana hawa kwa kuwaandalia wapi waende wakazalishe, nina hakika tutaendelea kuona wanayumbayumba mjini lakini si kosa lao, wafanye nini? Nani yuko tayari kwenda kukaa kijijini ambako hakuna huduma? Tungeboresha kijijini kukawa na huduma ya maji, kukawa na huduma ya umeme, vijana hawa wasingekimbilia mjini, wangebaki kule wakizalisha na wakichangia pato la taifa lakini kwa sasa hivi hakuna jitihada zinazofanyika kuona hawa vijana wanapata ajira. Kwa mfano, ni mategemeo yangu kwamba bajeti hii ingeweza kusaidia vijiji vya Manienga, Itipingi, Kangaga, Ipwani, Matemela, Mkandani, Chimala, Simike, Iyala, Mpolo, Luhanga, Ubaluku, Dindilwa, Ukwavila, Igulusi, Mkunywa, kupata maji na kwenye bajeti hii vilikuwa vimeonekana kwamba sasa vitapata ufumbuzi wa matatizo yao lakini kwa bajeti hii inaonyesha bado ni tatizo. Nasema hivi, nikipata majibu ya kuridhisha, namna gani hawa wananchi waliopata tabu kwa miaka mingi na wanaendelea kupata tabu watapata huduma hii muhimu, ndipo nitakuwa tayari kuunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ili iweze kuendelea ni lazima Serikali ikubali kubadilika, kama hatutabadilika tutakuwa tunaandaa bajeti kwa mazoezi, ndio haya yaliyotufikisha hapa. Inatakiwa bajeti iwe shirikishi, Wabunge tushirikishwe kwa sababu sisi ndio tunajua vipaumbele vya wananchi wetu. Sasa leo inakuja bajeti ambayo hatujashirikishwa, matokeo yake tunaanza kushikana hapa lakini tungekuwa tumeshirikishwa kutoka mwanzo leo tungekuwa tumepanga pamoja tusingekuwa tunapigiana kelele. Kwa hiyo, maoni yangu mimi ni kwamba nitaunga mkono bajeti hii kama haya mazuri ambayo Serikali imeshaonyesha kwamba ina nia ya kuwafanyia Watanzania yanaonekana kutekelezwa vinginevyo tukubali *OC* zipunguzwe tuingize kwenye maendeleo, mimi nitaunga mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi angalau nichangie bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Bunge lako lianze kutafakari kama bajeti hii inakidhi maswali na matatizo ya Watanzania, ndio maswali ambayo tunahitaji kujiuliza. Tunahitaji kujiuliza kama waliokuwa wanaandaa bajeti hii walifuata mapendekezo/maoni/ushauri wa Wabunge na watu mbalimbali? Tunahitaji kujiuliza kama vipaumbele vilivyowekwa katika Mpango ambao unakwenda kutekelezwa katika bajeti, ni vile Watanzania wanavyovihitaji? Ndio maswali ya kujiuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitahi kujiuliza kama bajeti imekidhi vigezo vya kutatua matatizo ya Watanzania na majibu ambayo yamekosekana kwa takribani miaka 50 sasa, tusizungumzie bajeti ya mwaka mmoja. Tunachofanya ni kutafuta *reflection* ya bajeti kwa miaka 50, ndio maswali ambayo Watanzania wanahitaji kujua majibu yake. Nchi ina tatizo la maji na wakati ni nchi iliyozungukwa na maziwa ya kila aina, tuna mito mikubwa, huwezi kutulinganisha na nchi kama Misri ambako ni jangwa, huwezi kutulinganisha na nchi kama Libya ambako ni jangwa lakini wananchi wake zaidi ya asilimia 80 wanapata maji safi na salama, bajeti haijatueleza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kufahamu, kama Watanzania wamekwenda kuulizwa tatizo la afya, kwa wananchi wote kwa ujumla ambalo bajeti ilihitaji kujibu je, wataalam wanajua kwa kina ama wanajua tu kwamba kuna tatizo la maji, kuna tatizo la barabara, yanaweza kuwa yanajulikana lakini watu hawajui matatizo kwa undani wake. Tunahitaji kujua ni maoni gani yalitumika kuainisha vipaumbele vilivyowekwa, hayo ndio maswali yanayohitaji kujibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishapata majibu ya maswali hayo ndio tutakuwa na uwezo wa kutatua matatizo ya Watanzania, Watanzania wamechoka. Miaka 50 bajeti imekuja na sababu zilezile na hakuna kitu ambacho kinaudhi ndani ya Bunge, watu tumekuwa tukizungumza vitu vya namna ileile mwaka jana wamezungumza, miaka ya nyuma wamezungumza, lakini majibu ya msingi ya maswali yanayoulizwa na Wabunge bado Serikali inashindwa kuyapatia majibu. Ukali wetu si kwa sababu tu wamebadilisha Waziri kwa sababu Ofisi ya Waziri wa Fedha ipo, ilikuwepo, na itaendelea kuwepo. Kwa hiyo, tutaendelea kuihoji Serikali kwa sababu ndio inayowajibika kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali haya Watanzania wanahitaji majibu, hatuhitaji kuendelea kuwa na *propaganda*. Tatizo kubwa linalolikabili Taifa letu, viongozi wengi siyo *visionary* na wala siyo *strategist*, yaani hawana mikakati na wala hawana dira wamekaa katika *propaganda* zaidi kuliko kitu kingine. Kiongozi unahitaji kuwa na vitu vyote vitatu lakini tume-*rely* kwenye kitu kimoja *propaganda* zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kukueleza ni kwamba bajeti hii inatupa *agenda* ya kuzungumza kwa Watanzania. Mimi nawashangaa sana kwa nini huwa mnapenda kutupa *agenda*? Bajeti haijajibu majibu ya wananchi wa chini wanaoishi vijijini na maeneo mengine angalau watu wa kati na kuendelea huku mbele lakini watu wa chini hawahusiki kabisa katika bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanahitajika majibu katika haya maswali. Ukisoma katika Mpango uliosomwa na Mheshimiwa Stephen Wasira, Mpango unaeleza kwamba mwaka jana

uchumi wa Afrika kwa ujumla ulikua kwa asilimia 2.7 na umejaribu kueleza sababu kwamba miongoni mwa sababu ni kuchafuka kwa hali za kisiasa nchi za Misri pamoja na Libya na maeneo ya nchi za Kiarabu lakini kiukweli nilikuwa naangalia ukuaji wa uchumi wa kila nchi, nchi maskini kabisa ambayo nimejaribu kupitia Somalia, sijui Sudan wenyewe uchumi wao wanasema ulikua kwa zaidi ya asilimia 3.3 lakini nchi ambayo uchumi wake ulikua zaidi ni zaidi ya asilimia 7.2, *overall* ya nchi kama nchi ya mwisho ni asilimia 3, tunakuaje na pato la ukuaji wa uchumi kwa asilimia 2.7 kama siyo taarifa ni ya uongo ni nini? *Propaganda* imekuwa kubwa kuliko uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, taarifa ya jumla ni kwamba wote humu ndani uwezo wetu ni milioni saba lakini taarifa ya uongo kila mmoja akisema mimi uwezo wangu, mtu wa mwisho anasema mimi kwa mwaka napata milioni tisa na mtu wa *highest* anasema kwamba kwa mwaka napata milioni 18 maana yake ukijumlisha pato la jumla linakuwa ni zaidi ya milioni 10 lakini unataja kiwango cha chini, maana yake ni uongo. Kwa hiyo, taarifa zenyewe zinakinzana. Ni muhimu masuala haya yapatiwe majibu ya msingi ili watu waweze kuyaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuja kukigundua ni kwamba tuna Usalama wa Taifa na tuna Usalama wa Viongozi wa Taifa. Usalama wa Taifa wa nchi umepoteza mwelekeo, Usalama wa Taifa wa nchi hausaidii Watanzania umekuwa ukisaidia tu watu fulani waendelee kubaki, nani anatupinga na nini lakini hausaidii Watanzania, wametoka kabisa katika dhamira ya kweli ya kusaidia Taifa hili. Unakuta wanazungumza nani kasema nini, kwa nini na kwa sababu gani, wameshindwa kujua na kubainisha matatizo ya msingi yanayolikabili hili Taifa kwa takribani miaka 50 sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kufanya mabadiliko makubwa kwenye Kitengo cha Usalama wa Taifa. Msipofanya mabadiliko kwa mwendo huu nawaambia siku zote na tatizo la Usalama wa Taifa wa sasa hivi limekuwa na hulka ya kuwa na taarifa za kuridhisha viongozi kwamba haya matatizo ya Watanzania ni mpito tu, ni *propaganda* siyo ya kweli lakini wanashindwa kueleza hali halisi ya taifa letu. Ndicho ambacho kimekuwa kikionekana kwa sababu kama Usalama wa Taifa wangeainisha matatizo ya Watanzania wakayapeleka kwenye ofisi zinazohusika tafsiri yake ni kwamba hii leo tusingekuwa tunajadili bajeti ambayo haina mantiki kama hii. Watanzania wanasema kama Serikali imekosa majibu ya msingi ya kila hoja, kuna haja gani ya kujadili bajeti, kuna haja gani ya kuendelea kuwatawala watu ambao tumeshindwa kuwa na majibu ya matatizo yao? Ni kweli unapokuwa kiongozi lazima ulaumiwe, lakini lawama zinapozidi kiwango maana yake wewe kiongozi hufai kuwa kiongozi hiyo ndio tafsiri yake. Sasa majibu mengine katika Wizara zetu na katika Serikali yetu, Serikali imekuwa ikishindwa kutoa majibu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti za kwetu tulizokuwa tunazipitia kwenye kila Idara ukisoma randama asilimia 80 ya bajeti tumekuwa tukinunua vitu vilevile, kila mwaka kununua kompyuta, safari, posho sijui nini yaani vitu vilevile wanarudia *printers* sijui gharama yake ni kubwa na ndio maana bajeti inaonekana kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tunapokuwa tunazungumza na baadhi ya marafiki zetu wanasema kabisa kwenye *OC* ndiko wanakopigia fedha, ndio wanasema; na ndio maana mwaka jana tulikuwa tunapinga kwa nguvu zote ile sheria iliyopitishwa ya kununua vitu chakavu, tulikuwa tunapinga kwa sababu hii, kwa sababu kila mwaka tunanunua vitu vilevile yaani haieleweki kwamba hivi vitu vinanunuliwa ama, ukiwauliza wanasema tumebadilisha matumizi tumepeleka eneo lingine, kwa hiyo, mwaka huu inabidi tununue tena, hii ni michezo tu, ni sanaa kwa Watanzania. Tunasema jamani mwaka 2015 tusubiri Watanzania watatuhukumu kwa kile tunachokifanya na watu wanafikiri, unajua hata Gaddaf wakati anaondoka alikuwa hajui kama anaondoka. Narudia tena, nilishawahi kuzungumza hii sentensi mtu anayefilisika huwa hajui kama anafilisika lakini sisi tulio pembeni tunajua kwamba anafilisika na ndivyo watawala walivyo, siku zote watawala wote wanaoondoka huwa hawajui wanaondoka ni kwa sababu mmeshindwa kujibu maswali ya msingi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hali ni ngumu lakini ndio hivyo, Watanzania wanataka Bunge litoe tamko juu ya masuala ya rushwa, Wabunge wanakula rushwa, Bunge halijatoa tamko. Bunge linaogopa kutoa tamko, maswali haya Watanzania wanahitaji kujibiwa kwa sababu

haiwezekani tuwe tunapanga bajeti, tunatenga fedha kwenye *PCCB* lakini masuala kama haya Bunge lenyewe linaogopa kuyajibu, Watanzania wanataka hayo majibu kwamba taifa hili sasa hivi hatujafikia huko wanakotaka twende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha za rada, tuliambiwa Bungeni fedha zile zitakaporudishwa zitakwenda kwenye mashule, madawati na mambo mengine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Namwita msemaji wetu wa mwisho kwa jioni hii Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu na pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano huu unajadili bajeti ya shilingi trilioni 15.1 ambayo ni ya mwaka 2012/2013 lakini mimi nahisi bila ya kupata tabu ili kuona uwezekano wa bajeti hii ambayo tunaijadili leo kutekelezeka kwake, ni vizuri turudi kwenye bajeti ambayo ilikuwa na shilingi trilioni 13.5 utekelezaji wake umekuwa vipi? Nadhani tukiona ilivyotekelezwa na hasahasa katika sehemu ya maendeleo siyo matumizi ya kawaida, kwa sababu matumizi ya kawaida yako karibu asilimia 87 mpaka Aprili, sasa nadhani hapo tutaona uwezekano wa bajeti hii ambayo tunaijadili kuwa ipo au haipo, tuone matatizo ambayo imeikabili ile bajeti iliyopita, tuone hayatatokea tena matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, katika fedha zake za maendeleo ilitengewa fedha karibu shilingi bilioni 20, mpaka Mei mwaka 2012, Wizara hii imepewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.6, hii ni sawasawa na asilimia 17, kama ziko Wizara zimepata asilimia 30, 40 hiyo ni bahati. Unapoidharau ardhi, kwa kweli nchi imekwisha kwa sababu leo Tanzania inaonekana kama ardhi haipo wakati si kweli, ardhi imekosa mipango bora, matumizi bora ya ardhi katika nchi hii hayapo, kwa hiyo, wafugaji na wakulima wanapigana kwa sababu haijatengwa ardhi ya wafugaji na ardhi ya wakulima, nani atakayepanga ardhi hiyo? Ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi! Fedha walizopewa kutoka shilingi bilioni 20 wamepewa shilingi bilioni 3, leo Wizara tutakuja kuilaumu, hii ndio hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo kwenye ardhi utakuta wawekezaji wanapambana na wanavijiji kwa sababu ardhi haipo, Serikali haina Benki ya Ardhi, wanaostahili kufanya hivyo ni Wizara ya Ardhi, lakini bado fedha ya maendeleo waliyopewa ni shilingi bilioni 3.6 ambayo ni sawasawa na asilimia 17. Kwa hiyo, ni dhahiri ukichukua hii Wizara moja utaona kuwa utekelezaji wa mpango uliopita ambao unaishia Juni mwaka huu haukuwa katika ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara nyingine, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano. Hawa walitakiwa wapewe shilingi bilioni 12 za maendeleo, wamepewa shilingi bilioni 5.3, sawasawa na asilimia 36. Sasa ukichukua Wizara zote utakuta utaratibu ni huu, fedha ya maendeleo haipo. Kwa hivyo, hakuna haja ya kuamini kuwa Serikali hii itatuhakikishia sisi kuwa *budget* inayokuja fedha ya maendeleo itapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukosefu wa fedha uliosababisha haya bado upo palepale, hakuna miujiza. Hakuna miujiza wa ukusanyaji wa fedha ambayo itafikia kiwango ambacho kinatakiwa. Kwa hivyo, bado bajeti hii ninavyoiona mimi ya shilingi trilioni 15.1 ni kiini macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia kwangu mimi karibu shilingi trilioni mbili nukta fulani hivi ambazo hazipo katika bajeti iliyopita. Sasa unaposema bajeti iliyopita ni shilingi trilioni 13.5, ukitoa shilingi trilioni mbili, bajeti halisi ina maana ni shilingi trilioni 11 lakini mipango iliyopangwa ni ya shilingi trilioni 13.5. Kwa hivyo, hata hii ya shilingi trilioni 15.1 bado ni suala lilelile ambalo litakuwa fedha za nje hazipo, makusanyo yamepungua, inaweza ikafika pengine mwisho

wa mwaka mwakani ikawa pengine ni shilingi trilioni 13, kesi ikawa ni ileile. Kwa hivyo, hii mimi mtazamo wangu si shilingi trilioni 15.1 ni shilingi trilioni 13 tu kama itafika hivyo. Kwa hivyo, kwa kweli yaliyopangwa yote basi hayawezi yakatekelezeka kama ambavyo yamepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichogundulika kingine ni kuwa Serikalini sijui kuna utaratibu gani wa ugawaji wa fedha, ni jambo la ajabu kweli. Inaonekana wengine ni watoto wa kambo, wengine watoto hasa katika hizi Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fedha ambazo ni za ndani zilizokusanywa ni asilimia 64.2 zote kwa ujumla lakini za nje ni asilimia 47, kwa hiyo ukichukua wastani ina maana fedha ambazo zimepatikana na asilimia 55.6. Kwa hivyo, ina maana kila Wizara ilikuwa ipate fedha hizo, lakini leo utakuta Wizara kama niliyoitaja ya Ardhi imepata asilimia 17, Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano asilimia 36, sasa hizi nyingine zina upendeleo gani kutoka Wizara ya Fedha? Mimi nadhani pengine inatokana na uenyeji, pengine inatokana na kuelewana, lakini Serikali haiendi hivyo, Serikali ina utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haiwezekani kuwa Wizara zingine zipewe fedha kidogo mno, nyingine zipewe nyingi wakati hii ni bajeti imeletwa hapa na ikapitishwa. Inaonekana sisi kukaa hapa tukapitisha kwa kweli ni kazi bure tu, kinachokwenda kufanywa huko ni Serikali wanachokiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa kweli kama haijajikita katika uzalishaji hasa, basi tutabakia hivihivi na tutanung'unika kila siku. Leo tuangalie suala dogo la utalii ambalo ni njia mojawapo ambayo Serikali inaweza ikapata fedha. Leo Tanzania kila mmoja anajua kuwa ina vivutio vya utalii ambavyo haviko duniani au sehemu nyingi za dunia, lakini bado utalii wake unashangaza. Kwa mfano mwaka 2010, watalii walioingia Kenya ambao Kenya na sisi, sisi tuna vivutio vingi, ni nchi ya pili duniani pengine kwa vivutio vya utalii lakini watalii walioingia Kenya kutoka nchi za nje, ni milioni 1,600,000, Uganda ni laki 945,899, Tanzania ambao tuna vivutio kuliko nchi yoyote katika hizi katika mwaka 2010 wameingia watalii laki 782,699, hivi sasa wamefikia laki 897,994.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nawataka radhi kwamba nilisema mchangiaji wa mwisho, tunaendelea. Sasa naomba niwataje watakaochangia, tutaanza na Mheshimiwa Rosweeter Kasikilia, Mheshimiwa Tundu Lissu ajiandae, Mheshimiwa Habib Mnyaa na Mheshimiwa David Kafulila wajiandae. Mheshimiwa Rosweeter.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa nafasi hii nzuri ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, lakini pia niweze kumshukuru Waziri wa Fedha kwa bajeti hii ambayo wameiandaa. Najua wamechukua muda mwingi kuweza kuandaa walichokiandaa. Hata kama kitakuwa na upungufu mkubwa ndiyo maana wamekileta hapa Bungeni ili tuweze kukiangalia na kukijadili, tuweze kuweka sawa. Ingekuwa ni bajeti ambayo imeandaliwa kwa uzuri wa asilimia 100 kwa 100, hapakuwa na haja ya kuleta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda huu mfupi nilionao, ningependa nijikite moja kwa moja kwanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa jinsi ambavyo ameweza kutusaidia wananchi wa Rukwa kuweza kutuletea zile barabara. Sasa hivi tuna barabara ya Tunduma-Sumbawanga, Sumbawanga kwenda Kasanga na Kasesha, lakini pia barabara ya Sumbawanga kwenda Mpanda. Tunajua kwa hakika huu ni mwanzo wa Mkoa wa Rukwa ambao kwa kiwango fulani uko nyuma sasa hivi tutaanza kupata maendeleo. Barabara hizi zitatusaidia lakini nilikuwa naomba basi fedha zinazokuwa zimetengwa kwa ajili ya barabara hizi, ziwe zinatolewa mapema maana zinacheleweshwa kwa kiwango ambacho hata Wakandarasi kazi yao ya kutengeneza barabara *speed* inakwenda ikisuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea kidogo kuhusu barabara, ningependa kuongelea kuhusu umeme. Kwa hakika Mkoa wa Rukwa, bila umeme maendeleo ni kitendawili. Tunajua kabisa kwamba Rukwa ni Mkoa tajiri sana. Mkoa wa Rukwa una rasilimali nyingi sana na hakuna asiyejua kwamba Mkoa wa Rukwa pia unalisha nchi hii na hata nchi jirani. Kwa maana hiyo, Mkoa wa Rukwa tungekuwa na umeme wa uhakika, tungeweza kuwa na viwanda vingi tu, sasa hivi tuna kinu kimoja tu Mkoa wa Iringa ambacho kinachosindika unga kwa ajili ya nchi hii lakini Rukwa tungekuwa na umeme wa uhakika, basi ina maana kwamba na sisi tungeweza kuwa na kinu, tukaweza kusindika unga, tukasaidia wale wenzetu wa Iringa katika kulisha nchi hii hata nchi jirani. Si kiwanda kwa ajili ya unga tu, tungeweza kuwa hata na viwanda vingi vya kuchimba madini, tunayo madini ya aina nyingi sana Mkoa wa Rukwa, lakini tungeweza kusindika hata samaki, tumezungukwa na Maziwa, Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa, tuna samaki wengi ambao wengi pia wanakaushwa tu kwa njia za kienyeji kupelekwa Gongo, Zambi, Malawi na sehemu nyingine lakini tungekuwa na umeme wa uhakika, tungeweza kuwa na viwanda vikubwa ambavyo vingeweza kusindika samaki, tungesindika unga, tunayo alizeti nyingi sana na ufuta tunalima. Yote haya ni kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa wa Rukwa, lakini bila umeme wa uhakika kwa kuendelea kutumia tu umeme wa jenereta, wenzenu Rukwa tutaendelea kuwa nyuma siku zote. Tunaomba basi, ile ahadi kwamba Mkoa Rukwa utapewa umeme wa uhakika wa Gridi ya Taifa, tunaomba basi hiyo ahadi itekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Wabunge hapa wanalalamika. Mwaka juzi wamezungumzia Gridi ya Taifa kwenda Rukwa, mwaka jana imezungumziwa, tunaona na sasa hivi iko kwenye mpango. Hatutaki tena kusikia mwakani, tunaendelea kuahidiwa Rukwa kupatiwa umeme wa uhakika. Tulikuwa tunaomba katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013, tuweze kupata umeme wa uhakika, Gridi ya Taifa kutoka Nyakanazi, Kigoma, Mpanda, Rukwa unaopita Tunduma kwenda Mbeya, Makete, Makambaku na kuishia Iringa, tulikuwa tunaomba na sisi tuweze kupata. Kwa kweli mimi nachelewa kusema kwamba naunga mkono hoja hii, nitaunga mkono hoja endapo Waziri wa Fedha atatutamkia wazi kwamba lini Mkoa wa Rukwa hii Gridi ya Taifa itatufikia na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapoambiwa kwamba ni mwezi fulani mwaka fulani yaani *timeline*, tuelezwe kabisa, hii ya kusema kwamba tutaleta, tutaleta kwa kweli tumechoka Rukwa. Tumechoka na ahadi na sisi tunahitaji maendeleo kama wengine, tumejikuta tuko kule mpakani, hatukupenda. Kwa hiyo, kwa kuwa mpakani isitufanye sisi tusahaulike kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kitabu cha bajeti cha Mheshimiwa Mgimwa, ukurasa wa 47 wametenga shilingi bilioni 498.9, sasa sijui kipaumbele cha hizi pesa ni kwenye umeme huu wa uhakika, hizi pesa zinapelekwa wapi? Tulikuwa tunaomba basi zipelekwe kwenye hiyo Gridi ya Taifa ili basi na Mkoa wa Rukwa tuweze kupata umeme wa uhakika kwa haraka kwa maendelo yetu na ni kwa maendeleo ya Taifa. Kama tunaweza tukasaidia nchi hii kwa chakula, je, tutakapokuwa tumepata viwanda mbalimbali, nchi hii itanufaika sana kutoka Mkoa wa Rukwa. Wapo wawekezaji wengi ambao wameanza kuonyesha nia ya kuja Mkoa wa Rukwa, lakini wanapokuja wanakuta umeme hakuna, umeme uliopo ni wa jenereta tu, mtu anaondoka kimyakimya na unakuwa na wasiwasi sijui kama watarudi hao. Tunaomba umeme wa uhakika *this time*. Kama vipaumbele basi huwa vinawekwa, tunaomba *first priority* ya umeme wa uhakika iende Rukwa na tungependa narudia tena, tuelezwe Rukwa tunapata Gridi ya Taifa lini, tutajiwe mwezi na mwaka ikiwezekana na tarehe kabisa ili tuendelee kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu wafugaji Mkoa wa Rukwa. Jamani wafugaji wahamiaji Mkoa wa Rukwa sisi hatuwakatai wala hatuwezi kuwafukuza, sisi wote ni Watanzania, lakini basi tunaomba ufugaji uwe wa tija. Mkoa wa Rukwa unalisha nchi nzima kwa sababu ya misitu mizuri iliyopo, mvua ya uhakika lakini sasa hivi ufugaji unaofanyika ni kama fujo, ni kama ya uchokozi vile sijui watu muongee kitu gani? Misitu inakatwa hovyo, ufugaji ni wa kiholela, wakulima hawaheshimiwi, tulikuwa tunaomba wafugaji, wafuge kwa tija, hatutaki kuona Rukwa inaingia kwenye jangwa. Kuna baadhi ya Mikoa mimi nilikuwa napita wakati nikiwa msichana kwenda shule, kulikuwa na misitu mizuri sana, lakini sasa hivi ni majangwa matupu na watu wanahama kwenye majangwa hayo. Sasa sisi hatutaki Mkoa wa Rukwa uwe ni jangwa. Maana Mkoa wa Rukwa utakapokuwa jangwa, basi tena, njaa itazidi hapa nchini. Kwa hiyo, tunawapenda wafugaji, lakini washirikiane na wakulima ili ufugaji wao uwe wa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niongelee ratiba ya vikao vya bajeti, sijui kama kuna *rigidity* gani kwamba hatuwezi tukabadilisha. Mimi nilikuwa nadhani vikao hivi vingeanza, kuna msemaji alisema vingeanza Aprili, vianze Aprili au Machi ili shughuli za Bunge zikifika mwishoni mwa Mei, Wizara zote zimeshapitisha bajeti zao, ili mwezi Juni basi iwe ni mwezi wa kuidhinisha fedha na Hazina kuanza ku-*release funds* kwenye Wizara na Halmashauri mbalimbali ili utekelezaji wa bajeti uanze Julai kwenye robo ya kwanza ya mwaka wa fedha. Ianze *July, August, September* utekelezaji unafanyika, ili basi hiyo taarifa iliyoandikwa kwenye Mpango wa Maedeleo wa Mheshimiwa Wasira kwamba *report* ya *first quarter* ianze kutoka *October*, iwe ni utekelezaji ambao umeshafanyika Julai, *August* na *September* lakini kama tunafika mpaka *August* hata Wizara nyingine bado hazijazungumziwa bajeti zao, ni taarifa gani ya mwaka wa fedha kwa robo ya kwanza, ni taarifa gani itakayoandaliwa mwezi wa kumi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Namwita Mheshimiwa Tundu Lissu na badala ya Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Amina Amour na Mheshimiwa Kafulila na Murtaza Magungu wajiandae.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipatia nafasi hii kujadili hoja hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kipindi kingine tena ambacho wengine wanakiita *silly season. Silly season*, muda wa mambo ya kipuuzi, *silly season*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka, tunakutana katika Bunge hili kuzungumza na kupitisha mambo ambayo tunajua hayatekelezeki. Serikali inakuja na bajeti, inakuja na ahadi ambapo yenyewe inajua hazitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wanasimama, wanasema wanaunga mkono mia kwa mia, kinachofuata ni kuponda hicho walichokiunga mkono mia kwa mia kwa sababu wanajua *deep down* ni uwongo, hakitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *this is another silly season. This is another season to lie to ourselves, to lie to our children, to lie to our country. We should be ashamed of ourselves. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikuja tena kwenye *silly season* ya mwaka jana, tukaambiwa na Serikali inayojua kwamba haya mambo hayatekelezeki, tukaletewa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano. Serikali inayojua kwamba haya mambo hayatekelezeki, ikatuambia kwamba kwa maneno yao, kwa maneno ya Mpango wenyewe, kuanzia sasa tutatenga shilingi trilioni 8.6 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo. Asilimia 35 Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, trilioni 43 *approximately*, tukaambiwa kwamba tutatenga kila mwaka shilingi trilioni 8.6 ili kutekeleza mpango huu, *another silly season*. Tukaitwa *St. Gasper* na Mheshimiwa Rais, tukalishwa, tukanyweshwa, tukapiga makofi, mwaka huohuo mwaka jana, badala ya kutenga shilingi trilioni 8.6, wakatenga trilioni 4.9, *silly season. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukahoji hapa, tukahoji kwamba mbona mmesema mtatenga shilingi trilioni 8.6, mbona mmetenga shilingi trilioni 4.9? Wakasema huu ni mwaka wa mpito. Sasa leo, tunakutana hapa kujadiliana juu ya Mpango wa Maendelo na bajeti ambayo imetenga shilingi trilioni 4.5 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo, tuliambiwa, tutatenga kila mwaka shilingi trilioni 8.6, *they knew they were lying, we knew they were lying; we should be ashamed of ourselves. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *we should be ashamed of this Government, we should be ashamed of this party, and we should be ashamed of these Members of Parliament* wanaopitisha *this kind of silly thing. (Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu naomba ukae. Mheshimiwa Lukuvi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu tu, namkumbusha *uncle* wangu, lugha hizi za kuudhi haziruhusiwi humu Bungeni, tafadhali sana. Naomba tu aendelee na mchango wake, lakini lugha za kuudhi, Kanuni zetu zinakataza, Kanuni ya 64.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, ninaamini una hoja nyingi nzuri, unaweza kuwasilisha vizuri na kila mmoja akaelewa, Kanuni ya 64 inatufunga kutumia maneno ya kuudhi wengine, naomba uchangie hoja zako kwa uzuri, Serikali inakusikia, naomba uendelee.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Mpango wa mwaka jana tuliambiwa kwamba, Serikali itaziba mianya ya ukwepaji kodi, itapunguza misamaha ya kodi. Hii lugha ni ya miaka mingi sana. Leo hii, mwezi huu, viongozi wetu wa kidini wa Baraza la Maaskofu Tanzania wa *Christian Council of Tanzania* na wa *BAKWATA,* wametoa ripoti wanaiita *The One Billion Dolar Question;* jinsi ambavyo Tanzania inapoteza fedha kutokana na mianya, ukwepaji na misamaha ya kodi ambayo imepitishwa na Bunge hili na kila mwaka tunaambiwa itashughulikiwa, lakini Serikali haifanyi hivyo, Wabunge wa Chama kinachotawala hawafanyi hivyo na wao ndio wenye *responsibility* kwa sababu, wao ndio wengi. Kwa hiyo, *this One Billion Dollar Question, this One Billion Dollar Disaster* ni *disaster* ya CCM *and nobody else. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa wasiofahamu historia ya mambo haya, mwaka 1998, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, alikuwa Waziri wa Madini, ndiye aliyeleta Muswada wa Sheria ya Madini hapa. Mimi sikuwepo hapa, Mzee Cheyo, alikuwepo na kwenye Muswada, kwenye mjadala wa kupitisha Sheria ya Madini ya Mwaka 1998, *Hansard* za wakati huo, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda na Mawaziri wenzake wakati huo waliliambia Bunge hili kwamba, sekta ya madini italiingizia Taifa hili 52% ya *revenue* yote inayotokana na madini; *we were told,* walituambia, walituahidi, leo hii viongozi wetu wa kidini wanatuambia katika mabilioni yanayotokana na madini yetu, tunapata *an average* dola milioni 100 kama kodi na mirahaba na vitu vinginevyo na wanasema kitu kingine kwamba, 65% ya hizo dola milioni 100 zinatokana na kodi za wafanyakazi. *Shame on this Government, shame on this party, shame on this people. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Samahani. Waheshimiwa ambao mnashabikia kwa kuongea, Kanuni zinatuzuia. Huruhusiwi kuongea, isipokuwa kwa idhini ya Mwenyekiti au Spika. Muacheni achangie vizuri, mtamshangilia huko nje.

Mheshimiwa Tundu Lissu, tafadhali!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumekuwa na dini mpya Bunge hili na kwa Serikali hii, tuna Miungu wapya na hawa Miungu wanaitwa wawekezaji. *They are our new Gods, they are untouchable;* kila kitu ukifanya, eeh, wawekezaji, eeh, wawekezaji, *don't touch them.* Hawa ndio Miungu wetu wapya, *what have they done for us out of other? No!* Madini wanatuambia, ni *product* inayoingiza *more foreign exchange than any other.* Hizo fedha mlizotuambia zitakuja ziko wapi,? *We have struck up and immerse riches off our cost. Natural gas,* kwa utaratibu wa hawahawa, wa chama hikihiki, wa Serikali hiihii, *natural gas* ambayo imegunduliwa *off our cost* itakwenda njia ileile ya dhahabu na *tanzanite. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi *I have lost faith completely* na Serikali hii. *I have lost faith* na chama hiki. *I have lost faith* na watu hawa. Nawaomba Watanzania, watuunge mkono katika hili. *There is obsolutely no future* kama nchi yetu itaendelea kuwa chini ya watu wenye rekodi ya aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie maana wengine wanataka kuzungumza. Mwalimu Nyerere kwenye kitabu chake cha 'Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania', alisema na wala hatuwajibiki kuendelea na chama na Serikali hii na kama tukiendeleanayo, mbele ni giza tupu, majuto ni mjukuu. Watanzania wenzangu hatuhitaji kuendelea na chama hiki, hatuendelei, hatuhitaji kuendelea na *this kind of silly* na vitu ambavyo ni vya uongo, havitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sio kampeni.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema bajeti hii haijalenga kumsaidia mwananchi wa kawaida na suala la kupunguza makali ya maisha itakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kusema siungi mkono bajeti hii. Siiungi mkono bajeti hii kwa sababu, mengi ambayo tuliyapendekeza yatekelezwe ni 1% tu ndio yaliyotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza naanza kuzungumzia mishahara hewa. Nilizungumzia mishahara hewa kwa watumishi hewa bajeti iliyopita na Serikali ilitoa ahadi kuwa, itaweka siku moja maalum, itafuatilia na itapatiwa ufumbuzi wa hawa watumishi hewa. Cha kusikitisha, hiki kitabu chote hakijaeleza kuhusu watumishi hewa; sijui kwa kuwa hawajafanya kazi hiyo au sijui inakuwa vipi? Sasa kama ndio hawajafanya kazi hiyo, lakini angalau wangetueleza kwa mwaka huu wamepata watumishi hewa wangapi na pia kwa mwaka huu wameweza kuokoa pesa ngapi za watumishi hewa? Kwa hiyo, namwomba Waziri atueleze jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilitaka kuzungumzia sekta ya uvuvi. Tangu mwaka 2003 Kambi ya Upinzani ilikuwa inasema kuwa tujielekeze kwenye uvuvi, lakini mpaka hii leo, Serikali imekaa kimya na haijafanya chochote kwenye uvuvi. Sijui kwa nini, kama mwanzo walikuwa na wasiwasi kwa kuwa samaki hawapo wengi, lakini ilidhihirika katika samaki wa Magufuli, samaki chungu nzima walivuliwa na Japan na wakaenda kukamatwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwekeze kwenye uvuvi, tutaweza kukusanya mapato ya kutosha na hivyohivyo tutaweza kupata ajira za kutosha. Katika ajira 12,000,000 ajira 4,000,000 ni za sekta ya uvuvi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ilione jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninataka kuzungumzia ukurasa wa 17, Serikali imesema, kutakuwa na mkopo kwa ajili ya ujenzi wa umeme wa *megawatt* 60, Nyakato Mwanza. Suala hili lilikuwa kwenye bajeti iliyopita, sasa ninataka kuiuliza Serikali, je, ni lini itafanya ujenzi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye ukurasa wa 28, hapa kuna suala la kufunguliwa kwa Benki ya Maendeleo, hii imekuwa ni hadithi ya kila siku. Nataka Serikali ituambie ni mwezi gani na tarehe gani itafunguliwa hii Benki ya maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 37, kipengele cha 9, Serikali imesema, kuimarisha utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, *PPP,* ili kupanua fursa ya kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, huu umekuwa wimbo wa kila siku. Kwanza, tulikuwa tunasema kwa kuwa Sheria bado, Kanuni bado, lakini sasa hivi yote yameshakuwa tayari. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye haraka suala hili kwa kuwa, sekta binafsi ndio inachangia mapato ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija hapa kwenye suala la misamaha ya kodi, hii nimeshaizungumzia asubuhi na ninaomba Waziri anijibu swali langu hili nililoliuliza asubuhi ambapo niliambiwa nije niliulize katika bajeti. Suala lenyewe linasema je, Serikali iko tayari kuleta programu inayoonesha utekelezaji wa mpango wa kupunguza misamaha ya kodi? Kwa hivyo, ninaiomba hiyo progarmu utupatie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 39, kipengele cha 5, tunaendelea kupitia mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya majengo. Kila siku tunaangalia majengo makubwa makubwa

yanajengwa Dar-es-Salaam na nje ya miji, lakini ukitizama pesa zinazopatikana katika kodi ya majengo ni kidogo mno. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ikae kitako chini, iweke mfumo mzuri ambao utawezesha kupatikana pesa nyingi za majengo kwani kupatikana pesa hizi, kutaweza kuongeza mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija ukurasa wa 54, kukabiliana na mfumuko wa bei. Kwa kuwa, sasa hali imeshakuwa mbaya katika nchi hii, naiomba Serikali hii miezi mitatu iliyokuwepo iweze kununua sukari na mchele kwa haraka badala ya kutegemea uzalishaji. Hii miezi mitatu inunue mchele na sukari kwa haraka ili kukabiliana na huu mfumuko wa bei maana tukianza kuzalisha itachukua miezi sita na saba na sasa hivi hali imeshakuwa mbaya. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilione hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 71, hapa kuna mambo ya kodi. Kuna magari ambayo yana kikomo cha miaka 10, hayaruhusiwi tena ila yanaruhusiwa magari yenye kikomo cha miaka 8. Haya magari ya kikomo cha miaka 10 ndio wanayonunua wanyonge kwa sababu yanakuwa nafuu. Kwa hiyo, kuyakataza yasije na kuongeza ushuru wa 20% ni kuwakomoa wanyonge. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, hili suala lirudi kama lilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika ukurasa wa 72, ambapo ni wa mwisho namalizia, kuna haya majina ya magari, mtu anayetaka kuweka majina yake kwenye gari na umeshafanya tathmini kuwa utapata majina 10 na kila jina litakuwa shilingi 5,000,000/=, ni kwa nini isiwe shilingi 300,000/= tukapata watu 1,000 na ikawa *total* ya shilingi milioni 300? Kwa hiyo, naishauri Serikali ipunguze hii bei isiwe shilingi 5,000,000/= badala yake iwe shilingi 300,000/= ili tupate pesa nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninataka kuzungumzia habari ya ajira. Mheshimiwa Waziri, naona mpaka sasa hivi suala la ajira, vijana hatujawapa kipaumbele. Naomba sasa hivi vijana tuwaelekeze kwenye kilimo cha kisasa. Vijana wengi wako mijini hawana kazi yoyote wanapita wakiranda, badala ya kuwahamasisha kwenda vijijini tukaweza kuwapa ajira ya kilimo, lakini wameachwa hovyo, wanaranda hovyo, wanapita wakifanya mambo yasiyokuwa na maana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijielekeze kwenye kilimo na kilimo cha kisasa na iweze kuwapatia mikopo na pembejeo na mashine za kisasa waweze kulima, ili tuongeze kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nizungumzie kuhusu mafuta ya kupikia, mafuta ya alizeti. Mafuta ya alizeti, tulizungumza katika kipindi kilichopita cha bajeti na Mheshimiwa Waziri akaahidi kuwa, tutavuna mafuta ya alizeti ya kutosha na wala hatutaagiza tena nje mafuta ya alizeti lakini naona mpaka hivi sasa jambo hilo halijafanyika, isipokuwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nizungumze na Watanzania. Awali ya yote, Watanzania wanatakiwa wawe makini sana na waigizaji. Ukimpata mwigizaji mzuri, unaweza ukalia, kumbe mwenzio anaigiza na hiki ndicho ambacho kimetokea muda mfupi uliopita hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nakuomba ufute neno uigizaji.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta kama kuna waigizaji hapa.

**MWENYEKITI:** Naomba ufute neno uigizaji.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta neno uigizaji kama kuna waigizaji, lakini maana ya kusema hivi ilikuwa ni hii, tatizo linalojitokeza hapa ni kwamba, bajeti imeandaliwa na wataalam, lakini watu badala ya kuuliza wajue undani wa bajeti, aliyesomea Sheria za Mambo ya Kichawi na yeye anakuwa mchambuzi wa uchumi, mwenye uzoefu wa kuendesha disko anakuwa mchambuzi wa uchumi, unawachanganya Watanzania. Sasa uhalisia ndio huu, mimi ni Mchumi wa Daraja la Kwanza na Mwandamizi wa Benki Kuu ya Tanzania, ngojeni niwaambie uhalisia wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, tunapoongelea 35%, tunajumuisha pamoja na uwekezaji kwenye sekta ya elimu lakini tunapozungumzia bajeti hii ya leo, sekta ya elimu iko pembeni, fedha zake zimewekwa pembeni, zile za maendeleo zimewekwa pembeni. Watanzania tuulizane, hivi kweli tunaposomesha wanafunzi vyuo vikuu, hatuwekezi? Hivi kweli tunapojenga maabara, hatuwekezi? Hivi ni kweli tunaposomesha vyuo, tunapoandaa Wataalam wa Ugani, tunapoandaa Madaktari, hatuwekezi? Tulisoma wapi? Hiyo Sheria iliyokuwa inatenga *investiment on human capital,* ilikuwa ni ya miaka ya 50 na 60 lakini ukisoma David Roma, ukasoma Waive, ukasoma Mankyu, miaka ya 90, *Cop Douglas Production Function,* inatambua *human capital* kama *investiment.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mpango wa Maendeleo huu tunaojadili, umejumuisha *investiment on human capital* ndio ukapata 35%. Ukienda kwenye bajeti ya mwaka huu, ukichukua *investiment* kwenye elimu, uwekezaji tuliouweka kwenye elimu, bajeti ya maendeleo inaenda 39% kwenda 40%. Mmesoma wapi nyie? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ukiingalia kiutaalamu tu bajeti yenyewe, kiutaalamu tu, *dependency ratio,* utegemezi bajeti imepungua. Ukiweka na ile mikopo kwa sababu mikopo nayo ni fedha yetu tutalipa, ukiondoa na ile ya mikopo, utegemezi kwenye bajeti imebaki 6.5%. Sifa nyingine ya bajeti, ukienda zile fedha zinazoenda kwenye kulipa mishahara, hamna hata senti moja inayoenda kwenye mishahara, mishahara inalipwa na fedha za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu muone sasa hili nililolisema ambalo mmesema nilifute, hebu oneni sasa Bajeti ya Kivuli, wameandika kwamba, kima cha chini kitakuwa 315,000/= hawajui wanaolipwa kima cha chini ni wangapi, zidisheni mpate hesabu, mimi nitawaambia mwishoni. Halafu chukueni Walimu muwapandishie mishahara mara 50, chukua Madaktari uwapandishie mara 50, chukua Manesi uwapandishie mara 50, tafuta jumla yake. Halafu chukua walewale, makundi matatu haya, uwapandishie mara moja na nusu, bajeti ya matumizi inaenda zaidi ya hii shilingi bilioni tisa waliyoandika wao. Hii waliyoandika kwenye matumizi ya kawaida inazidi, ukijumlisha na ile wanayosema kwamba watalipa pensheni kwa wazee, hawajui idadi ya wazee, ukijumlisha inakuwa zaidi ya shilingi trilioni 15, mmnatumia bajeti ya wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wanasema...

**MBUNGE FULANI:** *Silly thinking.*

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hili nitalirudia tu, halafu wanasema kujenga, wanasema kupunguza mzigo wa matumizi ya magari. Mwaka jana Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Mbowe, alirudisha gari akisema kwamba, kupunguza matumizi, akawahadaa Watanzania. Baada ya muda fulani, kumbe alilikataa lile gari kwa sababu limechakaa, lilikuwa linatumiwa na Kiongozi aliyepita, baada ya muda fulani kachukua kimyakimya gari lingine analitumia. Amelirudisha kimyakimya hajawaambia Watanzania kama ameshalichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wanatakiwa kwa kweli Wachamungu wote, mimi tangia nizaliwe sijawahi kuona Kambi ya Upinzani yenye pepo mtaka vyeo kama hawa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatakiwa waombewe, watalipeleka Taifa pabaya, mimi nawaambia Watanzania mkiendelea kushabikia watu ambao haijulikani kama wako *normal* au wanatakiwa wawe Mirembe mtapata kiongozi kama Iddi Amini hapa.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MBUNGE FULANI:** Mwehu huyu!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo! Anatutukana huyu!

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Nimesema niseme na Watanzania, ngojeni niwaambie, jambo lingine ambalo wanalolikataa hapa, ngojeni mjue unafiki uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wanalolikataa wanaongelea *OC* kama vile ni dhambi kubwa kwelikweli, angalieni *OC* kuna nini, *OC* Serikali imetenga shilingi bilioni 140 kupeleka vijana JKT, hivi kweli hiyo ni dhambi kupeleka vijana JKT. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Serikali imetenga *OC* kwenda kwenye Tume ikakusanye maoni ya Katiba Mpya, mnataka Katiba Mpya hamtaki tuweke bajeti, mnataka Katiba mpya kwa kutumia fedha gani.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Serikali imetenga fedha kwenye *OC* kwa ajili ya sensa, mnataka sense, hamtaki tuweke bajeti. Serikali imetenga fedha kwenye *OC* kwa ajili ya fidia za watu wanaondolewa kwenye maeneo kupisha miradi ya maendeleo, mnataka zisiwekwe, wale watu mtawapatia hela gani mnapowaondoa pale? Serikali imetenga fedha kwenye *OC* kwa ajili ya chakula, wanafunzi, wafungwa, wagonjwa mnataka ziondoke mtawapa nini? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mimi sijawahi kuona Bajeti Kivuli ya aina hii, *this is concisely and precisely rubbish. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Samahani kaa chini, Mheshimiwa naomba ukae.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja*. (Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Ngojea Mheshimiwa Mwigulu, *order in the House*, Mheshimiwa Mwigulu naomba ufute neno pepo kwa sababu ni kinyume…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea)*

**MWENYEKITI:** *Order in the House.*

**MBUNGE FULANI:** Mbona walipotaja Mungu mpya hukusema?

**MWENYEKITI:** *Order in the House.*

**MBUNGE FULANI:** Afute.

**MWENYEKITI:** *Order in the House,* naomba ufute neno pepo halafu tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu futa neno pepo tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa humu ndani nafuta lakini watu wa aina hiyo wakaombewe, nafuta neno hilo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Naomba tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Naomba tuendelee, sasa namwita Mheshimiwa Ahmed Ally Salum na Mheshimiwa Amina Clement ajiandae na atafuatia Mheshimiwa Komba. Yupo au hayupo?

**MBUNGE FULANI:** Yupo!

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza kabisa nashukuru sana nilitoka juzi tu Jimboni, kuna matatizo makubwa sana ya bodaboda na baiskeli lakini naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wake na kufuta kabisa matatizo ya bodaboda na ningeomba sana Serikali iende mbele zaidi kwenye baiskeli pamoja na *taxi*, hawa wote nao wakafutiwe ushuru ili wafanye kazi vizuri waweze kuwa na mapato mazuri katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ya mwaka huu 2012/2013, siyo mbaya sana lakini naomba niongelee kwenye maeneo mawili matatu. Naomba Serikali izingatie na ikumbuke kwamba mwaka 2009/2010, fedha ambazo tulipitisha Bungeni hapa mpaka kufikia mwisho wa mwaka ule hazikufika karibu asilimia 30, mwaka 2010/2011 hivyohivyo, mpaka tunaishia sasa hivi asilimia 42 ya fedha ambayo tulipitisha kwa ajili ya bajeti ya maendeleo yetu mpaka hivi sasa hazikufika kwenye Halmashauri zetu. Kibaya zaidi hatuelezwi ni tatizo gani, hatulezwi kwamba hizi fedha zilitumika namna gani, tunaingia kwenye mwaka huu wa fedha 2012/2013 wasiwasi wangu tena mpaka tufike mwakani tuambiwe tena asilimia 40 ama 35 haziji. Hivi sasa hebu Serikali itoe ufafanuzi iseme kwamba zile fedha tunazipata ama hatuzipati, ionyeshe *commitment* ya fedha ambazo hatujazipata kwa miaka mitatu yote iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kwa stahili hii sisi Wabunge wa Majimbo ndiyo tunaongea na wananchi kule, maswali yote tunaulizwa sisi kule, Ilani ya CCM ndiyo tunaitekeleza kule, sasa kama fedha hizi hazitoshi ni muhimu sana Serikali ikaona ni namna gani ya kuweza kutuongezea. Kwa mfano mimi peke yangu tu kwenye Jimbo la Solwa, ziko zahanati 12 ambazo ziko tayari kabisa kupauliwa na kuanza kazi lakini fedha tulizozipata mwaka huu tunatengeneza zahanati mbili tu na vituo vya afya viwili, ina maana zahanati zile 10 tunazi-*postponed* kwa mwaka wa fedha ujao tupate fedha mwakani ili zifanye kazi hiyo iliyokusudiwa. Katika miradi ya *World Bank* kuna visima 15, tumepata viwili tu, tuna tatizo la maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hapa nipewa taarifa kuna *one billion* kwa maana ya *consultation* lakini *2.2 trillion* kwa maana ya kupeleka kwenye maendeleo ni kidogo sana. Ni muhimu sasa Serikali angalau ikaenda kama ilivyofanya mwaka jana hii *two point seven, five hundred billion* Serikali ikienda kujibana vizuri kwa maana ya *OC* hizi za kwenye Wizara ndogondogo, fedha hizi zipatikane zielekezwe kwenye maendeleo kule. Haitakuwa jambo la busara kama kila mwaka kwa mfano tunatengeneza visima viwili vya *World Bank*, mwaka unakuja visima viwili ina maana tunabakiza miaka mitatu visima sita tu, visima vinane tunakwenda 2015/2020 kule, wananchi walioko vijijini hawaelewi masuala haya zaidi ya kuona mambo yao na kero zao zinatatuliwa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za rada, shilingi bilioni 83 za rada zimepangiwa kwamba shilingi bilioni 60 iwe vitabu, shilingi bilioni 27 iende kwenye madawati. Halafu juu ya hivyo ni kwamba wamechagua maeneo, mimi naishauri Serikali kwamba fedha za rada hizi zigawanywe kwa mgawanyo ulikuwa wa uwiano kwenye Halmashauri zote Tanzania na Halmashauri ziseme

wanahitaji nini kutokana na mgao wao wa fedha hizi za rada badala ya kuchagua Halmashauri mbili tatu au tano na kuziacha Halmashauri zingine. Katika hizi fedha za rada tumesikia kama TAMISEMI kuna huyu mtu mmoja tu wanayemwita bila kuwa na *competitive tender* kitu ambacho inaweza kule mbele ya safari ikawa ni kashfa kubwa sana na skendo. Kwa hiyo, mimi naomba sana ufuate sheria na Halmashauri zote zinufaike na fedha hizi za rada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba, naomba sana wananchi wakulima wa pamba, wakulima wa pamba msiuze pamba zenu kama alivyosema Mheshimiwa Cheyo, *no one* ***book*** *no* pamba, nawaombeni sana. Mheshimiwa Ndassa hapa ameongea na mimi naunga mkono, nasema wauzaji wote mnaolima pamba hata mimi kwenye Jimbo langu kuna Kata kama tatu, nne zinalima pamba, kero ni bei, kuna ujanja wanaofanya wafanyabiashara wa pamba nje ya nchi wana-*release* pamba kwenye soko la dunia bei ikishuka wanakuja kuwahi kununua, wakinunua hizi wakija kufanya *average* wanapata kwa kilo moja shilingi 820 *solution* ndogo tu, wakulima muuze pamba kidogo kwa mahitaji yenu, nyingine muweke *stock*, mwezi wa kumi, kumi na moja bei itapata tu mpaka shilingi 1000.

**MBUNGE FULANI:** Haiozi!

**MHE. AHMED A. SALUM:** Haiozi pamba, nawaombeni sana wakulima muungane na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, fedha kwenye suala la kilimo ni kidogo sana. Mimi kwenye Jimbo langu asilimia 95 wote ni wakulima, suala la Kilimo Kwanza mimi sijaliona kwenye Jimbo langu. Kubwa zaidi naomba sana fedha ambazo tumeziweka kwenye *TIB, TIB Bank* wanafanya kazi nzuri sana lakini wakulima wetu bado hawakopesheki, sasa Serikali iingilie kati.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Ya mwisho hiyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa nakushukuru sana.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, namwita sasa Mheshimiwa Amina Clement na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Capt. John Komba.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nishukuru kwa kunipa nafasi nichangia bajeti hii.

Kwanza nikuambie mimi nafikiri moja ya masharti ya kuingia humu ndani tuwe tunapimwa akili kama wote tuna akili sawasawa au namna gani, inawezekana watu waliambiwa waende Mirembe halafu waje humu, wameanzia humu kabla ya kwenda Mirembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili litajirudia sana maana huwezi kusema kila mwaka tunashuhudia upuuzi humu ndani, tunapanga bajeti ya upuuzi humu ndani, mwaka jana upuuzi, mwaka huu upuuzi na yeye yumo humuhumu ndani, anakaa humu, huu ni wendawazimu kabisa. Ni vizuri tukapimana akili kidogo wa Mirembe wakaenda Mirembe, halafu wakarudishwa hapa wakawa wamesharekebishwa katika ugonjwa.

**MBUNGE FULANI:** Tuanze na wewe.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Maana yake inapotukanwa, hapa hakitukanwi chama chochote hapa, lakini mtu anaposimama anazungumza habari jamani wananchi acheni CCM, hii siyo kampeni humu ndani, humu tujadili habari ya bajeti hii. Kama ulishindwa kupata watu wengi huko ulikotoka miaka miwili iliyopita wananchi wale ndiyo wameipa CCM ridhaa ya kutawala miaka mitano, sasa unapowatukana wananchi wale mimi ndiyo nauita ukichaa. Kwa hiyo, ni vizuri watu wakapimwa kwanza kabla hawajaingia humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naangalia sana hizi *TV* za nje, *UBC* ya Uganda, *KBC* ya Kenya, naangalia Wabunge wa Uganda na wa Kenya wanaisifu bajeti yetu tumejali wanafunzi, tumejali barabara, tumeleta matrekta wanayaona na wanaizungumza kila siku lakini sisi tunaiponda hiyo bajeti halafu tunasema bajeti yetu ni kujirudia mwaka hadi mwaka. Ni lazima irudiwe kwa sababu sisi kazi yetu ni kusaidia wananchi lazima tuwasemee wananchi jana, kesho, kesho kutwa tutawazungumza tu, wanafunzi watazungumzwa mwaka jana, mwaka huu, mwakani kwa sababu ndiyo lengo la kuwakomboa wanafunzi na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimeitwa ghafula niende kwenye Jimbo langu, Jimbo langu ni maskini...

**WABUNGE FULANI:** Ohoo! Hapohapo.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Jimbo langu ni maskini, katika Wilaya ya Mbinga, lile Jimbo ambalo limetengwa ndiyo Jimbo maskini, lakini bahati mbaya sana wenzetu wanaofanana na sisi wa Malawi ndiyo wanaozalisha samaki kupeleka nje, ziwa lilelile huku hakuna samaki lakini upande ule wanazalisha samaki, wanapaki kwenye makopo wanapeleka nje. Mimi silaumu sana Serikali yangu kwa sababu Malawi ni nchi ndogo sana, Malawi inaingia kwenye nchi yetu zaidi ya mara kumi, kwa hiyo, katika nchi wengine walipendelewa mapema, watu wa Kaskazini walipata, watu wa katikati walipata, mashariki walipata sasa bajeti hii ilenge sisi watu wa pembezoni kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa akizungumza siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa kule Mbinga Magharibi kule ama kule Nyasa tunategemea bandari ya Bambabay, lakini ukiangalia bandari ya Bambabay haijapewa pesa hata senti tano sasa maendeleo yatakujaje? Kama unatengeneza bandari ya Mtwara unataka bidhaa ziende Malawi, Zimbambwe, Botswana, Namibia, South Afrika, Kongo, zitakwendaje kama bandari ya Bambabay haiwezi kupitisha mizigo hiyo? Kwa hiyo, naomba sana bandari yetu ya Bambabay ipewe umuhimu wa kwanza kama zilivyo bandari zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa letu la Nyasa, ni Ziwa ambalo vifaa vyake ni duni na kwa vile sisi tulikubali kuwasaidia watu wa Kaskazini tulikuwa tunawalimia mashamba, maana tunalima mahindi wanakula wao, tunalima maharage wanakula wao, tunalima mchele wanakula wao, sasa ni wakati wa kusaidia watu wale waweze kuvua vizuri samaki ili wale vizuri, tena na hao tunawapelekea maana samaki wako, vyombo vya kuvulia ni duni, teknolojia ni duni. Tunaomba sana bajeti hii ilenge kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo wanaokaa kandokando ya Ziwa Nyasa na pia na maziwa mengine kwa mfano Rukwa, Tanganyika, Nyumba ya Mungu wapi wasaidiwe hao, maana tumeshawasaidia sana Ziwa Victoria, kila siku, maana hata siku hizi nikiangalia wanavyotoa habari ya hali ya hewa wanazungumza halafu wanasema Ukanda wa Ziwa, hivi sisi Tanzania tuna Kanda moja tu maana yake ni Ziwa Victoria basi uko Ukanda wa Ziwa Victoria, Ukanda wa Ziwa Nyasa, Rukwa haya maziwa haya nayo yana ukanda wa ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba sana kutukanana tukuache, maana yake tumeshaona huko katika Mabunge mengine watu wanapigana ngumi, sasa huku tunakoenda tutapigana ngumi na ngumi zilizo upande huu ni nyingi kuliko za upande huu mtakufa. Kwa hiyo, naomba sana heshimu chama cha wenzako, heshimu chama kilicho madarakani, heshimu wananchi waliotoa madaraka hayo, changia hoja yako, vunja hoja iliyoko siyo kutakana Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na uwe unaangalia pande zote wanaotukana sana hawa uwaambie ndiyo watoe maneno, lakini yule uliyemwambia atoe neno lile neno halina sababu ya kulitoa. Wanaotukana hawa ndiyo uwaambie, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Tumebakiwa na dakika kama sita hivi sasa kama Mheshimiwa Kafulila utakuwa tayari uongee, kama hauko tayari basi niahirishe kikao. Mheshimiwa Kafulila!

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukubwa wa agenda hii ya bajeti, naomba nichangie kesho kwa sababu dakika sita ni chache sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru na naomba kuwataja ambao kesho wataanza asubuhi, tutaanza na Mheshimiwa Prof. Kahigi, atafutiwa na Mheshimiwa Mussa Kombo, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa David Kafulila na Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

Baada ya kuwataja hao, naomba kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ahsanteni sana.

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 19 Juni, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*